Elimu ya Dini ya Kiislamu

Madrasa na Shule za Msingi

# Kitabu cha Saba



Islamic Propagation Centre

# Elimu ya Dini ya Kiislamu

## Madrasa na Shule za Msingi

# KITABU CHA SABA

Islamic Propagation Centre

Toleo la Kwanza 2005

Islamic Propagation Centre (IPC)
S.L.P 55105, Dar es Salaam, Tanzania.

©Hakimiliki 2005 IPC

Elimu ya Dini ya Kiislamu
Madrasa na Shule za Msingi
Kitabu cha Saba

Wachapaji/Wasambazaji
Islamic Propagation Centre (IPC)
S.L.P 55105, Dar es Salaam, Tanzania.
Chapisho la Kwanza, 02, May, 2005
Nakala 1000

Kimetayarishwa na Islamic Propagation Centre
P.O.BOX 55105, simu 022-22450069.

Usanifu wa kurasa na Jalada: Islamic Propagation Centre.

بسم الله الرحمن الرحيم

# Neno la Awali

Shukrani zote njema anastahiki Allah (s.w). Rehema na Amani zimwendee Mtume Muhammad (s.a.w) na wale wote wanaofuata njia yake.

Tunamshukuru Allah (s.w) kwa kutuwafikisha kutoa kitabu hiki cha Saba kwa ajili ya watoto wetu wa Madrasa na Shule za msingi. Kitabu hiki ni katika mfululizo wa vitabu saba kwa ajili ya Madrasa zetu na shule za msingi.

Vitabu hivi vimeandaliwa kwa lengo la kuwawezesha watoto wa kiislamu kupata elimu ya msingi ya dini yao katika fani za Qur'an, Tawhid, fiqh, akhlad na tarekh.

Tunamuomba Allah atujaalie kulifikia lengo lililokusudiwa na atujaalie sisi na watoto wetu kuwa makhalifa wa Allah (s.w).

Wabillah Tawfiq

Mwalimu Mratibu
**Islamic Propagation Centre**

## Yaliyomo

1. Somo la Kwanza……………………………………………………1
Hukumu za usomaji Qur-an……………………………………1
Vituo vya kusimama wakati kusoma Qur-an……….1
Aina na usomaji wa Hamzah………………………….5
Hukumu za Qalqaalah……………………………………9
Hukumu za Mim na Nun zenye shadda…………….11
Hukumu za Mim sakna…………………………………13
Zoezi la Kwanza………………………………………………16

2. Somo la Pili…………………………………………………………17
Imani ya Kiislamu……………………………………………17
Maana ya Imani katika Uislamu………………………17
Ni yupi muumini wa kweli?……………………………18
Maana ya kumuamini Allah (s.w.)……………………22
Maana ya kuamini Malaika……………………………27
Maana ya kuamini vitabu vya Allah (s.w.)…………28
Maana ya kuamini Mitume wa Allah (s.w.)……….28
Maana ya kuamini siku ya mwisho…………………29
Maana ya kuamini Qadar ya Allah (s.w.)………..30
Maana na aina za Dini……………………………………31
Zoezi la Pili……………………………………………………42

3. Somo la Tatu…………………………………………………………43
Kuhifadhiwa Sunnah ya Mtume……………………………43
Njia zilizotumika kuhifadhi Sunnah)…………………43
Historia fupi ya Uandishi wa Hadith…………………45
Vigezo vya Hadith Sahihi………………………………49
Kuna aina kuu mbili za Hadith…………………………51
Zoezi la Tatu……………………………………………………53

4. Somo la Nne…………………………………………………………54
Lengo la Maisha ya wanadamu…………………………54

Kwanini watu wameumbwa?..............................54
Maana ya Ibada katika Uislamu.........................54
Lengo la nguzo za Uislamu...............................55
Kusimamisha Swala wakati wa Dharura..............60
Mambo yanayopaswa kufanyiwa maiti...............65
Zoezi la Nne..................................................................77

5. Somo la Tano.................................................................78
Sifa za Muumini katika Qur-an.......................................78
Suratul-Mu-uminun (23:1-11,57-61)...................78
Suratul Al-Furqaan (25:63-77)............................81
Suratul Al-Ma'arij (70:19-35)..............................87
Surat Ttawba (9:71,111-112)..............................89
Surat Ar-Raad (13:19-29)...................................93
Surat As-Sajadah (32:15-17)..............................97
Surat Al-Ahzab (33:35-36).................................98
Surat Ash-Shuura (42:36-43)...........................100
Surat Al-Fat-h (48:29)......................................102
Surat Al-Hujurat (49:15)...................................103
Zoezi la Tano...............................................................105

6. Somo la Sita................................................................106
Uislamu baada ya Makhalifa.......................................106
Dola ya Banu Ummaiya...................................106
Utawala wa Banu Abbas..................................109
Maimamu wanne wa Fiq-hi..............................110
Upinzani wa Wakristo dhidi ya dola ya Kiislamu..111
Harakati za Kuhuisha Uislamu..........................112
Kuingia Uislamu Afrika Mashariki.....................118
Zoezi la Sita.................................................................125

Somo la 1. Qur'an

# Hukumu za Usomaji Qur'an

**Umuhimu wa kusoma Qur'an kwa hukumu**

Waislamu tumeamrishwa kuisoma Qur'an vilivyo, kuizingatia na kuifuata katika kuendesha maisha ya kila siku.

وَرَتِّلِ ٱلْقُرْءَانَ تَرْتِيلًا

*"...... na Soma Quran vilivyo"*. (73:4).

Kusoma Qur'an vilivyo ni pamoja na kuzingatia hukumu mbali mbali za usomaji ili kuipatia maana iliyokusudiwa na kuitekeleza inavyostahiki.

**Alama na vituo vya kusimama wakati wa kusoma Qur'an.**

**Meem** (م)

Ni kituo ambacho msomaji analazimika kusimama.Katika kituo hiki neno la Qur'ani pamoja na maana yake vinatowa ujumbe kamili wa maudhui ya kipande cha aya.

Mfano: (1) Baqarah (2:26)

وَأَمَّا ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ فَيَقُولُونَ مَاذَآ أَرَادَ ٱللَّهُ بِهَـٰذَا

مَثَلًاۘ

Mfano: (2) Annisaai (4:171)

إِنَّمَا ٱللَّهُ إِلَـٰهٌ وَٰحِدٌ ۖ سُبْحَـٰنَهُۥٓ أَن يَكُونَ لَهُۥ وَلَدٌ ۘ

Mfano: (3)Almaaidah (5:73)

لَّقَدۡ كَفَرَ ٱلَّذِينَ قَالُوٓاْ إِنَّ ٱللَّهَ ثَالِثُ ثَلَـٰثَةٖۘ

Mfano: (4)Al an a'm (6:20)

ٱلَّـذِينَ ءَاتَيۡنَـٰهُـمُ ٱلۡكِـتَـٰبَ يَعۡرِفُونَـهُۥ كَمَا يَعۡرِفُـونَ

أَبۡنَـآءَهُمُۘ

Mfano: (5)Al Ankabuut (29:26)

فَـَٔـامَنَ لَـهُۥ لُـوطٞۘ

Alama ya ***meem*** inayomuashiria msomaji kusimama huweza kuwa juu ya herufi ya kusimamia (kama ilivyo kwenye mifano) au ikawa mbele ya herufi hiyo.

**Vituo ambavyo msomaji anaweza kusimama au kuendelea**

**Qalyi (قلي)** ni kituo ambapo ni vyema msomaji wa Qur'an akasimama, kisha akaendelea kusoma kipande cha aya kinachofuata.

Mfano: (1) Al Baqarah (2:263)

قَوۡلٞ مَّعۡرُوفٞ وَمَغۡفِرَةٌ خَيۡرٞ مِّن صَدَقَةٖ يَتۡبَعُهَآ أَذٗىۗ

Mfano: (2) Fatir (35:31)

وَٱلَّذِيٓ أَوۡحَيۡنَآ إِلَيۡكَ مِنَ ٱلۡكِتَـٰبِ هُوَ ٱلۡحَقُّ مُصَدِّقٗا

لِّمَا بَيۡنَ يَدَيۡهِۗ

Mfano: (3) Al an'am (6:126)

وَهَٰذَا صِرَٰطُ رَبِّكَ مُسۡتَقِيمٗاۗ

Mfano: (4) An-naml (27:59)

قُلِ ٱلۡحَمۡدُ لِلَّهِ وَسَلَٰمٌ عَلَىٰ عِبَادِهِ ٱلَّذِينَ ٱصۡطَفَىٰٓۗ

Mfano: (5) Ash shuura (42:17)

ٱللَّهُ ٱلَّذِيٓ أَنزَلَ ٱلۡكِتَٰبَ بِٱلۡحَقِّ وَٱلۡمِيزَانَۗ

**Salyi (صلي)** ni kituo ambapo ni vyema msomaji akaendelea kusoma badala ya kusimama.

Mfano: (1) Al Maaidah (5:8)

ٱعۡدِلُواْ هُوَ أَقۡرَبُ لِلتَّقۡوَىٰۖ وَٱتَّقُواْ ٱللَّهَۚ

Mfano: (2) Al Maaidah (5:27)

وَلَمۡ يُتَقَبَّلۡ مِنَ ٱلۡأٓخَرِ قَالَ لَأَقۡتُلَنَّكَۖ قَالَ إِنَّمَا يَتَقَبَّلُ

ٱللَّهُ مِنَ ٱلۡمُتَّقِينَ ٢٧

Mfano: (3) Al-Isra (17:32)

وَلَا تَقۡرَبُواْ ٱلزِّنَىٰٓۖ إِنَّهُۥ كَانَ فَٰحِشَةٗ وَسَآءَ سَبِيلٗا ٣٢

Mfano: (4) Al-Jinni (72:2)

يَهۡدِيٓ إِلَى ٱلرُّشۡدِ فَـَٔامَنَّا بِهِۦۖ وَلَن نُّشۡرِكَ بِرَبِّنَآ أَحَدٗا

Mfano: (5) Al-Insaan (76:13)

مُّتَّكِـِٔينَ فِيهَا عَلَى ٱلْأَرَآئِكِ ۖ لَا يَرَوْنَ فِيهَا شَمْسًا
وَلَا زَمْهَرِيرًا ﴿١٣﴾

**Jeem (ج)** ni kituo ambapo ni sawa kwa msomaji akiamuwa kusimama au kuendelea, kwakuwa maana ya neno la Qur'an haipotei wala kukatika.

Mfano: (1) Al-Mutaffifiina (83:26)

خِتَٰمُهُۥ مِسْكٌ ۚ وَفِى ذَٰلِكَ فَلْيَتَنَافَسِ ٱلْمُتَنَٰفِسُونَ ﴿٢٦﴾

Mfano: (2) Al-Baiyyinah (98:5)

وَمَآ أُمِرُوٓا۟ إِلَّا لِيَعْبُدُوا۟ ٱللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ ٱلدِّينَ
حُنَفَآءَ وَيُقِيمُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ وَيُؤْتُوا۟ ٱلزَّكَوٰةَ ۚ وَذَٰلِكَ
دِينُ ٱلْقَيِّمَةِ ﴿٥﴾

Mfano: (3) Al-Fajr (89:23)

وَجِا۟ىٓءَ يَوْمَئِذٍۭ بِجَهَنَّمَ ۚ يَوْمَئِذٍ يَتَذَكَّرُ ٱلْإِنسَٰنُ وَأَنَّىٰ
لَهُ ٱلذِّكْرَىٰ ﴿٢٣﴾

**Laam Alif (لا).** Hapa ni mahala ambapo msomaji haruhusiwi kabisa kusimama au kupumzika. Haipasi kusimama kwakuwa kisomo cha kuishia hapo hakitoi maana iliyokusudiwa kwasababu ukamilifu wa maudhui hupatikana kwa kuungana na kipande cha aya kinachofuatia.

Mfano: (1) Al-Maaidah (5:53)

وَيَقُولُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ أَهَٰٓؤُلَآءِ ٱلَّذِينَ أَقۡسَمُواْ بِٱللَّهِ
جَهۡدَ أَيۡمَٰنِهِمۡ ۙ إِنَّهُمۡ لَمَعَكُمۡۚ

Mfano: (2) An-nahl (16:25)

لِيَحۡمِلُوٓاْ أَوۡزَارَهُمۡ كَامِلَةٗ يَوۡمَ ٱلۡقِيَٰمَةِ ۙ وَمِنۡ أَوۡزَارِ
ٱلَّذِينَ يُضِلُّونَهُم بِغَيۡرِ عِلۡمٍۗ

Mfano: (3) An-nahl (16:32)

ٱلَّذِينَ تَتَوَفَّىٰهُمُ ٱلۡمَلَٰٓئِكَةُ طَيِّبِينَ ۙ يَقُولُونَ سَلَٰمٌ
عَلَيۡكُمُ

**Seen (س)** ni kituo ambapo msomaji anaruhusiwa kupumzika kidogo (juu kwa juu) na kuendelea pasina kukatisha kisomo.

Mfano: (1) Al-Mutafiffiin (83:14)

كَلَّاۖ بَلۡۜ رَانَ عَلَىٰ قُلُوبِهِم مَّا كَانُواْ يَكۡسِبُونَ ١٤

Mfano: (2) Al-Qiyamah (75:27)

وَقِيلَ مَنۡۜ رَاقٖ ٢٧

## Aina na Usomaji wa Hamzah

**Hamzah Fasl:** ni hamza tenganishi itenganishayo herufi za neno. Hutokea mwanzoni, katikati au mwishoni mwa neno. Hamzah *fasl* hujitokeza pamoja na nomino (*ismu*) viwakilishi (*dhamiri)*, vitenzi (*fi'ilu*). Katika usomaji, *Hamzah fasl* hutamkwa bayana, yaani kwa dhahiri.

Mfano: (1) Al-fath (48:1)

إِنَّا فَتَحْنَا لَكَ فَتْحًا مُّبِينًا ﴿١﴾

Mfano: (2) Al-fath (48:29)

مُّحَمَّدٌ رَّسُولُ ٱللَّهِ وَٱلَّذِينَ مَعَهُۥٓ أَشِدَّآءُ عَلَى ٱلْكُفَّارِ

Mfano: (3) Al-Imraan (3:5)

إِنَّ ٱللَّهَ لَا يَخْفَىٰ عَلَيْهِ شَىْءٌ فِى ٱلْأَرْضِ وَلَا فِى ٱلسَّمَآءِ

Mfano: (4) Al-Baqarah (2:4)

وَٱلَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِمَآ أُنزِلَ إِلَيْكَ وَمَآ أُنزِلَ

مِن قَبْلِكَ وَبِٱلْءَاخِرَةِ هُمْ يُوقِنُونَ ﴿٤﴾

Mfano: (5) Al-A'araaf (7:4)

وَكَم مِّن قَرْيَةٍ أَهْلَكْنَٰهَا فَجَآءَهَا بَأْسُنَا بَيَٰتًا

أَوْ هُمْ قَآئِلُونَ ﴿٤﴾

**Hamzah Wasl**

Hamzah Wasl ni hamzah unganishi inayotokea mwanzoni mwa neno ambalo herufi ya pili kutoka (*hamzah)* huwa na *saakin. Hamzah wasl* huwa na alama ya ***saad*** ndogo **juu** ya ***alif.***

**Hamzah Wasl** husomeka kwa sauti ya ***fatah*[a]** pale inapoambatana na herufi ya ***laam*** mwanzoni mwa neno (*ambalo ni jina-**ismu***). Mfano: (1) Al-fatiha(1:2)

ٱلْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿٢﴾

Mfano (2) Al-Baqarah (2:229)

ٱلطَّلَٰقُ مَرَّتَانِۖ فَإِمۡسَاكُۢ بِمَعۡرُوفٍ أَوۡ تَسۡرِيحُۢ بِإِحۡسَٰنٖۗ

Mfano (3) Al-Baqarah (2:255)

ٱللَّهُ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ٱلۡحَيُّ ٱلۡقَيُّومُۚ

Mfano (4) Al-Imraan (3:60)

ٱلۡحَقُّ مِن رَّبِّكَ فَلَا تَكُن مِّنَ ٱلۡمُمۡتَرِينَ ٦٠

Mfano (5) Al-Furqaan (25:26)

ٱلۡمُلۡكُ يَوۡمَئِذٍ ٱلۡحَقُّ لِلرَّحۡمَٰنِۚ

**Hamzah Wasl** husomeka kwa sauti ya ***kasrah*[i]** pale inapotokea mwanzoni mwa neno (*kitenzi*-***fi'ilu***)lenye **fatah** au **kasrah** katika herufi yake **ya tatu**.

Mfano (1) An-Nazi'at (79:17)

ٱذۡهَبۡ إِلَىٰ فِرۡعَوۡنَ إِنَّهُۥ طَغَىٰ ١٧

Mfano (2) Al-Mujadilla (58:19)

ٱسۡتَحۡوَذَ عَلَيۡهِمُ ٱلشَّيۡطَٰنُ فَأَنسَىٰهُمۡ ذِكۡرَ ٱللَّهِۚ

Mfano (3) Al-Mujadilla (27:37)

ٱرۡجِعۡ إِلَيۡهِمۡ فَلَنَأۡتِيَنَّهُم بِجُنُودٖ لَّا قِبَلَ لَهُم بِهَا
وَلَنُخۡرِجَنَّهُم مِّنۡهَآ

**Hamzah Wasl** husomeka kwa sauti ***dhammah*[u]** inapotokea mwanzoni mwa neno (*kitenzi-**fi'ilu***) lenye **dhammah** katika herufi yake **ya tatu.**

Mfano (1) Al-Hijr (15:46)

ٱدْخُلُوهَا بِسَلَٰمٍ ءَامِنِينَ ﴿٤٦﴾

Mfano (2) An-nahl (16:125)

ٱدْعُ إِلَىٰ سَبِيلِ رَبِّكَ بِٱلْحِكْمَةِ وَٱلْمَوْعِظَةِ ٱلْحَسَنَةِ ۖ

Mfano (3) Twaha (20:31)

ٱشْدُدْ بِهِۦٓ أَزْرِى ﴿٣١﴾

Mfano (4) Al-ankabuut (29:45)

ٱتْلُ مَآ أُوحِىَ إِلَيْكَ مِنَ ٱلْكِتَٰبِ وَأَقِمِ ٱلصَّلَوٰةَ ۖ

إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ تَنْهَىٰ عَنِ ٱلْفَحْشَآءِ وَٱلْمُنكَرِ ۗ

Mfano (5) Ghaafirt (40:76)

ٱدْخُلُوٓا۟ أَبْوَٰبَ جَهَنَّمَ خَٰلِدِينَ فِيهَا ۖ فَبِئْسَ مَثْوَى

ٱلْمُتَكَبِّرِينَ ﴿٧٦﴾

**Hamzah Wasl** wakati mwingine huwa haitamkwi kabisa pale inapokuwa kati (*ndani*) ya neno au hata kama itakuwa *hamzahWasl* itakuwa mwanzoni mwa neno, haitotamkwa endapo itatanguliwa na neno lingine nyuma yake.

Mfano (1) Al-baqarah(2:72)

وَإِذْ قَتَلْتُمْ نَفْسًا فَٱدَّٰرَْٰٔتُمْ فِيهَا ۖ وَٱللَّهُ مُخْرِجٌ مَّا

كُنتُمْ تَكْتُمُونَ ﴿٧٢﴾

Mfano (2) Al-baqarah(2:169)

إِنَّمَا يَـأْمُرُكُم بِٱلسُّوٓءِ وَٱلْفَحْشَآءِ تَقُولُوا۟ عَلَى

ٱللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ١٦٩

Mfano (3) Al-kahf(18:56)

وَيُجَـٰدِلُ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ بِٱلْبَـٰطِلِ لِيُدْحِضُوا۟ بِهِ

ٱلْحَقَّ ۖ وَٱتَّخَذُوٓا۟ ءَايَـٰتِى وَمَآ أُنذِرُوا۟ هُزُوًا ٥٦

**Hukumu za Qalqaalah**

Herufi za Qalqaalah ni **tano** ambazo huitwa '***Qutb Jad".*** Yaani ***Qaaf***, ***Taa***, ***Baa***, ***Jeem*** na ***Daal.*** Hizi ni herufi zinasomeka kwa kugongwa. Kizipi?



**Qalqaalah saghra:** ni kuigonga kidogo herufi ya **Qalqaalah** yenye ***sukuun*** inapokuwa ndani baina ya herufi za neno.

Mfano (1) An -nabai (78:8)

وَخَلَقْنَٰكُمْ أَزْوَٰجًا ﴿٨﴾

Mfano (2) Al-adiyat(100:5)

فَوَسَطْنَ بِهِۦ جَمْعًا ﴿٥﴾

Mfano (3) Al-adiyat(100:1)

وَٱلْعَٰدِيَٰتِ ضَبْحًا ﴿١﴾

Mfano (4) Yaasin (36:59)

وَٱمْتَٰزُوا۟ ٱلْيَوْمَ أَيُّهَا ٱلْمُجْرِمُونَ ﴿٥٩﴾

Mfano (5) An-nasr(110:2)

وَرَأَيْتَ ٱلنَّاسَ يَدْخُلُونَ فِى دِينِ ٱللَّهِ أَفْوَاجًا ﴿٢﴾

**Qalqaalah mutawasita:** ni kuigonga pasina mkazo (*bila shaddah*), pale msomaji anaposimama kwenye herufi ya **Qalqaalah.**

Mfano (1)Falaq (113:1)

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ ٱلْفَلَقِ ﴿١﴾

Mfano (2) Hud(11:92)

إِنَّ رَبِّى بِمَا تَعْمَلُونَ مُحِيطٌ ﴿٩٢﴾

Mfano (3) Falaq (113:3)

وَمِن شَرِّ غَاسِقٍ إِذَا وَقَبَ ﴿٣﴾

Mfano (4) Qaf (11:5)

بَلْ كَذَّبُوا۟ بِٱلْحَقِّ لَمَّا جَآءَهُمْ فَهُمْ فِىٓ أَمْرٍ مَّرِيجٍ ﴿٥﴾

Mfano (5) Falaq (113:4)

وَمِن شَرِّ ٱلنَّفَّٰثَٰتِ فِى ٱلْعُقَدِ ﴿٤﴾

**Qalqaalah kubra:** ni kuigonga kwa mkazo pale msomaji anapoisoma herufi ya Qalqaalah yenye shaddah.

Mfano (1) Al-baqarah(2:176)

ذَٰلِكَ بِأَنَّ ٱللَّهَ نَزَّلَ ٱلْكِتَٰبَ بِٱلْحَقِّ ۗ

Mfano (2) Al-Masad(111:176)

تَبَّتْ يَدَآ أَبِى لَهَبٍ وَتَبَّ ﴿١﴾

## Hukumu za Mim na Nun zenye Shadda

**MIM** yenye **shadda**

**MIM** yenye **shadda** ni sawa na **MIM mbili** zenye kufuatana. Wakati wa kutamka, **MIM** ya kwanza huingizwa (huidighamishwa) kwenye **MIM** ya pili kwa **ughani (ghunnah)** wa dhahiri. Hebu tusome mifano ifuatayo kutoka kwenye Juzuu Amma.

## Mifano ya Hukumu ya MIM yenye Shaddah

| No | Aya | surat |
|---|---|---|
| 1. | كَلَّا لَمَّا يَقْضِ مَآ أَمَرَهُۥ ﴿٢٣﴾ | Abasa |
| 2. | فَأُمُّهُۥ هَاوِيَةٌ ﴿٩﴾ | Qaaria |
| 3. | ثُمَّ كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُونَ ﴿٤﴾ | Attakaathur |
| 4. | وَٱمْرَأَتُهُۥ حَمَّالَةَ ٱلْحَطَبِ ﴿٤﴾ | Masad |

**NUN** yenye **shadda**

Kadhalika**, NUN** yenye **shadda** ni sawa na **NUN mbili** zenye kufuatana. Wakati wa kutamka, **NUN** ya kwanza huingizwa yenye saakinah (huidighamishwa) kwenye **NUN** ya pili kwa **ughani (ghunnah)** wa dhahiri. Hebu tusome mifano ifuatayo kutoka kwenye Juzuu Amma.

## Mifano ya Hukumu ya NUN yenye Shaddah

| No | Aya | surat |
|---|---|---|
| 1. | لَتَرَوُنَّ ٱلْجَحِيمَ ﴿٦﴾ | Attakaathur |
| 2. | إِنَّ ٱلْإِنسَٰنَ لَفِى خُسْرٍ ﴿٢﴾ | Asr |
| 3. | كَلَّا لَيُنۢبَذَنَّ فِى ٱلْحُطَمَةِ ﴿٤﴾ | Humazzah |
| 4. | إِنَّآ أَعْطَيْنَٰكَ ٱلْكَوْثَرَ ﴿١﴾ | Kauthar |
| 5. | قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ ٱلنَّاسِ ﴿١﴾ | Annas |

## Hukumu za MIM SAKNA

**Hukumu za MIM SAKNA ni tatu.** *Iz-haar shafawiy*, *Ikhfau shafawiy* **na** *Idgham mithlain saghir*.

## Idh-haar shafawiy

**Idh-haar shafawiy** ni kuitamka ***Mim Sakna*** kwa kuidhihirisha pasina ughani. Yaani, wakati wa kuitamka ***Mim Sakna,*** msomaji atabana kidogo tu midomo na kuidhihirisha bayana herufi inayofuatia. Msomaji hupaswa kusoma hivyo kwa herufi zote zitakazofuatia ***Mim Sakna*** isipokuwa kwa ***Be*** na ***Mim*** yenyewe.




Mifano

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِعَادٍ ﴿٦﴾

ٱلَّتِى لَمْ يُخْلَقْ مِثْلُهَا فِى ٱلْبِلَـٰدِ ﴿٨﴾

فَقَالَ لَهُمْ رَسُولُ ٱللَّهِ نَاقَةَ ٱللَّهِ وَسُقْيَـٰهَا ﴿١٣﴾

## Ikhfau shafawiy

**Ikhfau shafawiy** ni kuisoma ***Mim Sakna*** kwa ughani (ghunnah) bila ya kutia shaddah, pale inapokuwa nyuma ya herufi ya ***Be.*** Wakati wa kusoma, sauti ya ughani wa ***Mim*** udhihiri kwenye uficho wa mkandamizo wa midomo na kutamkwa pamoja na ***Be.***

Mfano (1) At-tuur (52:20)

مُتَّكِـِٔينَ عَلَىٰ سُرُرٖ مَّصۡفُوفَةٖۖ وَزَوَّجۡنَٰهُم بِحُورٍ
عِينٖ ٢٠

Mfano (2) Al-Muluk (67:12)

إِنَّ ٱلَّذِينَ يَخۡشَوۡنَ رَبَّهُم بِٱلۡغَيۡبِ لَهُم مَّغۡفِرَةٞ وَأَجۡرٞ
كَبِيرٞ ١٢

Mfano (3) Al-Insaan (76:12)

وَجَزَىٰهُم بِمَا صَبَرُواْ جَنَّةٗ وَحَرِيرٗا ١٢

Mfano (4) Al-Fiil (105:4)

تَرۡمِيهِم بِحِجَارَةٖ مِّن سِجِّيلٖ ٤

Mfano (5) Al-Adiyaat (100:11)

إِنَّ رَبَّهُم بِهِمۡ يَوۡمَئِذٖ لَّخَبِيرُۢ ١١

**Idgham mithlain saghir** ni kuisoma ***Mim Sakna*** kwa ughani (ghunnah) wa kuiingiza kwenye ***Mim*** ya mbele yenye ***Shaddah.***

Mfano (1) Al-Quraysh (106:4)

ٱلَّذِيٓ أَطۡعَمَهُم مِّن جُوعٖ وَءَامَنَهُم مِّنۡ خَوۡفِۭ ٤

Mfano (2) Al-buruuj (85:20)

وَٱللَّهُ مِن وَرَآئِهِم مُّحِيطُۢ ٢٠

Mfano (3) Al-Jinni (72:16)

وَأَلَّوِ ٱسۡتَقَٰمُواْ عَلَى ٱلطَّرِيقَةِ لَأَسۡقَيۡنَٰهُم مَّآءً غَدَقٗا

Mfano (4) Al-Waaqi'a(56:81)

أَفَبِهَٰذَا ٱلۡحَدِيثِ أَنتُم مُّدۡهِنُونَ ٨١

Mfano (5) Al-Hadid (57:10)

لَا يَسۡتَوِي مِنكُم مَّنۡ أَنفَقَ مِن قَبۡلِ ٱلۡفَتۡحِ وَقَٰتَلَۚ



## Zoezi la Kwanza

1. Taja na kueleza kwa ufupi vituo ambavyo msomaji wa Qur-an analazimika:
    (a) Kusimama Kusoma Qur-an
    (b) Kusimama au kuendelea Kusoma Qur-an
    (c) Kutosimama kusoma Qur-an
    (d) Kupumzika kidogo, na kuendelea

2. (c) Kwa kutoa mifano dhahiri toka kwenye Qur-an, tafautisha baina ya ***Hamzah Fasl*** na ***Hamzah Wasl***
  (b) Bainisha aina ya Hamzah zilizopo katika aya zifuatazo

ٱدْخُلُوهَا بِسَلَٰمٍ ءَامِنِينَ ﴿٤٦﴾ ٱلْمُلْكُ يَوْمَئِذٍ ٱلْحَقُّ لِلرَّحْمَٰنِ

ٱذْهَبْ إِلَىٰ فِرْعَوْنَ إِنَّهُۥ طَغَىٰ ﴿١٧﴾

3. (a) Taja Herufi Tano za Qalqaala
  (b) Bainisha aina za Qalqaala zilizopo katika aya zifuatazo:

وَخَلَقْنَٰكُمْ أَزْوَٰجًا ﴿٨﴾ إِنَّ رَبِّى بِمَا تَعْمَلُونَ مُحِيطٌ

تَبَّتْ يَدَآ أَبِى لَهَبٍ وَتَبَّ ﴿١﴾

4. (a) Mim yenye shada na Nun yenye shada ni Mim na Nun za namna gani?
  (c) Soma kwa sauti aya zifuatazo

كَلَّا لَيُنۢبَذَنَّ فِى ٱلْحُطَمَةِ ﴿٤﴾ كَلَّا لَمَّا يَقْضِ مَآ أَمَرَهُۥ ﴿٢٣﴾

5. (a) Taja Hukumu tatu za Min Sakna
  (b) Soma kwa sauti aya zifuatazo kisha taja hukumu ya Min Sakna iliyopo katika kila aya.

ٱلَّتِى لَمْ يُخْلَقْ مِثْلُهَا فِى ٱلْبِلَٰدِ ﴿٨﴾ تَرْمِيهِم بِحِجَارَةٍ مِّن سِجِّيلٍ

إِنَّ رَبَّهُم بِهِمْ يَوْمَئِذٍ لَّخَبِيرٌۢ ﴿١١﴾ وَٱللَّهُ مِن وَرَآئِهِم مُّحِيطٌۢ ﴿٢٠﴾

# Somo la 2. Tawhid

# Imani ya Kiislamu

## Maana ya Imani katika Uislamu

Imani ni neno la Kiarabu lenye maana ya kuwa na yakini au kuwa na uhakika juu ya jambo fulani usiloliona kwa macho akini kuna dalili za kutosha za kudhihirisha kuwepo kwake.

Imani ya Kiislamu hupatikana kwa kuwa na yakini moyoni kuwa yuko Allah (s.w.) na malaika wake, na vitabu vyake, na Mitume wake, na siku ya mwisho na Qudra yake. Hivi ni vipengele vya Imani ya Kiislamu. Vipengele hivi vimebainishwa katika Hadith ndefu ifuatayo:

> *Umar amesimulia: "Siku moja tulipokuwa tumeketi pamoja na Mtume (s.a.w.) alitutokea mtu mmoja ambaye nguo zake zilikuwa nyeupe kama theluji na nywele zake nyeusi sana, hakuwa na dalili zozote za msafiri, ingawa alikuwa mgeni kwetu sote. Halafu alikaa mbele ya Mtume hali magoti yake yakikabiliana na yale ya Mtume. Akaweka mikono yake katika mapaja ya Mtume halafu akasema: "Ewe Muhammad nifahamishe juu ya Uislamu". Mtume akasema: "Ni kushuhudia kuwa hakuna Mola ila Allah, na kwamba Muhammad ni Mtume wa Allah; kusimamisha swala, kutoa zakat, kufunga Ramadhani na kuhiji kwa mwenye kuweza". Halafu yule mgeni akasema: "Umesema kweli". Tulistaajabu kwa nini aliuliza halafu akasadikisha. Halafu akasema: "Nifahamishe juu ya Imani". Mtume akasema: "Ni kumuamini Allah, malaika wake, vitabu vyake, Mitume wake, siku ya mwisho na Qudra yake kuwa kheri na shari hutoka kwake". Kisha*

*akasema: "Nifahamishe juu ya Ihsan". Mtume akajibu: "Ni kumuabudu Allah kana kwamba unamuona, kwani ingawa humuoni yeye anakuona". Yule mgeni alipoondoka, Mtume alikaa kimya kwa muda halafu akasema: "Ewe Umar unamfahamu muulizaji?" Sote tukajibu kuwa Allah na Mtume wake ndio wajuao. Mtume (s.a.w.) akasema: "Huyo ni Jibril amekuja kuwafundisheni dini yenu". (Muslim)*

Kwa mujibu wa mapokezi ya hadithi hii, Umar na masahaba wale walipotoka kumtazama mtu yule hawakuweza kujua alielekea wapi. Hadithi hii ndefu imetufahamisha kuwa nguzo za Uislamu ni tano, Nguzo za imani ni sita kama zilivyoorodheshwa na kuwa nguzo ya Ihsani ni moja.

Kwenye kiini cha mhimili wa imani ya kiislamu anasimama Allah(s.w), Muumba wa mbingu, ardhi na vilivyomo. Kwa mujibu wa Uislamu ili Mtu aweze kuwa Muumini hanabudi kuwa na yakini inayotokana na ujuzi unaotokana na hoja madhubuti zisizo na tone la shaka zitokanazo na ushahidi wa mazingira yaliyomzunguka kuwa Muumba wa Viumbe vyote ni Mwenyezi Mungu mmoja asiye na mshirika katika uumbaji wake, anayestahiki kuabudiwa na vyote alivyoviumba. Imani ya kiislamu imesimama juu ya nguzo sita ambazo ni Kuamini kuwepo kwa Allah, kuamini Malaika wake, kuamini vitabu vyake, kuamini Mitume wake, kuamini siku ya Mwisho na kuamini Qadari.

**Ni yupi muumini wa kweli?**

Je, yatosha mtu kuitwa muumini kwa kuwa tu anadai kuwa anaamini nguzo sita za Imani? Haitoshi kwa sababu mtu yeyote anaweza kujifanya kuwa anaamini lakini akawa hana yakini moyoni mwake. Wanadamu hatuna uwezo wa kuona moyoni mwa mtu. Allah (s.w.) anatufahamisha:

وَمِنَ ٱلنَّاسِ مَن يَقُولُ ءَامَنَّا بِٱللَّهِ وَبِٱلْيَوْمِ ٱلْءَاخِرِ وَمَا
هُم بِمُؤْمِنِينَ ﴿٨﴾

*"Na katika watu wako wasemao: Tumemuamini Allah na siku ya mwisho na hali ya kuwa wao si wenye kuamini.*(2:8)

يُخَٰدِعُونَ ٱللَّهَ وَٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَمَا يَخْدَعُونَ إِلَّآ
أَنفُسَهُمْ وَمَا يَشْعُرُونَ ﴿٩﴾

*Wanatafuta kumdanganya Allah na wale walioamini, lakini hawadanganyi ila nafsi zao, na hawatambui".* [2:9]

Katika aya hizi, Allah (s.w.) anatufahamisha wazi kuwa kuna watu wanaodai kuwa wanaamini, lakini kwa kweli si wenye kuamini. Si wenye kuamini kwa sababu hakuna athari yoyote ya imani katika matendo yao. Imani ya kweli ni ile inayoyakinishwa moyoni, kisha ikabainishwa na ulimi na kisha ikathibitishwa katika vitendo.

Muumini wa kweli ni yule ambaye ni mcha Mungu. Mcha Mngu ni yule ambaye baada ya kuwa na yakini na vipengele vya nguzo za Imani, humtii Allah (s.w.) na Mtume wake kama inavyostahiki. Kumtii Allah (s.w) na Mtume wake inavyostahiki ni kufuata kwa unyenyekevu maamrisho yote ya Allah (s.w.) na Mtume wake na kuacha makatazo yote ya Allah (s.w.) na Mtume wake. Aya za Qur'an zinatufahamisha kuwa waumini wa kweli hasa ni wale:

ٱلَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِٱلْغَيْبِ وَيُقِيمُونَ ٱلصَّلَوٰةَ وَمِمَّا
رَزَقْنَٰهُمْ يُنفِقُونَ ﴿٣﴾

*"Ambao huyaamini yasiyoonekana (yaliyofichikana) na husimamisha swala na hutoa katika yale tuliyowapa.*

وَٱلَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِمَآ أُنزِلَ إِلَيْكَ وَمَآ أُنزِلَ مِن قَبْلِكَ
وَبِٱلْأَخِرَةِ هُمْ يُوقِنُونَ ﴿٤﴾

*Na ambao wanaamini yaliyoteremshwa kwako na yaliyoteremshwa kabla yako, na wanaamini kuwa iko akhera.*

أُوْلَٰٓئِكَ عَلَىٰ هُدًى مِّن رَّبِّهِمْ ۖ وَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْمُفْلِحُونَ

*Hao wako juu ya uongozi utokao kwa Mola wao, na hao ndio wenye kuongoka".* [2:3-5]

Katika Suratul Anfal tunafahamishwa ni akina nani waumini wa kweli kweli:

إِنَّمَا ٱلْمُؤْمِنُونَ ٱلَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ ٱللَّهُ وَجِلَتْ قُلُوبُهُمْ
وَإِذَا تُلِيَتْ عَلَيْهِمْ ءَايَٰتُهُۥ زَادَتْهُمْ إِيمَٰنًا وَعَلَىٰ
رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٢﴾

*"Hao wanaoamini kweli ni wale ambao anapotajwa Allah nyoyo hujaa khofu; na wanaposomewa aya zake huwazidishia imani, na wakamtegemea Mola wao tu basi.*

ٱلَّذِينَ يُقِيمُونَ ٱلصَّلَوٰةَ وَمِمَّا رَزَقْنَٰهُمْ يُنفِقُونَ ﴿٣﴾

*Ambao wanasimamisha swala na wanatoa katika yale tuliyowapa.*

أُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْمُؤْمِنُونَ حَقًّاۚ لَّهُمْ دَرَجَٰتٌ عِندَ

رَبِّهِمْ وَمَغْفِرَةٌ وَرِزْقٌ كَرِيمٌ ﴿٤﴾

*Hao ndio wanaoamini kweli., Wao wana vyeo vikubwa kwa Mola wao, na msamaha na riziki bora".* [8:2-4]

Katika Suratul - Hujurat tunafahamishwa tena ni nani Muumini wa kweli:

إِنَّمَا ٱلْمُؤْمِنُونَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ بِٱللَّهِ وَرَسُولِهِۦ ثُمَّ لَمْ

يَرْتَابُواْ وَجَٰهَدُواْ بِأَمْوَٰلِهِمْ وَأَنفُسِهِمْ فِى سَبِيلِ

ٱللَّهِۚ أُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلصَّٰدِقُونَ ﴿١٥﴾

*"Wenye kuamini kweli kweli ni wale waliomuamini Allah na Mtume wake, kisha wakawa si wenye shaka, na wakaipigania dini ya Allah kwa mali zao na nafsi zao. Hao ndio wenye kuamini kweli".* [49:15]

Katika Suratit-Tawba tunafahamishwa juu ya waumini kuwa:

وَٱلْمُؤْمِنُونَ وَٱلْمُؤْمِنَٰتُ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَآءُ بَعْضٍۚ

يَأْمُرُونَ بِٱلْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ ٱلْمُنكَرِ وَيُقِيمُونَ

ٱلصَّلَوٰةَ وَيُؤْتُونَ ٱلزَّكَوٰةَ وَيُطِيعُونَ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥٓۚ

أُوْلَٰٓئِكَ سَيَرْحَمُهُمُ ٱللَّهُۗ إِنَّ ٱللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٧١﴾

*"Na wanaoamini wanaume na wanaoamini wanawake, ni marafiki wao kwa wao. Huyaamrisha yaliyo mema na kuyakataza yaliyo mabaya, na husimamisha swala na hutoa zaka, na humtii Allah na Mtume wake. Hao ndio ambao Allah atawarehemu. Hakika Allah ni mwenye nguvu, mwenye hikima".* [9:71]

Kwa muhutasari aya hizi zinatufahamisha kuwa Muumini wa kweli ni yule:

(1)Anayeyakinisha moyoni juu ya kuwepo Allah (s.w.) na vipengele vingine vyote vya imani ya Kiislamu.

(2)Anayemtii Allah (s.w.) na Mtume wake ipasavyo kwa kusimamisha swala, kutoa zakat na kufanya yale yote mengine yaliyoamrishwa na Allah (s.w.) na Mtume wake. Pamoja na kuacha yale yote yaliyokatazwa na Allah (s.w.) na Mtume wake.

(3)Ambaye rafiki zake wa moyoni ni Allah (s.w.) na Mtume wake na waumini. Ambaye kamwe hawafanyi maadui wa Allah (s.w.) na Mtume wake kuwa ni marafiki zake.

(4)Anayeshirikiana na waumini wenzake bega kwa bega katika kuamrisha mema na kukataza maovu.

(5)Anayejitoa muhanga katika kupigania dini ya Allah (s.w.) kwa mali yake na nafsi yake.

### Maana ya kumuamini Allah (s.w.)

Maana ya kumuamini Allah (s.w.) ni kumpwekesha Allah (s.w.) katika utendaji wa kila siku. Kumpwekesha Allah (s.w.) ni kumfanya Allah (s.w.) kuwa ndiye Mungu pekee anayestahiki Uungu katika dhati yake, ndiye yeye anayestahiki kusifiwa kwa sifa zote njema,

ndiye yeye peke yake mwenye haki ya utawala anayepasa kuongoza, kunyenyekewa, kuogopwa. kutiiwa, kuombwa, kutegemewa na kutukuzwa na viumbe wote.

Kwasababu ni Allah ndiye aliyeumba mbingu na kuikinga kwa nguvu zisizoonekana. Ndiye aliyeziumba sayari ikiwemo ardhi yetu hii zote zikiogelea na kuelea angani pasi na mgongano wowote. Na kwamba bila ya uweza wake huo vyote vinavyoonekana na visivyoonekana visingekuwepo. Aliyeumba miti, Mimea na Wanyama na ni yeye aliyewaumba Wanaadamu na Majini. Kuwepo na kuendelea kuwa hivyo kwa kila chembe ya ulimwengu huu kunategemea yeye. Kwa ajili hiyo, mja hanabudi kufuata vile aliyoelekeza Muumba huyo.

Mwenyezi Mungu ndiye mwenye habari za mambo yote yanayotendwa ulimwenguni. Kwa hakika Allah ndiye anayestahiki kuwaelekeza Wanadamu mfumo wa maisha wa amani na furaha ya kweli. Kwasababu huyajuwa matashi ya mja kwa hiyo ni yeye tu mwenye haki ya kuelekeza katika kuyakidhi kwa namna iliyo bora.

Kutekeleza anayoyaamrisha Allah ni kujihakikishia amani na utulivu wa kweli katika moyo. Viumbe wote wanamuhitaji yeye kuweza kuendesha maisha yao na msafara wao wote unaelekea kwake kwa msaada na amri yake yeye Muumba na mlezi wa viumbe. Allah ametukuka kwa utukufu wa juu, mwenye kustahiki kuabudiwa.

Vitu vyote vinavyoweza kuhisiwa na kuchunguzwa kwa jicho la kawaida au kwa utaalamu wa sayansi kulingana na teknolojia , maumbile hayo ni kazi ya Allah inayotokana na uumbaji wake usioweza kudirikiwa. Allah mwenyewe si sehemu ya maumbile haya kama alivyo mwanadamu anavyoweza kuishi ndani ya kile alichokiunda. Kwa hivyo ni muhali sifa na silka ya Muumba kuweza kufanana au kuwa sawa na sifa za viumbe vyake.

**Shirki: Kumshirikisha Allah (s.w)**

Kumtii yoyote kinyume cha maamrisho ya Allah (s.w.) ni shirki. Kumuomba yeyote asiyekuwa Allah (s.w.) maombi yaliyokiuka uwezo wa binadamu kama vile kuomba baraka, riziki, mtoto, au kuogopa chochote kile kwa kuvuka mipaka ni shirki. Anayemshirikisha Allah (s.w) huwa si muumini wa Kiislamu.

Kwa maana nyingine, maana ya kumuamini Allah (s.w.) ni kutomshirikisha Allah (s.w.) na chochote katika maisha yetu ya kila siku. Kumshirikisha Allah (s.w.) ni kujaalia kuwa kuna wengine asiyekuwa Allah (s.w.) wanaostahiki kutiiwa, kuogopwa, kuombwa, na kutegemewa badala au pamoja na Allah (s.w.).

## Aina za shirki na ushirikina

### *(a) Kumshirikisha Allah (s.w.) katika Dhati yake*

Kumshirikisha Allah (s.w.) katika Dhati yake ya Uungu ni kuvijaalia viumbe kuwa miungu wanaoshirikiana na Allah (s.w.). Kumjaalia kiumbe kuwa mungu ni kama vile kufanya maombi au matambiko mbele ya sanamu, mienge ya moto, mbuyu, kaburi, masharifu,watakatifu, milima na kadhalika. Chochote kitakachowekwa mbele na kuelekewa kwa maombi na mategemeo kitakuwa kimefanywa mungu badala ya Allah (s.w). Pia kudai kuwa Allah (s.w.) ana mtoto au kukifananisha chochote na Allah (s.w.) ni kumshirikisha Allah (s.w.) katika Dhati yake. Kwasababu:

هُوَ ٱللَّهُ أَحَدٌ ١ ٱللَّهُ ٱلصَّمَدُ ٢ لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ

٣ وَلَمْ يَكُن لَّهُۥ كُفُوًا أَحَدٌۢ ٤

*Yeye ni Allah aliye mmoja tu. Allah Ndiye anayestahiki kukusudiwa (na viumbe vyake vyote kwa kumuabudu kumuomba na kumtegemea). Hakuzaa wala hakuzaliwa. Wala hana anayefanana naye hata mmoja".* [112:1-4]

### (b)Kumshirikisha Allah (s.w.) katika sifa zake

Kumshirikisha Allah (s.w.) katika sifa zake ni kukitukuza kiumbe chochote kama anavyostahiki kutukuzwa Allah (s.w.) au kukijaalia kiumbe chochote kuwa na uwezo wa kiungu. Kwa mfano kuitakidi kuwa mwanadamu anagawa baraka, au ana uwezo wa kuhuisha wafu, au ana uwezo wa kufisha, au ana uwezo wa kujua mambo ya ghaibu, au..., ni kumshirikisha mtu huyo na Allah (s.w). Yaani mtu huyo atakuwa amepachikwa sifa ya Allah (s.w.). Qur'an tukufu imetukataza kujisifu au kuwasifu wengine kiasi cha kuvuka mipaka kama inavyoelezwa katika aya ifuatayo:

فَلَا تُزَكُّوٓا۟ أَنفُسَكُمْ ۖ هُوَ أَعْلَمُ بِمَنِ ٱتَّقَىٰٓ ﴿٣٢﴾

*"... Basi msizitakase (mzizisifu) nafsi zenu, yeye (Allah) anamjua sana aliyetakasika".* [53:32]

### (c)Kumshirikisha Allah (s.w.) katika ulezi na utawala wake

Kumshirikisha Allah (s.w.) katika ulezi na utawala wake ni kukipa kiumbe mamlaka ya kulea na kutawalia viumbe vya Allah (s.w.). Allah (s.w.) ndiye aliyeumba viumbe vyote kwa makusudio maalum. Hivyo ndiye pekee mwenye uwezo na mwenye kustahiki kuviwekea viumbe sheria na mwongozo ili vifikie lengo lililokusudiwa. Kwa mfano mwanadamu ameumbwa kwa lengo la kumuabudu Allah (s.w.) na kuwa khalifa wake hapa ulimwenguni. Hivyo yeye ndiye pekee mwenye haki na uwezo wa kumuwekea mwanadamu sheria na mwongozo wa maisha.

Mwanadamu anapaswa atii sheria hizi na kufuata kwa unyenyekevu mwongozo wa maisha aliowekewa na Muumba wake. Sasa, atakapoamua kuchukua mamlaka ya Allah (s.w.) na kuwatungia wanadamu wenziwe sheria na mwongozo kinyume na sheria na mwongozo wa Allah (s.w.) na kuwalazimisha waufuate atakuwa amechukua nafasi ya uungu wa Allah (s.w). Na wale watakaomtii na kufuata sheria na mwongozo kinyume na ule wa Allah (s.w.) watakuwa wamemfanya huyu ndiye mungu wao. Shirki

hii imewekwa wazi katika aya ifuatayo:

ٱتَّخَذُوٓاْ أَحۡبَارَهُمۡ وَرُهۡبَٰنَهُمۡ أَرۡبَابٗا مِّن دُونِ ٱللَّهِ

*"Wamewafanya wanavyuoni wao na* watawa wao kuwa ni miungu *badala ya Allah (s.w.)...".* [9:31]

Katika kufafanua aya hii Mtume (s.a.w.); Mayahudi na Wakristo wameshutumiwa kuwafanya viongozi wao miungu badala ya Allah (s.w.) kwa sababu viongozi wao waliwawekea sheria kinyume na sheria za Allah (s.w.) na wao wakakubali kuzitii. Kwa mfano viongozi wao waliwaharamishia vile alivyovihalalisha Allah (s.w.), wamekuwa wakiwatii. Pia waliwahalalishia vile alivyoharamisha Allah (s.w.) kamavile riba, ulevi n.k. na wao wakawatii. Hivyo kumtii yeyote kinyume na sheria na mwongozo wa Allah (s.w.) ni kumfanya mungu wako.

***(d)Kumshirikisha Allah (s.w.) katika Hukumu zake***

Kumshirikisha Allah (s.w.) katika hukumu zake ni kuhukumia jambo au kutoa uamuzi juu ya jambo lolote kinyume na hukumu ya Allah (s.w.) iliyobayana katika Qur'an. Mwenye haki na uwezo wa kumuwekea mwanadamu sheria ni Allah (s.w.) pekee. Pia ndiye pekee mwenye haki ya kutoa adhabu kwa wavunjaji wa sheria zake. Allah (s.w.) amekemea vikali tabia hii katika aya zifuatazo:

فَلَا تَخۡشَوُاْ ٱلنَّاسَ وَٱخۡشَوۡنِ وَلَا تَشۡتَرُواْ بِـَٔايَٰتِي
ثَمَنٗا قَلِيلٗاۚ وَمَن لَّمۡ يَحۡكُم بِمَآ أَنزَلَ ٱللَّهُ فَأُوْلَٰٓئِكَ
هُمُ ٱلۡكَٰفِرُونَ ﴿٤٤﴾

*"…Basi (nyinyi Waislamu) msiwaogope watu bali niogopeni Mimi wala msibadilishe aya Zangu kwa thamani ndogo (ya kidunia). Na wasiohukumu kwa yale aliyoyateremsha Allah, basi hao ndio makafiri".* [5:44]

## Matendo ya Shirk katika maisha ya kila siku

Ukizingatia aina kuu nne za Shirk, yafuatayo ni matendo ya Shirk yanayofanywa kila mara katika maisha ya kawaida ya kila siku:

(i)Kuomba makaburi, matambiko n.k.
(ii)Kujikinga na hirizi, azima, matalasimu n.k.
(iii)Kupiga ramli, kutazamia kwa nyota, utabiri n.k.
(iv)Kuomba baraka kwa watu, kuomba dua kupitishia kwa watu wema au Mitume.
(v)Kuamini uchawi na kuroga.
(vi)Kuitakidi kuwa mashetani (majini) wana mamlaka juu ya mwanadamu.
(vii) Kuogopa watu, mamlaka na tawala ambako hupelekea mtu kutumikishwa, kutawaliwa na kudhulumiwa.
(vii)Kuwatii watu kinyume na sheria ya Allah (s.w.).
(viii)Kufuata mwongozo na sera zilizo kinyume cha Qur'an na Sunnah.
(ix)Kufuata hukumu au utawala ulio kinyume na maelekezo ya Qur'an na Sunnah.
(x)Kuwapa watu mamlaka ya kutunga sheria na kuongoza watu kinyume na Qur'an na Sunnah.
(xi)Kutii nafsi kinyume na Allah (s.w.) ni kuifanya nafsi yako mungu badala ya Allah (s.w.).
(xii)Kuamua kufuata baadhi ya sheria za Allah (s.w.) na kukufuru baadhi yake.

Haya yote ni matendo ya kumshirikisha Allah (s.w.). Kila atakachokifanya mtu kinyume na kumpwekesha Allah (s.w.) katika maisha ya kila siku atakuwa amemshirikisha kwa njia moja au nyingine.

## Maana ya kuamini Malaika

Miongoni mwa kazi za Malaika ni kudhibiti matendo ya binadamu katika maandishi kwa kila wanalolifanya, jema au ovu.

Hivyo, muumini mwenye yakini na kuwepo kwa Malaika na kazi zao kama zilivyoelezwa katika Qur'an, atajitahidi kufanya matendo mema na kujiepusha na maovu. Jaalia una hakika kabisa askari wanakuchunguza kwa kila unalolifanya. Je, utathubutu kuvunja sheria mbele yao? Huthubutu kwa kuwa watakukamata na kukupeleka kwenye mahakama. Vyombo vya Dola vitakutia mikononi na kukuadhibu inavyostahiki. Hali kadhalika muumini wa kweli juu ya malaika atajitahidi kutenda mema na kujiepusha na maovu ili ipelekwe ripoti nzuri mbele ya Mola wake na malaika wanaodhibiti matendo yake.

## Maana ya kuamini vitabu vya Allah (s.w.)

Maana ya kuamini vitabu vya Allah (s.w.) ni kufuata vitabu hivyo kama muongozo wetu pekee katika kuendesha maisha yetu ya kila siku. Kwa kuwa leo hii kitabu cha Allah (s.w.) katika asili yake na usahihi wake ni Qur'an pekee, muongozo wetu wa maisha hauna budi kuwa Qur'an pekee. Muumini wa kweli huyatekeleza maamrisho na maagizo yote ya Qur'an na anajiepusha mbali na makatazo na makemeo yake yote.

## Maana ya kuamini Mitume wa Allah (s.w.)

Maana ya kuamini Mitume wa Allah (s.w.) ni kufuata mafundisho y a Mitume wote kuanzia wa kwanza, Adam (a.s.) hadi wa mwisho, Muhammad (s.a.w.). Mitume wote wamefundisha Uislamu na mifano yao ya maisha ni ya kuigwa na waumini wa nyakati zote. Hakuna Mtume aliyekuja kufundisha imani au dini nyingine isiyokuwa Uislamu, kama inavyobainishwa katika Qur'an kuwa:

إِنَّ ٱلدِّينَ عِندَ ٱللَّهِ ٱلْإِسْلَٰمُ ۗ

*"Hakika dini mbele ya Allah ni Uislamu"… . (3:19).*

Mtume wa Ummah huu wa mwisho ni Muhammad (s.a.w.). Ndiye aliyeshushiwa Qur'an, kitabu cha mwisho cha Allah (s.w.). Mtume Muhammad (s.a.w.) ndiye mfasiri wa Qur'an kinadharia na kivitendo. Muumini wa kweli hivi sasa ni yule anayefuata vilivyo mafundisho yote ya Qur'an na mafundisho yote ya Mtume Muhammad (s.a.w.). Muumini wa kweli hatazamiwi hata kidogo kwenda kinyume na Qur'an na Sunnah (mafundisho na mwenendo wa Mtume). Allah (s.w.) anatufahamisha katika Qur'an:

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى ٱللَّهُ وَرَسُولُهُۥٓ أَمْرًا
أَن يَكُونَ لَهُمُ ٱلْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ ۗ وَمَن يَعْصِ ٱللَّهَ
وَرَسُولَهُۥ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَٰلًا مُّبِينًا ﴿٣٦﴾

*"Haiwi kwa mwanamume aliyeamini wala kwa mwanamke aliyeamini, Allah na Mtume wake wanapokata shauri, wawe na hiari katika shauri lao. Na mwenye kumuasi Allah na Mtume wake, hakika amepotea upotovu ulio wazi kabisa".* [33:36]

## Maana ya kuamini siku ya mwisho

Kuamini siku ya mwisho, kwa ujumla ni kuamini kuwa kuna maisha mengine ya akhera baada ya maisha haya ya hapa duniani. Kituo cha kwanza cha maisha ya akhera ni pale roho ya mtu inapotengana na mwili na kituo cha mwisho ni mashukio ya peponi au motoni.

Kulingana na mafundisho ya Qur'an na Hadith sahihi za Mtume (s.a.w.) watu wema, walioishi hapa duniani kwa kumtii ipasavyo Allah (s.w.) na Mtume wake wataishi maisha ya furaha na amani katika maskani mazuri ya kudumu milele ya peponi. Furaha hii huanzia pale roho zao zinapotoka. Kinyume chake walioishi hapa

duniani kwa kumuasi Allah (s.w.) na Mtume wake wataishi kwa huzuni kubwa na khofu katika maskani ya adhabu ya motoni. Huzuni hii huanzia pale wanapotolewa roho zao.

Bila shaka muumini wa kweli wa siku ya mwisho atapania maisha ya peponi kwa kujitahidi kufanya wema kwa kadiri ya uwezo wake. Atafuata maamrisho yote ya Allah (s.w.) kwa kadiri ya uwezo wake. Atamtii Mtume na kufuata mwenendo wake.

Kwa upande mwingine muumini wa kweli wa siku ya mwisho atajitahidi kwa kadiri ya uwezo wake kujiepusha na adhabu ya Jahannamu kwa kuacha maovu yote. Atajiepusha na makatazo yote ya Allah (s.w.). Pale atakapoteleza na kukosea atarejea haraka haraka kwa Mola wake kwa kuomba msamaha na kutubia toba ya kweli. Aidha kila mara muumini wa siku ya mwisho atakuwa anaomba dua ifuatayo:

رَبَّنَآ ءَاتِنَا فِى ٱلدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِى ٱلْءَاخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ ٱلنَّارِ ﴿٢٠١﴾

*"...Mola wetu! Tupe mema hapa duniani na (utupe) mema akhera, na utulinde na adhabu ya moto".* [3:201]

## Maana ya kuamini Qadar ya Allah (s.w.)

Kuamini Qadar ya Allah (s.w.) ni kuamini kuwa Allah (s.w.) ndiye mwenye uwezo juu ya kila kitu na amedhibiti kila kitu. Kila jambo la kheri au shari liko mikononi mwake. Ndiye aliyeviumba vitu vyote na kuvipangilia kama vilivyo. Muumini wa kweli wa Qadar ya Allah (s.w.) huwa na tabia ifuatayo katika utendaji wake wa maisha ya kila siku:

(1) Huridhika (hukinai) na vipawa na neema alizotunukiwa na Mola wake, hata kama zitaonekana kuwa duni ukizilinganisha na za wengine. Huridhika kuwa kile alichokadiriwa na Mola wake ndicho

kinachomfaa hapa duniani na huko Akhera.

(2) Hutumia vipawa na neema alizotunukiwa kwa kadiri ya uwezo wake katika harakati za maisha ndani ya mipaka ya Allah (s.w.). Kisha huridhika na matunda atakayoyapata hata kama yataonekana kuwa duni ukilinganisha na matamanio ya kibinadamu. Utazingatia neno la Kiswahili "Jitihada za mja hazishindi Qadar ya Mwenyezi Mungu".

(3)Hujihadhari yeye mwenyewe na kuwahadharisha wengine kujiepusha na yale yanayohatarisha maisha au kuleta misukosuko na misiba katika maisha. Lakini utakapotokea msiba wowote au janga lolote nje ya uwezo wake hatakata tamaa au kupatwa na ugonjwa wa moyo akikumbuka kuwa kheri zote na shari zote hutokana na Allah (s.w.).

## Maana na aina za Dini

Dini ni utaratibu au mwenendo mzima wa maisha anaoufuata binadamu katika kuendesha maisha yake yote. Dini ni mfumo mzima wa maisha ya jamii ya mwanadamu ambao ndani yake unakusanya mifumo mingi inayokamilisha mahitaji ya maisha ya mwanadamu. Kwa hiyo dini inajumuisha pamoja mifumo ifuatayo:

(1)Mfumo wa siasa.
(2)Mfumo wa uchumi.
(3)Mila na utamaduni
(4)Mfumo wa elimu
(5)Mfumo wa sheria
(6)Imani na Itiqadi
(7)Mfumo wa Ibada maalum n.k.

### Hakuna mtu asiye na Dini

Kwa mujibu huu, hapana mwanadamu asiye na dini.Kila mwanadamu anayo itiqadi fulani juu ya maisha na anafuata mfumo

fulani wa maisha katika kuendesha maisha yake kimwili, kimaadili na kijamii.

### Hapana mtenganisho wa maisha ya Dini na Dunia

Kwa mtazamo huu wa dini, hapana mtengano wa maisha ya Dini na Dunia kwani dini ni furushi zima la vipengele vyote vya maisha ya dunia.

### Aina kuu za Dini

Kila utaratibu wa maisha unajengwa kwa msingi wa Itiqadi fulani. Dini au mfumo wa maisha unaofuatwa na watu wenye itiqadi fulani utapewa jina kulingana na itiqadi hiyo. Katika ulimwengu huu kuna Itiqadi kuu tatu juu ya Mungu Muumba:

### Dini ya Kikafiri.

Kuna wanaoitakidi kuwa ulimwengu huu na vyote vilivyomo hauna aliyeuumba bali umetokea tu wenyewe. Itiqadi hii ni Itiqadi ya Kikafiri inayokanusha kuwepo kwa Allah (s.w.).Mfumo wa maisha anaouunda mwanadamu kwa msingi wa Itiqadi hii ni mfumo wa maisha wa kikafiri au

### Dini ya Kishirikina

Kuna wanaoitakidi kuwa ulimwengu huu una miungu wengi. Yaani aliyeuumba, pana chungu ya miungu wanaomsaidia katika uendesha, kulinda na kufanikisha maisha ya mwanadamu hapa ulimwenguni. Hii ni itikadi ya Ushirikina. Dini iliyofumwa katika msingi huu ni Dini ya Ushirikina.

### Dini ya Kiislamu

Kuna wanaoamini kwa yakini kuwa Muumba ulimwengu ni mmiliki wa vyote vilivyomo ni Allah (s.w.) peke yake. Yeye ndiye pekee mwenye uwezo wa kumuwekea mwanadamu utaratibu wa maisha wenye kumletea furaha na amani. Hii ni itikadi ya Kiislamu. Dini iliyofumwa katika msingi wa itikadi hii ni Dini ya Uislamu.

Kwa ujumla dini zote na mifumo yote ya maisha ulimwenguni huingia katika mojawapo ya makundi haya matatu ya dini. Kwa mfano Ukristo, Uyahudi, Upagani dini za jadi huingia katika dini ya ushirikina. Ubebari, demokrasia, ujamaa, utandawazi huingia katika dini ya Ukafiri. Dini ya ukafiri na dini ya Ushirikina zimeundwa na wanadamu. Dini ya Uislamu imeundwa na Mwenyezi Mungu Muumba wa kila kitu. Kwa msingi huu tunaweza tena kuzikusanya dini katika makundimakubwa mawili yafuatayo:

(a) Dini zilizoundwa na wanadamu (Ukafiri na Ushirikina).
(b) Dini iliyowekwa na Mwenyezi Mungu (Uislamu).

**Ni ipi Dini sahihi**

Dini iliyosahihi inayostahiki kuwa chaguo la mwanaadamu mwenye akili na busara ni ile yenye sifa zifuatazo:

(1) Iliyofumwa juu ya msingi wa itikadi ya kweli.
(2) Mfumo wa dini sahihi uwe sambamba na mfumo wa maumbile.
(3) Iwe na uwezo wa kutosheleza mahitaji yote ya mwanadamu ya kimwili na kiroho.
(4) Uwe ni mfumo wa maisha uliokamilika.
(5) Iwe ni dini ya ulimwengu isiyo na ubaguzi wa aina yoyote.
(6) Iwe na utaratibu madhubuti isiyo na ubaguzi wa aina yoyote.
(7) Iwe na taasisi maalum za kujenga utu wa mwanadamu.

Ukichunguza sifa hizi kwa makini utagundua kuwa Dini zilizobuniwa na wtu, yaani Ukafiri na Ushirikina, hazina sifa hizi. Kwa mfano ukizingatia sifa ya kwanza, makafiri wanadai kuwa ulimwengu huu hauna aliyeuumba na Washirikina wanadaikuwa ulimwengu huu una miungu wengi wanaoumiliki na kuuendesha. Madai haya hayaingii akilini kwa mtu mwenye akili na busara. Dini zilizobuniwa na watu zinaupungufu mkubwa unaotokana na udhaifu wa mwanadamu.Mwanadamu ana udhaifu wa ubinafsi na

anatawaliwa na matashi ya nafsi yake. Hana ujuzi wa mambo ya ghaibu (yaliyofichikana) na wala hana ujuzi wa mambo yatakayokuja baadaye. Mara zote hupanga na kufanya mambo yake kwa misingi ya dhana.

Uislamu ukichunguza kwa makini , sifa zote za dini sahihi, utaona kuwa ndio Dini sahihi pekee. Uislamu ni utaratibu wa maisha alioufuma Mwenyezi Mungu, Muumba wa ulimwengu na vyote vilivyomo. Kwa kuwa ndiye aliyemuumba mwanadamu kwa lengo maalum, ndiye pekee mwenye uwezo wa kumuongoza kwa usahihi mpaka afikie lengo lililokusudiwa.

Uislamu ni dini inayofuatwa na maumbile yote. Yaani maumbile yote yanatii kwa ukamilifu sheria zote za maumbile (*natural laws)* alizoziweka Allah (s.w.), Mungu Muumba wa kila kitu. Hivyo mwanadamu akiamua kuwa Muislamu kwa kutii sheria zote za Allah (s.w.) katika kukiendea kila kipengele cha maisha, atakuwa amejiiunga na maumbile yote katika kumtii Muumba. Mwanadamu atakayeamua kujitenga na maumbile katika kumtii Muumba ni lazima tumshangae kwa mshangao huu wa Qur'an:

أَفَغَيْرَ دِينِ ٱللَّهِ يَبْغُونَ وَلَهُۥٓ أَسْلَمَ مَن
فِى ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ طَوْعًا وَكَرْهًا وَإِلَيْهِ
يُرْجَعُونَ ﴿٨٣﴾

*"Je! Wanataka dini isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu, na hali kila kilichomo mbinguni na ardhini kinamtii yeye kipende kisipende? Na kwake watarejeshwa wote".* [3:83]

Uislamu ni Dini pekee yenye uwezo wa kutosheleza mahitaji yote ya mwanadamu ya kimwili, kihisia na kiroho. Uislamu umeweka mwongozo juu ya vyakula na vinywaji, ukabainisha vile vilivyo vizuri

vinavyofaa na vile vibaya vinavyomdhuru mwanadamu. Uislamu umeweka utaratibu wa kumtakasa mwili na roho ya mwanadamu. Uislamu unazingatia hisia za mwanadamu na umetoa mwongozo ni vipi mwandamu afanye anapokuwa katika furaha na ni vipi afanye anapokuwa katika matatizo na huzuni.

Uislamu ni mfumo wa maisha uliokamilika. Unamuongoza mwanadamu namna ya kuendea kwa usahihi kila kipengele cha maisha yake. Uislamu unamuelekeza mwanadamu namna atakavyoendesha maisha yake binafsi, maisha ya familia na maisha ya jamii. Uislamu una mfumo kamili wa siasa, utamaduni, uchumi, sheria, elimu na iada maalum. Katika Uislamu utenganisho wa siasa na dini, uchumi na dini au utamaduni na dini haupo na haujulikani. Uislamu ni mfumo kamili wa maisha usiohitaji kukopa chochote kutoka kwenye mifumo ya wanadamu.

Uislamu ni dini inayofuatwa na wanadamu wote kuanzia wa kwanza mpaka wa mwisho. Dini inayofuatwa na nchi zote ulimwenguni. Dini isiyo na ubaguzi wa kabila, lugha, rangi wala taifa. Waislamu wote ulimwenguni ni ndugu moja na lengo lao ni moja la kusimamisha Uislamu ulimwenguni. Mitume wote kuanzia Adam (a.s.) mpaka Muhammad (s.a.w.) wameletwa kufundisha Uislamu na kuusimamisha.

Uislamu ni dini ya amani. Uislamu ndio utaratibu wa maisha pekee unaoweza kusimamia haki za binadamu kwa kuwa unafuata sheria madhubuti kutoka kwa Allah (s.w.). Sheria zinazotungwa na kusimamiwa na mwanadamu zina kasoro nyingi na upungufu mwingi. Zina upendeleo na ubinafsi. Zimewekwa kuwalinda walioziitunga. Mara nyingi hukumu inaytolewa kutokana na sheria hizi ni ya kuwadhulumu wengine na kuwapendelea wengine. Qur'an imebainisha wazi kuwa:

وَمَن لَّمْ يَحْكُم بِمَآ أَنزَلَ ٱللَّهُ فَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ
ٱلظَّٰلِمُونَ ﴿٤٥﴾

*"... Na Wasiohukumu kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhalimu".* [5:45]

Sheria za Uislamu zinawahukumu wote sawa. Hakuna aliye juu ya sheria. Kiongozi wa ngazi yoyote ile katika Uislamu ni mtumishi wa watu na anaemkosea yeyote katika jamii, huhukumiwa kwa sheria moja sawa na mwanajamii yoyote. Sheria ya Kiislamu haibagui tajiri na masikini, mtumwa na muungwana, mtawala na mtawaliwa, bali wote wako sawa mbele ya sheria. Kila mmoja hupewa haki yake inayostahiki. Pia Uislamu unawaamrisha waumini wote kwa pamoja wasimame kidete kuamrisha mema yanayoleta kheri katika jamii, na kutokomeza maovu yanayoleta shari na kuvuruga amani katika jamii.

Uislamu ndio dini pekee yenye taasisi maalum za kujenga utu wa mwanadamu. Taasisi hizi ni kusimamisha swala, kutoa zaka, na sadakat, kufunga na kuhiji pamja na ibada za sunnah zinazoambatana na taasisi hizi. Taasisi hizi ambazo zimeitwa nguzo za Uislamu, humuandaa mwanadamu aweze kuishi maisha ya kumtii Allah (s.w.) katika kila kipengele cha maisha.

Uislamu, kutokana na sifa zote hizi ndio dini pekee inayoiwezesha jamii ya wanadamu kuishi kwa furaha na amani. Uislamu ndio dini pekee anayoiridhia Allah (s.w.):

إِنَّ ٱلدِّينَ عِندَ ٱللَّهِ ٱلْإِسْلَٰمُ ۗ

*"Bila shaka dini (ya haki) mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu..."* [3:19]

Mwenye kuchagua dini nyingine na kuacha Uislamu atakuwa amekosa busara na atakuwa amepotea njia kweli kweli. Na bila shaka atakuwa miongoni mwa wenye khasara hapa duniani na huko Akhera.

وَمَن يَبْتَغِ غَيْرَ ٱلْإِسْلَٰمِ دِينًا فَلَن يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِى ٱلْءَاخِرَةِ مِنَ ٱلْخَٰسِرِينَ ﴿٨٥﴾

*"Na anayetaka dini isiyokuwa ya Kiislamu, basi haitakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa katika wenye khasara (kubwa kabisa)".* [3:85]

## Maana ya Uislamu

*Islam* ni neno la Kiarabu lenye maana ya kutii kwa unyenyekevu au kujisalimisha kwa ukamilifu. Kutokana na maana hii Uislamu ni Dini ya kumtii Allah (s.w.) kwa unyenyekevu au dini ya kujisalimisha moja kwa moja kwa Allah (s.w.). Kiutendaji, Uislamu ni utaratibu wa maisha unaofuata barabara sheria za Allah (s.w.) katika kila kipengele cha maisha ya jamii. Yaani ni utaratibu wa maisha ambao sheria za Allah (s.w.) hufuatwa katika kuendesha maisha ya mtu binafsi, maisha ya familia, uchumi, utamaduni, siasa, sheria, mfumo wa elimu na katika kila kipengele kinachohusu maisha ya jamii.

## Maumbile yote yamesilimu

Maumbile yote yaliyomo mbinguni na ardhini yanatii sheria za maumbile zinazowekwa na Muumba. Katika Qur'an tunafahamishwa:

أَفَغَيْرَ دِينِ ٱللَّهِ يَبْغُونَ وَلَهُۥٓ أَسْلَمَ مَن فِى ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ طَوْعًا وَكَرْهًا وَإِلَيْهِ يُرْجَعُونَ ﴿٨٣﴾

*"Je! Wanataka Dini isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu, na hali kila kilichomo mbinguni na ardhini kinamtii Yeye kipende kisipende? Na kwake watarejeshwa wote."* [3:83]

Kutokana na aya hii wanyama wote ni Waislamu kwa kuwa wanafuata sheria zote za maumbile. Mimea yote ni Miislamu kwa kuwa inafuata barabara sheria za Baiolojia alizoziweka Allah (s.w.). Kila kilichomo ardhini hufuata sheria za maumbile. Jua, mwezi, dunia, sayari na nyota vyote vimejitiisha kwa ukamilifu kwa sheria za Allah (s.w.). Jua daima huchomoza mashariki na huchwea magharibi. Mwezi huandama kila mwezi. Dunia huzunguka kila siku katika muhimili wake na kutupatia usiku na mchana.

Kila kilichomo angani, jua, mwezi, nyota, n.k. hufuata barabara sheria za maumbile alizoziweka Allah (s.w.). Hivyo kila kilichomo mbinguni na ardhini ni Kiislamu, yaani kinatii sheria za Allah (s.w.) kwa ukamilifu.

Miili yetu inatii kwa ukamilifu sheria za maumbile alizoziweka Allah (s.w.). Chakula husagika tumboni kwa kufuata sheria za Allah. Chakula baada ya kusagwa tumboni hubadilika kuwa damu na kuzunguka mwilini kwa kufuata sheria za maumbile. Mapafu hufanya kazi yake kwa kufuata heria ya Allah. Moyo hudunda kwa kufuata sheria za Allah. Miili yetu hunawiri kwa kufuata sheria za maumbile. Usingizi hutujia kwa kufuata sheria za maumbile alizoziweka Allah (s.w.). Kwa ujumla miili yetu hufanya kazi kadhaa wa kadhaa zinazotuwezesha kuishi kwa kufuata sheria za maumbile. Sisi wenyewe hatuna mchango wowote tunaotoa. Hivyo miili yetu ni Miislamu kama Allah (s.w.) anavyotufahamisha katika Qur'an:

فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا ۚ فِطْرَتَ ٱللَّهِ ٱلَّتِى
فَطَرَ ٱلنَّاسَ عَلَيْهَا ۚ لَا تَبْدِيلَ لِخَلْقِ ٱللَّهِ ۚ ذَٰلِكَ
ٱلدِّينُ ٱلْقَيِّمُ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ ٱلنَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ

*"Basi uelekeze uso wako katika dini iliyo sawa sawa. Ndilo umbile Mwenyezi Mungu alilowaumbia watu, (yaani dini*

*hii ya Kiislamu inayowafikiana barabara na umbo la binadamu). Hakuna mabadiliko katika maumbile ya viumbe vya Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo dini iliyo ya haki lakini watu wengi hawajui".* [30:30]

**Je, nafsi zetu zimesilimu kama miili yetu?**

Si kila nafsi iliyo silimu. Miili yetu haina hiari ya kuamua kusilimu au kutosilimu. Inalazimika kufuata barabara sheria za maumbile ili tubakie kuishi. Tofauti na miili yetu, nafsi zetu zinahiari ya kutii maamrisho ya Allah (s.w.) na kuacha makatazo yake au kutotii. Hivyo anayemtii Allah (s.w.) kwa unyenyekevu kwa kutekeleza kwa ukamilifu maamrisho yake yote na kuacha makatazo yake yote huwa ni Muislamu. Anayeamua kwa hiari yake mwenyewe kutotii sheria za Allah (s.w.) huwa ni Kafiri.

**Nani Muislamu**

Muislamu ni yule aliyejisalimisha moja kwa moja kwa Allah (s.w.) kwa kufuata sheria zake zote. Hufuata maamrisho yote ya Allah (s.w.) na huacha makatazo yake yote. Hufuata utamaduni alioridhia Allah(s.w.). Huchuma kwa kuchunga mipaka ya Allah(s.w.). Huhukumia kila jambo kwa kufuata sheria za Allah(s.w.). Hufuata siasa na uongozi unaochunga mipaka ya Allah(s.w.). Hucheza na kujiburudisha kwa kuchunga mipaka ya Allah (s.w.). Huendesha maisha yetu yote ya binafsi, familia na ya jamii kwa kufuata barabara sheria za Allah (s.w.).

**Uislamu wa kufuata nusu nusu haukubaliki**

Yule anayejiita Muislamu lakini hafuati sheria zote za Allah(s.w.), lakini hufuata baadhi ya sheria na baadhi huzikufuru, huyo si Muislamu bali Munafiki. Watu wanaofuata baadhi ya maamrisho ya Allah na hukufuru baadhi ya maamrisho, Allah (s.w.) amewalaani hapa duniani na huko akhera. Allah (s.w.) anatukumbusha katika Qur'an kutokanana tabia waliyokuwa nayo Mayahudi:

أَفَتُؤْمِنُونَ بِبَعْضِ ٱلْكِتَـٰبِ وَتَكْفُرُونَ بِبَعْضٍ ۚ فَمَا
جَزَآءُ مَن يَفْعَلُ ذَٰلِكَ مِنكُمْ إِلَّا خِزْىٌ فِى ٱلْحَيَوٰةِ
ٱلدُّنْيَا ۖ وَيَوْمَ ٱلْقِيَـٰمَةِ يُرَدُّونَ إِلَىٰٓ أَشَدِّ ٱلْعَذَابِ ۗ

*"…Je! Mnaamini baadhi ya kitabu na kukanusha baadhi (yake)? Basi hakuna malipo kwa mwenye kufanya haya katika nyinyi ila fedheha katika maisha ya dunia na siku ya Kiyama watapelekwa katika adhabu kali…"* [2:85]

Kutokana na aya hii, Uislamu wa kuswali, kufunga na kuhiji na wakati huo huo kuwatii viongozi wanaoongoza kinyume na sheria za Allah (s.w.), hautambuliki mbele ya Allah(s.w.). Kwa ujumla wale wanaojiita Waislamu lakini katika kuendesha maisha yao ya kila siku katika uchumi, siasa, utamaduni, sheria n.k. na hawazingatii mipaka ya Allah (s.w.) aliyoiweka, si Waislamu bali ni Makafiri, Madhalimu na Mafaasiq kama Allah (s.w.) anavyotufahamisha katika Qur'an:

وَمَن لَّمْ يَحْكُم بِمَآ أَنزَلَ ٱللَّهُ فَأُو۟لَـٰٓئِكَ هُمُ
ٱلْكَـٰفِرُونَ ﴿٤٤﴾

*"…Na wasiohukumu kwa yale aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri".* [5:44]

وَمَن لَّمْ يَحْكُم بِمَآ أَنزَلَ ٱللَّهُ فَأُو۟لَـٰٓئِكَ هُمُ
ٱلظَّـٰلِمُونَ ﴿٤٥﴾

*"… Na wasiohukumu kwa yale aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhalimu".* [5:45]

وَمَن لَّمْ يَحْكُم بِمَآ أَنزَلَ ٱللَّهُ فَأُو۟لَـٰٓئِكَ هُمُ ٱلْفَـٰسِقُونَ ﴿٤٧﴾

*"… Na wasiohukumu kwa yale aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio Mafasiki".* [5:47]

Ili mtu awe Muislamu wa kweli hana budi kuitikia wito wa Allah (s.w.) ufuatao:

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱدْخُلُوا۟ فِى ٱلسِّلْمِ كَآفَّةً وَلَا تَتَّبِعُوا۟ خُطُوَٰتِ ٱلشَّيْطَـٰنِ ۚ إِنَّهُۥ لَكُمْ عَدُوٌّ مُّبِينٌ ﴿٢٠٨﴾

*"Enyi mlioamini! Ingieni katika hukumu zote za Uislamu, wala msifuate nyayo za shetani, kwa hakika yeye kwenu ni adui dhahiri".* [2:208]

Kufuata baadhi ya sheria za Allah na kukufuru baadhi ya nyingine ni kufuata nyayo za shetani, yaani ni kupotea. Na mwenye kumfuata shetani ataingia naye motoni.



## Zoezi la Pili

1. (a) Imani maana yake nini?
   (b) Taja nguzo za Imani zilizomo katika Hadith Aliyosimulia na Umar (r.a) kupitia Muslimu.
2. Orodhesha sifa Tano za Muumini wa kweli

3. (a) Nini maana ya Shirk ?
   (b) Mtu anaweza kumshirikisha Allah (s.w) katika namna ngapi?

4. Ni matendo gani mtu akiyafanya atakuwa anamshirikisha Allah (s.w)?

5. Taja mambo matatu yanayomthibitisha mtu anayeamini Qudra ya Allah (s.w)

6. (a) Dini maana yake nini?
   (a) Kuna aina ngapi za dini?
   (b) Dini sahihi hutambulika kwa kuwa na sifa zipi?

7. Eleza kwa kifupi
   (a) Maana ya Uislamu
   (b)Maana ya Muislamu

8. Bila shaka Dini mbele ya Allah (s.w) ni Uislamu. Kwanini na kwasababu gani?

Somo la 3 Sunnah

# Kuhifadhiwa Sunnah ya Mtume (s.a.w.)

Katika istilahi ya Kiislamu Sunnah ya Mtume Muhammad (s.a.w.) ni mwenendo au matendo ya Mtume ambayo ni sehemu ya utume wake. Waumini wanalazimika kufuata Sunnah ya Mtume (s.a.w.) kwa kuigiza tabia na mwenendo wa Mtume (s.a.w.) kwa kufuata aliyowaamrisha na kuacha aliyowakataza.

Tunajua Sunnah ya Mtume (s.a.w.) kutokana na Hadith. Katika Istilahi ya Kiislamu Hadithi ni simulizi au taarifa tuzipatazo kutoka kwa Maswahaba wa Mtume (s.a.w.) juu ya tabia na mwenendo wa Mtume, juu ya maamrisho na makatazo yake yaliyofanywa mbele yake na akaridhika nayo.

Maswahaba wa Mtume ni wale Waislamu walioshi pamoja na Mtume (s.a.w.) na wakawa naye bega kwa bega katika kuusimamisha Uislamu.

**Njia zilizotumika kuhifadhi Sunnah ya Mtume (s.a.w)**

Njia mbili kubwa zifuatazo zimetumika katika kuhifadhi Sunnah.

(a)Maswahaba kuhifadhi mafundisho ya Mtume (s.a.w.) vifuani mwao na kuigiza mwenendo wake katika maisha yao ya kila siku.

(b)Mafundisho ya Mtume (s.a.w.) na mwenendo wake kuhifadhiwa katika maandishi.

(a)Maswahaba kuhifadhi mafundisho ya Mtume (s.a.w.) vifuani mwao

Njia ya kwanza iliyotumika kuhifadhi Sunnah ya Mtume (s.a.w.) ni kutia matendoni mafundisho ya Mtume (s.a.w.) na kuigiza mwenendo

wake. Watu wa kwanza kumuigiza Mtume (s.a.w.) na kuweza kusimulia kwa usahihi mafundisho yake na mwenendo wake ni wale waliokuwa karibu sana naye katika muda mwingi wa maisha yake. Maswahaba walio wengi walipenda sana kuwa karibu na Mtume (s.a.w.) ili kujifunza Uislamu kwake. Wengine walifikia kiwango cha kuwekeana zamu za kukaa na Mtume kama alivyo simulia Umar bin Khattab (r.a.):

> *"Nilikuwa mimi na jirani yangu katika ukoo wa Banii Umayyah tunawekeana zamu ya kwenda kwa Mtume (s.a.w.) kila siku, siku ninapokwenda mimi namletea habari ya siku ile na anapokwenda yeye anafanya hivyo hivyo".*
> [Al-Bukhari]

Hata wale walioishi mbali na Mtume (s.a.w.) walituma wawakilishi wao kuja kukaa na Mtume na kujifunza kutoka kwake ili hatimaye warudipo kwa jamaa zao wakawe waalimu wa nadharia na matendo.

(b)Kuhifadhiwa Sunnah katika maandishi

Hadithi zilianza kuwekwa katika maandishi tangu wakati wa Mtume (s.a.w.). Mwanzoni mwa Utume. Mtume (s.a.w.) aliwakataza maswahaba wake kuandika hadithi ili wasije kuchanganya maneno ya Allah (s.w.) na maneno yake. Wakati huu wa mwanzo Mtume (s.a.w.) aliruhusu kuandikwa kwa Qur'an tu na aliwachagua waandishi maalumu. Baadaye Mtume (s.a.w.) alipoona maswahaba wake wamezoea vya kutosha aya za Qur'an kiasi cha kuweza kutofautisha maneno yake na yale ya Allah (s.w.), aliwaruhusu kuandika hadith. Wakati mwingine kabla hawajaanza kuandika au kutoa rai yao walikuwa wakimuuliza kwanza Mtume, "Ee Mtume wa Allah, hiyo ni rai yako au ni amri ya Allah (s.w.)?"

Hivyo uandishi wa Hadith ulianza kidogo kidogo tangu wakati wa Mtume (s.a.w.) na kushamiri kila muda ulivyosonga mbele mpaka kufikia kiwango cha juu cha uandishi wa vitabu vya Hadith vilivyopo hivi leo.

## Historia fupi ya Uandishi wa Hadith

Haja ya kuhifadhi Sunnah ya Mtume (s.a.w.) katika maandishi iliongezeka kila muda ulivyosonga mbele hasa baada ya kutawafu Mtume (s.a.w.). Historia ya kuhifadhiwa Sunnah ya Mtume (s.a.w.) mpaka kufikia kwenye uandishi wa vitabu vya Hadith sahihi vilivyopo hivi leo inabainika kwa kuzingatia vipindi vinne vifuatavyo:

### *(a)Uandishi wa Hadith wakati wa Mtume (s.a.w.)*

Wakati wa Mtume (s.a.w.) hapakuwa na uandishi mkubwa wa Hadith kwa sababu kubwa zifuatazo:

Kwanza, Mtume mwenyewe alikuwepo, hivyo kilichokuwa muhimu kwa maswahaba ni kufuata mafundisho ya Mtume na kuigiza mwenendo wake. Kila walipokuwa katika utendaji walimwendea Mtume.

Pili, Maswahaba katika kipindi hiki walijishughulisha sana na kuandika, kusoma na kuhifadhi Qur'an moyoni na kuitekeleza katika maisha ya kila siku.

Tatu, katika wakati huu, Mtume (s.a.w.) na maswahaba wake walijishughulisha sana katika harakati za kuuhami Uislamu ambao ulikuwa umesongwa sana na maadui wake ambao walipania sana kumuua Mtume, Waislamu na Uislamu.

Kutokana na sababu hizi, uandishi wa Hadith haukupewa nafasi nzito katika kipindi hiki. Hadith nyingi zilibakia katika matendo na vifuani mwa maswahaba.

### *(b) Uandishi wa Hadith katika kipindi cha Maswahaba*

(11-100A.H)

Kipindi hiki ni kuanzia pale alipotawafu Mtume (s.a.w.) mpaka kutawafu kwa Swahaba wa mwisho. Swahaba wa mwisho, Anas bin Malik alitawafu 914H. Hiki ni kipindi cha Makhalifah wanne

waongofu - Abu Bakar (r.a.). Ni katika kipindi hiki ambapo dola ya Kiislamu ilitawala sana mashariki na magharibi. Matatizo mengi ya wakati huo yalitatuliwa kwa kutegemea hukumu za Hadith zilizohifadhiwa vifuani mwa Maswahaba.

Katika kipindi cha Makhalifa wanne waongofu (11-40 A.H) kazi ya uandishi wa Hadith ilikuwepo, lakini si katika kiwango kikubwa. Vitabu mashuhuri vya Hadith vilivyokuwepo ni:

(1) *Al-Qatadaya* cha Ally bin Abittwalib (r.a.)
(2) Juzuu ya Hadith (Pamphlet) ya Ibn Abbas (r.a.)

Katika kipindi hiki haja kubwa ya kuhifadhi Hadith katika maandishi ilionekana baada ya kutokea matatizo ya kisiasa kati ya kundi la Ally na Muawiyah. Hadith zilianza kwa maslahi ya kundi. Vile vile kipindi hiki watu walizusha Hadith za uongo ili kutetea maslahi yao.

### *(c) Uandishi wa Hadith katika kipindi cha wafuasi wa maswahaba - Tabi'iin (101-200 A.H)*

Hiki ni kipindi cha wafuasi wa maswahaba wa Mtume (s.a.w.) - Tabi'iin kilichokuwa karne ya pili Hijiriyyah (101-200 A.H). Katika kipindi hiki walitokea wanachuoni wengi waliojizatiti katika kazi ya ukusanyaji wa Hadith katika vituo na miji mbalimbali ya Kiislamu kama vile Makkah, Madinah, Baghdad, Basra, Khurasah na Kufa.

Ni katika kipindi hiki walitokea Maimamu wanne mashuhuri ambao walitoa Fat-wa mbalimbali kwa kutumia Qur'an na Hadith sahihi walizozikusanya. Maimamu hawa ni:

(1) Abu Hanifa al-Numan bin Thabit

Aliyezaliwa Kufa nchini Iraq 80 A.H na kufariki 150 A.H (80-

150 A.H). Alifutu mas'ala mbalimbali ya Kiislamu kwa hoja ya Qiyasi kwa kuzingatia Qur'an, Hadith Sahihi na Ijma (makubaliano ya wanachuoni). Hakuandika kitabu chochote cha Hadith lakini alikuwa mwanachuoni mkubwa aliyetumia Qur'an na Hadith alizozikusanya katika vita bu vyake vya Fiqh.

(2) Malik bin Anas:

Aliyeishi Madina kati ya 95 A.H na 179 A.H aikuwa ni mwanachuoni mkubwa aliyefutu masuala ya Uislamu kwa kutegemea Qur'an na Hadith tu. Alianzisha umoja wa 'Ahli Hadith' ambao lengo lake lilikuwa kukusanya Hadithi na kuzitekeleza katika matendo. Aliandika kitabu cha Hadith kinachoitwa "*Al-Muwatta".*

(3) Muhammad bin Idris-al Shafii:

Aliyezaliwa Palestina katika mji wa Ghazzal 150 A.H na kufariki 240 A.H. Naye alikuwa mwanachuoni mkubwa aliyefutu masuala mbalimbali ya Fiqh kwa kutumia Qur'an na Hadith.

(4) Ahmad bin Hambal:

Alizaliwa Baghdad 164 A.H na kufariki 241 A.H. Alikuwa mwanachuoni mkubwa wa Hadith na aliandika kitabu cha Hadith mashuhuri kwa jina la *Isnad ya Ahmed bin Hambal.*

(d) Uandishi wa Hadith kipindi cha Tabii Tabi'iin (201 - 300 A.H)

Katika karne ya tatu Hijiriyyah, kazi ya ukusanyaji na uandishi wa Hadith ilipamba moto sana kutokana na haja iliyokuwepo. Pia kutokana na kuzuka kwa watu waliomzulia Mtume (s.a.w.) kwa kutunga Hadith za uwongo, Wanazuoni wa Hadithi wa kipindi hiki walikuwa waangalifu mno katika kukusanya na kuandika Hadith. Walitembea mji hadi mji na kukusanya Hadithi nyingi. Kisha walizichambua Hadith hizo kwa kutumia vigezo mbalimbali. Waliandika chache tu katika vitabu vyao ktika nyingi walizozikusanya. Kwa mfano Imamu Bukhari alikusanya Hadithi 600,000 lakini kutokana na uangalifu na tahadhari kubwa aliyoichukua katika kuhakikisha usahihi wa Hadith alizozipokea ni Hadithi 7275 tu

alizoziandika katika kitabu chake cha Sahihi Al-Bukhari. Kutokana na umakini huu vitabu vya Maimamu wa Hadidth wa kipindi hiki vilipewa heshima ya Usahihi. Maimamu mashuhuri wa Hadith waliotokea katika kipindi hiki cha historia ambao vitabu vyao vya Hadith vilipewa heshima ya Usahihi ni hawa sita wafuatao:

(1) Imam Muhammad bin Ismail Abu 'Abd-Allah el Ju'ufi - jina mashuhuri Imamu Bukhari aliyezaliwa Urusi katika mji wa Bulehena 194 A.H (810 a.d.) Na kufariki 256 a.h (870 A.D.). Kitabu chake cha Hadith kinajulikana kwa jina la *Sahihi Al-bBukhari*, kina Hadithi 7,275.

(2) Imamu Abul Husain Muslim bin al-Hajjaj, anayejulikana kwa jina la Imamu Muslim alizaliwa 202 A.H (817 A.D.) na kufariki 261 A.H (875). Kitbu chake mashuhuri cha Hadith kinajulikana kwa jina la *Sahihi Muslim*, kina Hadith 9,200.

(3) Imamu Abu Dawud aliyezaliwa 203 A.H katika mji wa Khurasan na kufariki 275 (888 A.D.). Kitabu chake cha Hadith kinaitwa *Sunnah ya Abu Daud*, kina hadithi 4,800.

(4) Imamu Abu Isa Muhammed bin Isa Sarwa bin Shaddad anayejulikana kwa jina la Imam At-Tirmidh alizaliwa katika mji wa Tirmidh 209 A.H na kufariki 279 A.H (892 A.D.). Kitabu chake cha Hadith kinaitwa *Jami'u ya Tirmidh.*

*(5)* Muhammed bin Yazid anayejulikana kwa jina la Ibn Majah alizaliwa 209 A.H na kufariki 295 A.H. Kitabu chake kinaitwa *Sunnah ya Ibn Majah.*

(6) Imamu Abu 'Abdur-Rahman Ahmed bin An-Nasai alizaliwa 214 na kufariki 303 A.H (315 A.D.). Kitabu chake cha Hadith kinaitwa *Sunnah ya An-Nasai.*

## Vigezo vya Hadith Sahihi

Hadithi ni tofauti na Qur'an. Qur'an imehifadhiwa na mwenyewe Allah (s.w.), na hapana mtu anayeweza kuipotosha kamwe. Ahadi ya kuhifadhi Qur'an tunaipata katika aya zifuatazo:

إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا ٱلذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُۥ لَحَٰفِظُونَ ﴿٩﴾

*"Hakika sisi ndio tulioteremsha mawaidha haya (hii Qur'an) na hakika sisi ndio tutakaoyalinda".* [15:9]

لَّا يَأْتِيهِ ٱلْبَٰطِلُ مِنۢ بَيْنِ يَدَيْهِ وَلَا مِنْ خَلْفِهِۦ ۖ تَنزِيلٌ مِّنْ

حَكِيمٍ حَمِيدٍ ﴿٤٢﴾

*"Hakitakifikia batili mbele yake wala nyuma yake, kimeteremshwa na Mwenye Hekima Ahimidiwaye".* [41:42].

Tofauti na Qur'an, Hadith za Mtume (s.a.w.) hazina ahadi ya hifadhi ndani ya Qur'an. Hivyo watu waovu, imetokezea katika historia kutunga Hadith za uwongo na kumsingizia Mtume. Wanazuoni wa Hadith walipogundua jambo hili la watu kumzulia Mtume, walikuwa makini katika kukusanya na kuandika Hadith. Wakaweka vigezo vya kuchunguza usahihi wa mapokezi -*Isnad* na usahihi wa *Matini* yenyewe ya Hadith.

## Uchunguzi wa usahihi wa Isnad

Katika kuchunguza usahihi wa wasimulizi au wapokezi wa Hadith wanazuoni wa Hadith wamefanya yafuatayo:

(1)Kuchambua msururu wa wapokezi kuwa umekwenda mpaka kumfikia Mtume (s.a.w.) au umeishia katikati. Yaani walichunguza kuwa huyo mtu wa kwanza aliyeeleza kutoka kwa Mtume (s.a.w.)

alikuwepo wakati wa Mtume wakati tukio hilo au habari hiyo ilipokuwa ikielezwa au iliposhuhudiwa na Mtume (s.a.w.).Kama alikuwepo, alikuwa na umri gani? Alishafikia balegh au la?

(2)Baada ya Isnad kukamilika, unafuatia uchambuzi wa historia ya maisha ya kila msimuliaji. Ili hadithi ikubalike kuwa ni sahihi kila mpokezi lazima awe na sifa zifuatao:

(a)Majina yake yote yafahamike, hata jina la utani.
(b)Awe ni mkweli.
(c)Awe mcha-Mungu.
(d)Awe hajawahi kufanya kosa kubwa kama vile kusema uongo, wizi, uzinzi n.k.
(e)Awe ni mwenye tabia njema kwa ujumla.
(f)Awe mwenye akili na mwenye kumbukumbu safi.

## Uchunguzi wa usahihi wa Matin

Pamoja na kuwa na usahihi katika upokezi, bado habari inayotolewa katika hadith (Matin) inaweza isiwe sahihi. Matini ya Hadith itakuwa sahihi iwapo itatosha vigezo vifuatavyo:

(a)Matini isipingane na Qur'an.
(b)Isipingane na Hadith nyingine iliyothibitishwa kuwa ni sahihi.
(c)Isiwe inamzulia Mtume.
(d)Isipingane na ukweli unaothibitika.
(e)Isipingane na hakika inayothibitisha historia.
(f)Isiwe na maneno ya uwongo ndani yake.
(g)Isiwe imeahidi adhabu kali sana kwa kosa dogo sana au isiwe imeahidi malipo makubwa sana kwa wema mdogo sana.

## Daraja za Hadith

Kulingana na kiwango cha Usahihi, Hadith zimegawanyika katika daraja zifuatazo:
(a)Hadith Sahihi ni ile ambayo inakamilika katika Isnad na Matini

yake. Yaani imetosheleza vigezo vyote vya Isnad na Matini.

(b)Hadith Hassan ni ile inayokaribia sifa za Hadith sahihi, bali wasimulizi wake wamekuwa dhaifu katika kumbukumbu (udhibitifu) ukiwalinganisha na wale wasimulizi wa Hadith Sahihi.

(c)Hadith Dhaifu ni ile Hadith ambayo miongoni mwa wasimulizi wake wana kasoro zilizojitokeza. Hadith za namna hii si zenye kuaminika.

(d)Hadith maudhu ni Hadithi ya uzushi ambayo inapingana na vipengele vya vigezo vya Hadith Sahihi.

## Mgawanyiko wa Hadith katika umaarufu

Pia Hadith zimegawanywa ili kuonyesha kiwango cha umaarufu wake katika kukubalika katika makundi mawili yafuatayo:

(a)Hadith Mutawatir - ni ile yenye kusimuliwa na watu wengi wanne au zaidi wote wakiwa na sifa zilizokubalika. Pia Hadith za aina hii hukubalika kwa watu wote na wa nyakati zote. Yaani watu wote wenye ujuzi wa Hadith hawana mushkeli nayo.

(b)Hadith Ahad ni ile ambayo japo wasimulizi wake ni wenye sifa zilizokamilika, hawana mfungamano mzuri mpaka kufikia kwa Mtume (s.a.w.). Hadith za namna hii hazikubaliki kwa watu wengine, si zenye kuaminika.
Aina ya Hadith

## Kuna aina kuu mbili za Hadith:

(a)Hadithin-Nabawi ni ile Hadith ambayo Matini yake inamnukuu Mtume moja kwa moja. Mfano wa Hadith Nabawiyyi:

> *Aisha (r.a.) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Yeyote atakayeingiza jambo jipya katika mambo yetu (dini yetu) lisilokuwa la humu litakataliwa".* [Bukhari na Muslim]

(b)Hadith Qudus ni ile Hadith ambayo Matini yake ni maneno ya Allah (s.w.) anayenukuliwa na Mtume (s.a.w.). Mfano wa Hadith Qudus:

> *"Abu Hurairah (r.a.) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Allah (s.w.) amesema: "Ni mwingi wa kujitosheleza kwa kiasi kwamba si hitaji mshirika yoyote. Kwa hiyo yeyote yule atakayefanya amali kwa ajili ya mtu mwingine pamoja na mimi nitaikataa hiyo amali na kuipeleka kwa yule aliyenishirikisha naye".* [Muslim, Ibn Majah]



# Zoezi la Tatu

1. (a) Istilahi ya Kiislamu inaeleza kuwa Sunnah ni nini?
   (b) Kwanini Waumini wa Kiislamu wanalazimika kufuata Sunnah?

2. Taja njia kuu zilizotumika kuhifadhi Sunnah ya Mtume (s.a.w)

3. (a) Taja vipindi vinne vya Uandishi wa Hadith
   (b) Orodhesha wakusanyaji wa maarufu wa Hadith za Mtume (s.a.w) pamoja na vitabu vyao.

4. (a) Eleza maana ya Istilahi zifuatazo
      (i) Hadith
      (ii) Matini
      (iii) Isnad
   (b) Isnad na Matini ya Hadith sahihi inatakiwa iwe na sifa zipi?

5. Bainisha:
      (a) Daraja za Hadith
      (b) Makundi ya Hadith kwa mujibu wa Umaarufu
      (c) Aina kuu za Hadith

# Somo la 4 Fiqh

# Lengo la Maisha ya Wanadamu

**Kwanini watu wameumbwa?**

Hakuna anaeweza kujibu swali hili isipokuwa yule aliyewaumba Muumba wa watu anatufahamisha katika Qur'an:

وَمَا خَلَقْتُ ٱلْجِنَّ وَٱلْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥٦﴾

*"Sikuwaumba majini na watu, ila (tu) waniabudu".* [51:56]

Aya hii inatufahamisha kuwa lengo la kuumbwa watu ni kumuabudu Mwenyezi Mungu au kufnya ibada ya Mwenyezi Mungu.

**Maana ya Ibada katika Uislamu**

*Ibada* ni neno la Kiarabu linalotokana na neno *Abd* lenye maana ya uja au utumwa. Kwahiyo neno *ibada* lina maana ya kutumikia, kutumwa.

Kwa maana hii, kumuabudu Allah ni kumtumikia Allah kwa unyenyekevu. Kumtumikia Allah (s.w.) ni kufuata kwa unyenyekevu maarisho yote ya Allah (s.w.) na kuacha makatazo yake yote. Kwa maana hii, Muislamu anatakiwa awe katika ibada kwa muda wote wa saa 24. Yaani analazimika kufuata sheria za Allah (s.w.) katika kila jambo analolifanya katika saa 24.

Analazimika kumuabudu Allah katika kutekeleza shughuli zake zote za binafsi, na shughuli zote za jamii kwa ujumla. Anatakiwa amuabudu Allah (s.w.) katika kutekeleza maamrisho mbalimbali

ya binafsi kama vile kusimamisha swala tano, kutoa zakat, kufunga na kuhiji, kuwa mkweli na muadilifu n.k. Anatakiwa amuabudu Allah katika uchumi, kwa kuzingatia mipaka ya halali na haramu aliyoiweka Mwenyezi Mungu. Anatakiwa amuabudu Allah (s.w.) katika utamaduni kwa kuchunga mipaka ya halali na haramu iliyowekwa katika kula na kunywa, katika mavazi na sitara, katika sherehe na mchezo n.k. Anatakiwa amuabudu Allah katika siasa kwa kufuata muongozo wa Allah (s.w) katika kuweka sera na maongozi ya jamii. Kwa ujumla mja atakuwa katika ibada katika kila jambo analolifanya iwapo atalifanya jambo hilo kwa kutaraji radhi za Allah (s.w.) na akawa anachunga mipaka ya halali na haramu aliyoiweka Allah (s.w.).

**Lengo la nguzo za Uislamu**

Nguzo za Uislamu na ibada za Sunnah zilizoambatanishwa nazo zimewekwa pale kwa lengo maalum. Zimewekwa pake kwa lengo la kumuandaa mja aweze kutenda mambo yake yote kwa kutii barabara sheria za Allah (s.w.). Mwenye kutekeleza ibada hizi maalum, yaani mwenye kusimamisha swala za faradhi na sunnah, mwenye kutoa zakat na sadakat, mwenye kufunga Ramadhani na funga nyingine za sunnah na mwenye kuhiji Makkah, huwa na tabia na nidhamu inayomuwezesha kuendesha maisha yake yote kwa kufuata sheria za Allah (s.w.). Hebu tuone namna kila nguzo ya Uislamu ilivyomuandaa Muislamu kuwa mja au mtumwa wa Allah (s.w.):

***1.Lengo la kutoa shahada mbili***

Shahada mbili humuandaa mja kuwa na yakini juu ya Allah (s.w.) na Mtume wake na huwa na yakini na yale Allah (s.w.) aliyoyateremsha kupitia kwa Mtume Muhammad (s.a.w.). Baada ya kuwa na yakini ya kuwepo Allah (s.w) na huwa na yakini kuwa Muhammad (s.a.w.) ni Mtume wake, muumini wa kweli hulazimika kuishi kwa kumtii Allah (s.w.) na Mtume wake kwa kufuata maamrisho

yote na kuacha makatgazo yote ya Allah (s.w.) na Mtume wake.

### *2.Lengo la kusimamisha swala*

Kusimamisha swala tano na swala za Sunnah humuwezesha mja kujizuilia na mambo maovu na machafu kama tunavyofahamishwa katika Qur'an:

ٱتۡلُ مَآ أُوحِيَ إِلَيۡكَ مِنَ ٱلۡكِتَٰبِ وَأَقِمِ ٱلصَّلَوٰةَۖ

إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ تَنۡهَىٰ عَنِ ٱلۡفَحۡشَآءِ وَٱلۡمُنكَرِۗ

*"Soma uliyoletewa wahay (uliyofunuliwa) katika kitabu na usimamishe swala. Bila shaka swala (ikiswaliwa vilivyo) humzuilia (huyo mwenye kuswali na) mambo machafu na maovu...".* [29:45]

Tunajifunza katika aya hii kuwa Muislamu anayesimamisha swala vilivyo huepukana na mambo ya aibu na maovu.Mambo maovu ni yale yote yanayompelekea mja kumuasi Mwenyezi Mungu kwa kuvunja amri zake. Hivyo swala humuandaa mja awe mtiifu kwa sheria za Allah.

Yule anayeswali na huku anaendeleakumuasi Mwenyezi Mungu kwa kuvunja sheria zake kadha wa kadhaa, awe na mashaka na swala zake. Bila shaka swala zake hakuzisimamisha vilivyo. Na bila shaka swala zake hazikupata malipo yoyote mbele ya Alalh (s.w.). Ni muhimu kila wakati Muislamu azingatie hililengo la swala lililobainishwa katika Qur'an na atathmini mara kwa mara swala zake.

### *3.Lengo la kutoa zakat na sadakat*

Lengo la kuamrishwa kutoa zakat na sadakat ni kuitakasa nafsi ya mtoaji, mpokeaji na kutakasa uchumi wa jamii. Mtume

(s.a.w.) aliamrishwa kuchukua sadakat kwa Waislamu waliofanya kosa la kutohudhuria vita vya Tabuku ili awatakase kwazo:

خُذْ مِنْ أَمْوَٰلِهِمْ صَدَقَةً تُطَهِّرُهُمْ

*"Chukua sadaka katika mali zao ili uwatakase kwazo...".* [9:103]

Zakat na Sadakat hutakasa nafsi ya mtoaji kutokana na yale yote maovu anayofanya mtu kutokana na utajiri wake. Huitakasa nafsi na kiburi, majivuno, ubakhili, uchoyo, upupiaji wa mali, uchumi haramu na kadhalika. Yule anayetoa zakat na sadakat halafu bado moyo wake hausafiki basi ajuekuwa utoaji wake una kasoro. Zakat na Sadakat huitakasa nafsi ya mpokeaji kutokan na husuda, kijicho, tamaa, unyonge na kadhalika.

Zakat na sadakat huitakasa jamii na utoaji na upokeaji wa rushwa na hongo. Huitakasa jamii na uchumi haramu unaotokana na riba, kamari, ulevi na vituo vya kuchochea zinaa. Uchumi uliojengwa katika msingi wa utoaji wa zakat na sadakat huistawisha na kuiendeleza jamii. Huiepusha jamii na vurumai zinazoletwa na uchumi uliojengwa katika msingi wa riba na kamari.

### *4.Lengo la Funga*

Lengo la funga limeelezwa katika Qur'an kuwa ni kumuandaa mja awe mcha Mungu:

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ كُتِبَ عَلَيْكُمُ ٱلصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى ٱلَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿١٨٣﴾

*"Enyi mlioamini! Mmeamrishwa kufunga kama walivyoamrishwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu".* [2:183]

Mcha Mungu (Muttaq) ni yule anayefuata kwa unyenyekevu maamrisho yote ya Allah (s.w.) na kuacha makatazo yake yote. Anayeishi kwa kufuata barabara sheria za Allah (s.w.) katika kuliendea kila jambo lake.

Mja anayefunga kwa ajili ya Allah huacha chakula chake, vinywaji vyake na vitu kadhaa wa kdhaa vilivyo halali na kujiepusha na makatazo yote ya Allah kwa ajili tu ya kutarajia radhi zake. Zoezi hili humzoesha mja kuwa muadilifu na mtiifu kwa Allah (s.w.).

Iwapo Muislamu anafunga Ramadhani na funga mbalimbali za Sunnah lakini bado anaendelea kumuasi Allah (s.w.), funga zake zitakuwa na kasoro na atakuwa hajapata thawabu (malipo mema) kutokana na funga zake. Hatuna budi kila mara kutathmini funga zetu, ili ziweze kutufikisha katika lengo lililokusudiwa.

### *5.Lengo la Hijjah*

Ibada ya Hijah humuandaa Muislamu kuwa tayari kujitoa muhanga kwa mali yake na nafsi yake katika kupigania dini ya Allah (s.w.). Pia ibada ya Hijjah huwakumbusha Waislamu kila mwaka kuwa wao ni ndugu moja na umma mmoja wenye kazi moja ya kusimamisha dini ya Allah (s.w.) ulimwenguni. Wale wanaotoka kuhiji lakini bado wanafanya vitendo viovu vinavyovunja dini ya Allah (s.w.), Hijjah yaoitkauwa si yenye kuswihi.

### *Waislamu ni Makhalifa wa Allah (s.w.) hapa ulimwenguni*

Ili mwanadamu aweze kumuabudu Allah (s.w.) ipasavyo katika kila kipengele cha maisha yake, Allah (s.w.) amempa cheo kikubwa hapa ulimwenguni. Hiki ni cheo cha Ukhalifa wa Allah (s.w.). Cheo cha Ukhalifa wa Allah (s.w.) ni cheo chenye hadhi kubwa sana mbele ya Allah (s.w.). Khalifa wa Allah (s.w.) ni yule mwenye mamlaka ya kuiendesha jamii kwa kufuata barabara sheria za Allah (s.w.). Hivyo anayestahiki cheo hiki kikubwa ni Muislamu tu aliyemuumini wa kweli kama Qur'an inavyotufahamisha:

وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ مِنكُمْ وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّـٰلِحَـٰتِ
لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِى ٱلْأَرْضِ كَمَا ٱسْتَخْلَفَ ٱلَّذِينَ مِن
قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ ٱلَّذِى ٱرْتَضَىٰ لَهُمْ
وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّنۢ بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ

*"Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri kuwa atawafanya Makhalifa katika ardhi kama alivyo wafanya Makhalifa wale waliokuwako kabla yao, na kwa yakini atawasimamishia dini yao aliyowapendelea na atawabadilishia amani baada aya khofu yao..."* [24:55]

Kutokana na aya hii tunajifunzakuwa ni waumini pekee wanaostahiki cheo hiki. Kwa maana nyingine ni Waislamu pekee wanaostahiki kuongoza ulimwengu. Ni Waislamu pekee watakaouongoza ulimwengu kwa kufuata mwongozo na sheria za Allah (s.w.) alizotushushia kupitia kwa Mitume wake na vitabu vyake. Utulivu na amani ya kweli inayotamaniwa na walimwengu hupatikana tu pale jamii itakapoongozwa na mwongozo wa Allah (s.w.) na kutawaliwa na sheria yake. Hivyo uongozi pekee unaoweza kuleta utulivu na amani katika jamii ni uongozi wa Kiislamu, unaofuata barabara mwongozo wa sheria za Allah (s.w). Uongozi wowote kinyume na uongozi wa Kiislamu, husababisha vurugu na khofu katika jamii. Hebu tutafakari aya ifuatayo:

ٱللَّهُ وَلِىُّ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ يُخْرِجُهُم مِّنَ ٱلظُّلُمَـٰتِ إِلَى
ٱلنُّورِ ۖ وَٱلَّذِينَ كَفَرُوٓا۟ أَوْلِيَآؤُهُمُ ٱلطَّـٰغُوتُ

يُخْرِجُونَهُم مِّنَ ٱلنُّورِ إِلَى ٱلظُّلُمَٰتِۗ أُوْلَٰٓئِكَ

أَصْحَٰبُ ٱلنَّارِۖ هُمْ فِيهَا خَٰلِدُونَ ﴿٢٥٧﴾

*"Mwenyezi Mungu ni mlinzi wa wale walioamini. Huwatoa katika giza na kuwaingiza katika nuru. Lakini waliokufuru walinzi wao ni matwaghuti. Huwatoa katika nuru na huwaingiza katika giza. Hao ndio watu wa motoni, humo watakaa milele".* [2:257]

GIZA katika aya hii ni maisha ya vurugu na khofu yanayosababishwa na kufuata miongozo na sheria zilizotungwa na wanadamu, na NURU hapa ina maana ya maisha ya utulivu na amani yanayopatikana kwa kufuata mwongozo wa sheria zote za Allah (s.w.). Hivyo ili utulivu na amani vipatikane katika jamii, Waislamu hawana budi kuwa viogozi (Makhalifa wa Allah (s.w.) katika jamii na kuhakikisha kuwa jamii inatawaliwa na sheria ya Allah (s.w.). Ni kosa kubwa mno mbele ya Allah (s.w.) Waislamu kuridhika kuongozwa na Matwaghuti (wapinzani wa sheria za Allah (s.w). Waislamu wanaoridhia uongozi wa Matwaghuti ni wanafiki na wameahidiwa adhabu ya moto pamoja na hao viongozi wao wa Kitwaghuti.

Waislamu wataweza tu kuwa Makhalifa wa Allah (s.w.) kwa kuitafsiri vizuri Qur'an na Sunnah katika uwanja wa siasa, uchumi, ustawi wa jamii, sheria, elimu, utamaduni na kadhalika.

### Kusimamisha Swala wakati wa Dharura

Kusimamisha swala tano kwa Waislamu ni faradhi ilyowekewa nyakati maalum kama Qur'n inavyosisitiza:

إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ كَانَتْ عَلَى ٱلْمُؤْمِنِينَ كِتَٰبًا مَّوْقُوتًا ﴿١٠٣﴾

*"...Kwa hakika swala kwa Waislamu ni faradhi iliyowekewa nyakati makhususi".* [4:103]

Kutokana na msisitizo huu, Muislamu kamwe hataiswali swala ya faradhi nje ya wakati wake ila kwa udhuru unaokubalika kisheria. Mtume (s.a.w.) amebainisha wazi kuwa nyudhuru za kuswali swala ya faradhi nje ya wakati wake makhususi ni mbili tu: (1) Kusahau (2) kupitiwa na usingizi pasina kukusudia. Bali Allah (s.w.) kwa rehema zake ametoa tahfif katika kusimamisha swala katika dharura za ugonjwa, kuwa safarini na vitani.

مَا يُرِيدُ ٱللَّهُ لِيَجْعَلَ عَلَيْكُم مِّنْ حَرَجٍ وَلَٰكِن
يُرِيدُ لِيُطَهِّرَكُمْ وَلِيُتِمَّ نِعْمَتَهُۥ عَلَيْكُمْ لَعَلَّكُمْ
تَشْكُرُونَ ﴿٦﴾

*"...Hapendi Mwenyezi Mungu kukutieni katika taabu, bali anataka kukutakaseni, na kutimiza neema yake juu yenu ili mpate kushukuru".* [5:6]

## Sharti za Swala

Sharti za swala kama tulivyojifunza katika vitabu vilivyotangulia ni hizi nne zifuatazo:

(i)Twahara
(ii)Sitara
(iii)Kuchunga wakati
(iv)Kusimama na kuelekea Qibla

## Twahara

Katika kitabu hiki tuiangalie tena twahara. Twahara ina maana ya utakaso wa mwili na nafsi. Kwa maana nyingine twahara haihusu usafi wa mwili tu bali pia inahusu usafi wa nafsi. Katika lugha ya

Qur'an, mtu mtwaharifu ni mtu aliyetakasika nafsi yake kutokana na maovu. Mwenyezi Mungu huwapenda watu wajitakasao:

إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلتَّوَّٰبِينَ وَيُحِبُّ ٱلْمُتَطَهِّرِينَ ﴿٢٢٢﴾

*"...Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanaotubu na kuwapenda wajitakasao".* [2:222]

Kwa mtazamo wa swala, mtu anayeweza kuswali ni yule aliyeepukana na aina zote za najisi na Hadath.

**Hadath**

Bila shaka tumeshafahamu aina zote za najisi na namna ya kuzitwaharisha. Lakini Hadath hatujaifahamu.

Tofauti na najisi, Hadath haihusiani na usafi wa mwili bali utakaso wa nafsi. Katika kuondoa Hadath tunaosha mwili kwa lengo la kupandikiza hisia za utakaso katika nafsi zetu.

Hadath ni hali ambayo anapokuwa nayo mtu hawezi kuswali. Kuna aina tatu za Hadathi:

(1)Hadath ndogo
(2)Hadath ya kati na kati
(3)Hadath kubwa

**Hadath ndogo** ni hali ya kutokuwa na udhu. Mtu asiyekuwa na udhu anahesabika kuwa ana hadath ndogo. Hadath hii huondoka kwa kutia udhu.

Yaliyoharamishwa kwa mwenye Hadath ndogo. Mwenye Hadath ndogo ameharamishwa kufanya yafuatayo:

(i)Kuswali
(ii)Kutufu kwenye Ka'abah

2.Hadath ya kati na kati (Janaba)

Mtu mwenye Hadath ya kati na kati ni mtu mwenye Janaba. Hadath hii huwapata watu wazima wanawake na wanaume waliofikia baleghe.

Yaliyoharamishwa kwa mtu mwenye Janaba ni:

(i) Kuswali
(ii) Kutufu
(iii) Kukaa Msikitini
(iv) Kushika msahafu
(v) Kusoma Qur'an

Mtu hutwaharika kutokana na Janaba kwa kuoga mwili mzima kwa maji safi kwa nia ya kuondoa janaba. Kama hapana maji au yuko safarini au mgonjwa asiyeweza kutumia maji atatayamamu kama tulivyojifunza katika kitabu cha nne.

3.Hadath kubwa

Hadath kubwa inawahusu watu wazima wanawake waliofikia baleghe. Mwanamke anakuwa na Hadath kubwa akiwa na hedhi (damu ya mwezi) au Nifasi (damu ya uzazi). Baada ya damu hizi kukatika anatakiwa ajitwaharishe kwa kuoga mwili mzima kwa maji safi kwa nia ya kuondoa "Hedh" au "Nifasi". Kama pana udhuru wa kutotumia maji atatayamamu kwa udogo safi.

Yaliyoharamishwa kwa mwenye Hadath kubwa ni:

(i) Kuswali
(ii) Kutufu
(iii) Kukaa Msikitini
(iv) Kuuchukua Msahafu
(v) Kusoma Qur'an
(vi) Kufunga
(vii) Kuingiliana kimwili na mumewe
(viii) Kuachwa iwapo ameolewa

**1.Swala ya mgonjwa**

Mgonjwa amepewa tahfifu zifuatazo:
(a)Mgonjwa ameruhusiwa kutayamamu iwapo maji yatamdhuru.

(b)Kama hajiwezi kabisa na hana mtu wa kumtawadhisha au kumtayamamisha mgonjwa huyo anaruhusiwa kutayamamu kwa ishara.

(c)Mgonjwa ameruhusiwa kuswali akiwa amekaa na kuelekea Qibla iwapo anaouwezo huo, vinginevyo anaruhusiwa kuswali akiwa ameelekea popote. Atarukuu na kusujudu iwapo ana uwezo, vinginevyo ataswali kwa ishara tu. Kama mgonjwa hawezi kukaa ataswali akiwa amelala kwa ubavu na huku ameelekea Qibla kama kuna uwezakano huo, vinginevyo atalala vile anavyoweza na kutekeleza vile anavyoweza kutekeleza vitendo vyote vya swala kwa ishara kwani Qur'an inatufahamisha.

يُرِيدُ ٱللَّهُ بِكُمُ ٱلْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ ٱلْعُسْرَ

*"…Mwenyezi Mungu anakutakieni yaliyo mepesi wala hakutakieni yaliyo mazito...".* [2:185]

لَا يُكَلِّفُ ٱللَّهُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا ۚ

*"Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi yoyote ila yaliyo sawa na uweza wake..."* [2:286]

(d)Mgonjwa pia amerusiwa kukusanya swala (angalia swala ya msafiri).

**2.Swala za Msafiri**

Msafiri amehafifishiwa usimamishaji wa swala kama ifuatavyo:
(a)Ameruhusiwa kutayamamu kwa kukosa maji yaliyo karibu au kushindwa kutumia maji akiwa ndani ya chombo. Pia anaruhusiwa

kutayamamu kwa kutumia sehemu yoyote ya chombo cha usafiri yenye vumbi vumbi lililotwahara.

(b)Ameruhusiwa kukusanya swala kwa kuwahisha au kuchelewesha. Swala hukusanywa pamoja katika pea zifuatazo: Adhuhuri + Alasiri na Magharibi + Isha. Subuhi aswali kwa wakati wake ule ule.

(c)Anaruhusiwa kufupisha (kupunguza) swala za rakaa nne na kuziswali kwa rakaa mbili. Swala zinazopunguzwa ni Adhuhuri, Alasiri na Isha.

**Namna ya kukusanya swala ya Safari kwa kuwahisha (Jamu-Taqadyim)**

Tujaalie kuwa unaswali swala ya adhuhuri na alasiri kwa kuwahisha katika wakati wa Adhuhuri. Utafanya ifuatavyo:

(i)Adhini na kukimu
(ii)Anza kuswali swala ya adhuhuri na kutoa salamu baada ya rakaa mbili
(iii)Simama ukimu, kisha uswali rakaa mbili za swala ya alasiri.

**Mamba yanayopaswa kufanyiwa maiti**

**1.Kumwosha maiti**

Kuosha maiti ya Muislamu ni faradhi. Maiti haiwezi kuswaliwa mpaka ioshwe kama vile Muislamu asivyoruhusiwa kuswali bila kuwa na twahara. Ila Mtume (s.a.w.) ameturuhusu kuwazika mashahidi na damu zao bila ya kuwaosha. Mashahidi ni wale waliokufa katika harakati za kuupigania Uislamu. Allah (s.w.) ametukataza kuwaita mashahidi wafu kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

وَلَا تَحْسَبَنَّ ٱلَّذِينَ قُتِلُوا۟ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ أَمْوَٰتًۢا ۚ
بَلْ أَحْيَآءٌ عِندَ رَبِّهِمْ يُرْزَقُونَ ﴿١٦٩﴾

*"Wala usiwadhani wale waliouliwa katika njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni wafu (maiti). Bali wahai, wanaruzukiwa kwa Mola wao.*

فَرِحِينَ بِمَآ ءَاتَىٰهُمُ ٱللَّهُ مِن فَضۡلِهِۦ وَيَسۡتَبۡشِرُونَ
بِٱلَّذِينَ لَمۡ يَلۡحَقُواْ بِهِم مِّنۡ خَلۡفِهِمۡ أَلَّا خَوۡفٌ
عَلَيۡهِمۡ وَلَا هُمۡ يَحۡزَنُونَ ﴿١٧٠﴾

*Wanafurahia aliyowapa Mwenyezi Mungu kwa fadhila zake, na wanawashangilia wale ambao hawajajiunga nao walio nyuma yao (waumini wenzao ambao bado hawajafa), ya kwamba haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika.*

يَسۡتَبۡشِرُونَ بِنِعۡمَةٖ مِّنَ ٱللَّهِ وَفَضۡلٖ وَأَنَّ ٱللَّهَ لَا يُضِيعُ
أَجۡرَ ٱلۡمُؤۡمِنِينَ ﴿١٧١﴾

*Wanashangilia neema na fadhila za Mwenyezi Mungu, na kwamba MwenyeziMungu hapotezi ujira wa wanaoamini".*
[3:169-171]

## Mazingatio kabla ya kuosha maiti

(1)Maiti ya kiume ioshwe na mwanamume na ya kike ioshwe na mwanamke. Ila Mume anaweza kumuosha mkewe na mke kumuosha mumewe.
(2)Ni mtu mmoja tu anayeosha mwingine au wengine watatoa msaada tu pale utakapohitajika.
(3)Muoshaji awe Muislamu.
(4)Mahali pa kuoshea pawe faragha - bafuni au uliojengwa maalumu kwa kazi hiyo au chumbani kama wengi wafanyavyo.
(5)Maiti aoshwe huku amefunikwa gubigubi na nguo nyepesi inayoruhusu maji kupenyeza kwa urahisi.

(6)Muoshaji asishike mwili wa maiti ila kwa glovu (gloves)
(7)Mwili wa maiti usiwe na kizuizi cha kufanya maji yapenyeze kwenye ngozi yake - misuko, rangi, na kadhalika vinavyozuia maji kupita vishughulikiwe.
(8)Pia najisi iondolewe kwenye mwili wa maiti kabla ya kuanza kuosha.
(9)Pawe na maji safi ya kutosha.

**Namna ya kumwosha maiti hatua kwa hatua**

Nguzo za kuosha maiti ni mbili tu, nia na kueneza maji mwili mzima. Hata hivyo si jambo jepesi kwa kuwa maiti hasogei kama alivyo mtu mzima. Isitoshe maiti inatisha kwa mtu asiye na mazoea ya kuosha. Kwa kurahisisha utamwosha maiti kwa kufuata hatua zifuatazo:

**1.**Maiti awekwe juu ya kitanda chenye tobo katikati la kupitishia uchafu utokao tumboni kama upo.

**2.**Lichimbwe shimo (ufuo) usawa wa tobo la kitanda, la kuhifadhi uchafu utakao toka kwa maiti. Iwapo hapana uwezekano wa kutengeneza ufuo, pawekwe kitu cha kukinga uchafu badala yake. Anaweza kuoshewa bafuni.

**3.**Maiti ifunikwe nguo moja kubwa, iliyo nyepesi kiasi cha kuruhusu maji kupita.

**4.**Maiti ikalishwe kitako juu ya hicho kitanda na makalio yake yawe sawa sawa na hilo tobo la kitanda na ufuo chini yake na iinamishwe kidogo nyuma.Kama ni maiti ya mtu mzima ni vyema msaidizi wa mwoshaji amuegemeze maiti kwa goti lake.

**5.**Mwoshaji apitishe mkono wake wa kushoto juu ya tumbo la maiti aliminyeminye kwa taratibu ili utoke uchafu uliomo humo ndani.

**6.**Amlaze chali na amminyeminye tumbo lake kama hapo awali.

**7.** Aikalishe tena kisha apitishe mkono wake wa kushoto chini, ukiwa umevalishwa kitambaa, au gloves asafishe tupu mbili huku anajiminimia maji kwa mkono wa kulia. Ikiwa, josho la awali halitakidhi haja, avue kitambaa kile na kukitupia kwenye ufuo na kujiviringisha kingine kisafi na kufanya kama mara ya kwanza mpaka patakate.

**8.** Muoshaji, baada ya hapo, azungurushe kitambaa kwenye kidole cha shahada cha mkono wa kushoto, akichovye majini, kisha amswakishe maiti vizuri meno ya juu na ya chini, kisha akitupe ufuoni.

**9**. Azungurushe kitambaa kingine kwenye kidole kidogo cha mkono wa kushoto, akichovye majini, kisha amsafishe kwacho tundu za pua, kisha akitupe ufuoni.

**10**. Achukue kijiti laini achokonoe kucha zake maiti, iwapo ni ndefu na chafu.

**11**. Akiwa pia amemkalisha, amtawadhishe maiti kwa kufuata utaratibu wa kawaida wa kutawadha. Lakini wakati wa kumwosha uso, amuinamishe mbele kidogo ili maji yasimwingie ndani.

**12.** Maiti akiwa katika hali hiyo hiyo ya kukaa, mwoshaji ataanza kumwosha kichwa huku akiwa amemuinamisha kwa mbele. Kama nywele ni nyingi zichanwe panapo uwezekano na zioshwe kwa sabuni. Kisha maji yamiminwe mpaka povu la sabuni liishe. Nywele na ndevu zichanwe vizuri na mwanamke mwenye nywele nyingi asukwe mikia. Nywele zitakazong'oka ziambatanishwe na sanda.

**13.** Baada ya kuoshwa kichwa, maiti alazwe kwa ubavu wa kushoto, kisha kuanza kumwosha ubavu wa kulia kwa kumiminia maji mbele na nyuma pamoja na kusugua kwa

sabuni. Kisha kumiminia maji mengi mpaka povu liishe.

**14.** Kisha maiti atalazwa kwa ubavu wa kulia na kuoshwa ubavu wa kushoto kama ilivyofanyika kwa ubavu wa kulia.

**15**. Baada ya makosho haya mawili - la maji na sabuni na la kuondoa sabuni, pawe na kosho la tatu la maji yaliyowekwa karafuu maiti na marashi kidogo. Karafuu maiti inasaidia kulegeza maungio na kufanya mwili wa maiti usitepete.

**16.** Baada ya makosho haya matatu, mwoshaji anyooshe viungo vya maiti na kumlaza sawasawa kama alivyolazwa mara baada ya kufa, kisha achukue nguo kavu na kumfuta maiti kama mtu anavyojifuta kwa taulo baada ya kukoga. Kisha maiti awekwe juu ya mkeka mkavu na afunikwe nguo kubwa kavu tayari kwa kupambwa na kuvalishwa sanda.

## Kumkafini Maiti

Kumkafini maiti au kumvalisha sanda ni Faradhi Kifaya. Nguo nzuri ya kutumia kwa ajili ya sanda ni nguo nyeupe ya pamba kama tunavyofahamishwa katika Hadithi ifuatayo:

> *Ibn Abbas amesimulia kuwa Mtume wa Allah (s.a.w) amesema: Vaeni nguo nyeupe, kwa sababu hilo ni vazi lenu lililo bora kuliko yote, na wakafinini maiti wenu nguo (nyeupe). (Abu Daud, Tirmidh na Ibn Majah).*

Pia ni vyema nguo hiyo isiwe ya gharama kubwa na nguo iliyotumika ni bora zaidi kama tunavyofahamishwa katika Hadith ifuatayo:

> *Ali (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Msigharamie sana nguo ya sanda, kwani inakwenda kuozeana (karibuni)". (Abu Daud).*

Hajj (mwenye kuhiji) akifa wakati wa Hija, akiwa bado kwenye "Ihram" (vazi rasmi la kuhijia - shuka mbili nyeupe zisizo shonwa),

Ihram yake huwa ndio sanda na kichwa chake kubakia wazi bila ya kufunikwa kama tunavyofahamishwa katika Hadithi:

> *Abdullah bin Abbas(r.a) amesimulia kuwa mtu mmoja alikuwa pamoja na Mtume (s.a.w) ngamia wake alimkanyaga, wakati akiwa anahiji mpaka akafa, Mtume wa Allah akasema:"Muosheni na maji na majani ya mkunazi na mumkafini kwa hayo mashuka yake mawili, msimpake manukato na msimfunike kichwa chake, na hakika siku ya Kiyama atafufuliwa akiitikia Labbaika. (Bukhari na Muslim).*

Ukubwa wa kitambaa cha sanda utategemea ukubwa wa maiti. Sanda ya mwanamume ina vipande vitatu vilivyo sawa sawa na sanda ya mwanamke ina vipande vitano.

## Sanda ya Mwanamume na Namna ya Kuivika

Sanda ya mwanamume ina vipande (majamvi) vitatu. Utaratibu wa kutayarisha sanda na kukafini ni kama ifuatavyo:

1. Weka kipande cha kwanza juu ya mkeka au jamvi, kisha cha pili na cha tatu na kila kipande kifukizwe ubani na kupakwa marashi. Vipande vyote hivi vitatu vishikizwe na uzi katikati.

2. Pasua kamba katika pembe mbili za jamvi la kwanza, kamba moja kwa ajili ya kufungia kichwani na nyingine ya kufungia miguuni. Kamba nyingine ya kumfungia maiti katikati itatolewa kwenye jammvi la pili. Kamba nyingine tatu za kufungia juu ya mkeka zitatoka kwenye jamvi la pili na la tatu.

3. Maiti italazwa juu ya vipande yote vitatu. Ichukuliwe pamba iwekwe manukato kisha iwekwe juu ya viungo vyote vya sijda - kipaji cha uso, viganja vya mikono, magotini na kwenye vidole vya miguu; pia pamba hiyo itumike kuzibia matundu yote mwilini - mdomo, pua, masikio na makalio.

4. Maiti itatatizwa na kipande cha kwanza mpaka kimuenee

- kwa kuanza kutatiza kunjo la kushoto, kisha kunjo la kulia lije juu. Vipande viwili viliyobaki vitatizwe kama hicho cha kwanza. Kisha zile kamba zitumike kufunga vitanzi kichwani, miguuni na tumboni ili sanda isije vuka na kumuacha maiti uchi. Katika hali hii maiti itakuwa tayari kwa kuswaliwa. Inaweza kuwekwa kwenye jeneza hivyo hivyo au inaweza kuzungushiwa mkeka kwanza ndio iwekwe kwenye jeneza.

## Sanda ya Mwanamke na Namna ya Kumvika

Sanda ya mwanamke kawaida ina vipande vitano. Vipande vikubwa viwili sawa na vile vya sanda ya mwanamume. Kipande cha tatu ni shuka au gagulo (*under skirt*), kipande cha nne ni kanzu na kipande cha tano ni ukaya au kipande cha nguo cha kufunikia kichwa na uso. Utaratibu wa kutayarisha sanda na kukafini ni kama ifuatavyo:

1. Vipande vikubwa viwili vitatandikwa kimoja hadi kingine kama inavyofanywa kwa sanda ya mwanamume.

2. Kikatwe kitambaa cha ukubwa wa shuka ya kawaida ya kufunga kiunoni. Kisha kipande hiki kiwekwe juu ya vipande viwili vikubwa katika sehemu ya chini atakapolazwa maiti ili shuka hii itatizwe kiunoni kama mtu anayefunga shuka ya kawaida.

3. Kisha ikatwe kanzu ambayo haishonwi vizuri, kwa kukunja kitambaa na kutoboa katikati ili iwe sehemu ya kuingiza kichwa wakati wa kuvalisha na kushikiza pembeni kwa uzi kufanya mfano wa kanzu kata mikono. Kanzu itatandikwa juu ya kipande kikubwa cha pili katika sehemu ya juu na sehemu ya chini itakuwa juu ya ile shuka (gagulo) baada ya kuwekwa manukato na kufukizwa ubani.

4. Kitambaa cha ukaya cha kutosha kufunika kichwa na uso kitaingizwa ndani ya shingo ya kanzu na kunyooshwa kwa juu. Baada ya hapo matayarisho ya sanda ya mwanamke yatakuwa yamekamilika.

5. Maiti ataanza kuvalishwa kanzu, kisha juu yake atafungwa shuka. Kisha atawekwa pamba yenye manukato viungo vyote vya sijda pamoja na sehemu zote za matundu kama inavyofanywa kwa maiti ya mwanamume. Baada ya hapo, maiti itatatizwa na vipande vikubwa viwili kimoja baada ya kingine, kila mara kunjo la kulia likiwa juu na itafungwa vile vile kwa kamba tatu - miguuni, tumboni na kichwani na kuwa tayari kuingizwa kwenye jeneza na kuswaliwa.

## Sanda ya Watoto

Sanda ya watoto wadogo, wa kike au wa kiume ni vipande vitatu tu kama ile ya wanaume wakubwa.

## Swala ya Jeneza

Muislamu anapofariki, Waislamu wanalazimika kumtendea haraka haraka mambo manne yafuatayo:

(1) Kumuosha mwili mzima kwa maji safi
(2) Kumvika sanda
(3) Kumswalia
(4) Kumzika

## Namna ya kumswalia maiti

Maiti huswaliwa baada ya kuoshwa na kuvikwa sanda. Swala ya maiti hukamilishwa kama ifuatavyo.

(1) Jeneza iwekwe mbele.
(2) Imamu asimame katikati ya mwili wa marehemu kama maiti ni ya kike, kama maiti ni ya kiume atasimama usawa wa mabega yake.
(3) Wanaomfuata Imamu wasimame kwenye mistari yenye idadi ya witri, 1,3,5,7 na kadhalika.
(4) Kuleta nia ya kuiswalia maiti iliyo mbele. Nia huletwa moyoni.(5)Kuleta takbira ya kuhirimia "Allahu Akbar"

(6)Kusoma Suratul Fatiha kimya kimya.
(7)Kuleta Takbira ya pili bila ya kuinua mikono.
(8)Kumswalia Mtume kama tufanyavyo katika swala.
(9)Kuleta takbira ya tatu
(10)Kumuombea maiti dua ifuatayo:

اللَّهُمَّ اغْفِرْ لَهُ وَارْحَمْهُ

*Allaahummaghfir lahuu warhamhu .*

*"Ewe! Allah, msamehe na umrehemu ".*

(11) Kuleta takbira ya nne.
(12) Kuwaombea dua Waislamu wote (Hii si lazima bali ni sunnah). Dua ifuatayo inaweza kuombwa hapa:

رَبَّنَا ٱغْفِرْ لَنَا وَلِإِخْوَٰنِنَا ٱلَّذِينَ سَبَقُونَا بِٱلْإِيمَـٰنِ وَلَا
تَجْعَلْ فِى قُلُوبِنَا غِلًّا لِّلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ رَبَّنَآ إِنَّكَ رَءُوفٌ
رَّحِيمٌ ﴿١٠﴾

*"Ewe Mola wetu! Tusamehe sisi na ndugu zetu waliotangulia (kufa) katika imani. Wala usijaalie katika nyoyo zetu uadui kuwafanyia Waislamu wenzetu. Mola wetu! Hakika wewe ni mpole sana, mwingi wa rehema".*
[59:10]

(14)Kutoa salamu kwa urefu

*Assalaam Alaykum Warahmatullah Wabarakatuh.*

**Kusindikiza Jeneza**

Baada ya maiti kuswaliwa jeneza litaongozwa kuelekea kaburini. Jeneza likipita tumeamrishwa kusimama hata kama hatuandamani nalo kama tunavyojifunza katika hadith ifuatayo:

> *Jabir (r.a.) amesimulia: Wakati jeneza lilipokuwa linapita, Mtume (s.a.w.) alisimama nasi pia tukasimama pamoja naye. Tukasema: "Ewe Mtume wa Allah! Hakika huyo ni Myahudi". Akasema: "Hakika kifo ni tishio. Kwa hiyo wakati wowote mtakapoona jeneza likipita simameni".* [Bukhari na Muslim]

Maandamano ya mazishi yawe kimya kimya. Hairuhusiwi hata kuleta tahalili wala kumswalia Mtume ili Waislamu wakumbuke tukio hilo tu la kifo wapate kuwaidhika.

**Kuzika**

Kuzika ni kitendo cha nne cha faradhi tunacholazimika kuifanyia maiti ya Muislamu. Mahali pa kuzikia ni kaburini. Kaburi linatakiwa liwe na kina cha kutosha kiasi kisichopungua meta mbili hivi.

Baada ya shimo kubwa la kaburi kukamilika, lichimbwe shimo ndogo karibu na upande wa Qibla, litakalokuwa na ukubwa wa kutosha kumlaza maiti kiubavu na kuweza kumfunikia ndani kwa ubao. Kishimo hiki kinaitwa "mwanandani". Maiti analazwa kiubavu kuelekea Qibla. Hivyo wakati wa kuchimba kaburi suala la Qibla ni lazima lizingatiwe.

**Kaburini maiti itazikwa kama ifuatavyo:**

1.Wateremke watu kaburini wenye idadi ya witri - watatu, watano n.k.

2.Jeneza liwekwe ukingoni mwa kaburi upande itakapokuwa miguu ya maiti.

3.Maiti atolewe kwa kutanguliza kichwa.

4.Maiti atakapoingizwa ndani ya kaburi, wapokeaji watamuweka magotini na kfungua kamba au vitanzi vyote vya miguuni, tumboni na kichwani. Pia watafunua shavu la kulia ili liguse ardhini wakati maiti atakapolazwa.

5.Maiti atalazwa kwa ubavu wa kulia ndani ya "mwanandani" na kuelekezwa Qibla. Wakati wa kumlaza ni sunnah kusema "Bismillahir Wabillah Wa-alaa millati rsuulillah".

6.Maiti apindwe kidogo miguuni na kichwani kiasi cha uso na miguu kugusa kuta za mwandani. Kifua, tumbo na sehemu nyingine za katikati zibinuliwe nyuma kidogo.

7.Pawekwe vipande vya udongo au mawe nyuma ya kichwa na miguu ili kuinua maiti isije binuka na kukaa visivyo. Kisha ni sunnah kusoma Qur'an Suratul Baqara ayaya 1-5 au aya ya 285-286.

8.Kisha maiti ifunikwe kwa ubao, na kama patakuwa na sehemu zilizowazi kiasi cha kuruhusu udongo kumfikia maiti zisiribwe kwa majani.

9.Kabla kaburi halijafunikwa, utupwe udongo kwa viganja vitatu na katika kila tupio ni sunnah kusema:
Mara ya kwanza:

مِنْهَا خَلَقْنَاكُمْ

*Katika hii ardhi tumekuumbeni"*

Mara ya pili:

وَفِيهَا نُعِيدُكُمْ

*Na humo tukakurudisheni"*

Mara ya tatu: وَمِنْهَا نُخْرِجُكُمْ تَارَةً أُخْرَىٰ

*Na kutoka humo utakutoeni mara nyingine".* [20:55]

10.Kaburi lijazwe mchanga mpaka lijae na kisha liinuliwe kidogo kiasi cha shubiri moja (sm 15). Ni vizuri kumimina maji juu ya kaburi ili kufanya udongo ushikamane na usipeperushwe na upepo.

Ipandwe miti mibichi inayochipua kwa upesi katika kona nne za kaburi ili kuweka alama. Ni haramu kujengea kaburi au kukaa juu yake au kuwasha taa juu yake au kulielekea wakati wa swala kama tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

*Jabir (r.a.) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amekataza kuyajengea makaburi au kuyajengea nyumba juu yake au kukaa juu yake.* [Muslim]

*Abu Marsad el-Ghafariyyi ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Msikae juu ya makaburi wala msiswali kwa kuyaelekea".* [Muslim]

11.Baada ya kumfukia maiti ni sunnah kumuombea dua ili Allah aithibitishe kauli yake katika kujibu maswali ya kaburini.

12.Baada ya kuzika ni sunnah kuwapa mikono wafiwa na kuwausia kusubiri.



## Zoezi la Nne

1. (a) Wanadamu wameumbwa na Allah (s.w) kwa lengo gani?
   (b) Ni nini hasa maana ya Ibada?

2. Taja lengo la ibada maalumu zifuatazo:
   (a) Shahada mbili
   (b) Kusimamisha swala
   (c) Kutoa Zakat
   (d) Kufunga katika Mwezi wa Ramadhani
   (e) Kuhiji

3. Eleza namna utakavyosimamisha swala wakati:
   (a) Mgonjwa
   (b) Msafiri

4. Taja mambo ya faradhi kufanyiwa maiti wa Kiislamu

5. Onesha tafauti iliyopo baina ya swala ya Ijumaa na Swala ya maiti

6. Eleza namna utakavyomuosha maiti hatua kwa hatua

Somo la 5 **Akhlaq**

# Sifa za muumini katika Qur'an

**Umuhmu wa kuigiza tabia ya Mtume (s.a.w)**

Muislamu aliyekamilika ni yule atayeigiza tabia ya Mtume (s.a.w.) katika kuendesha maisha yake ya kila siku. Bibi Aisha (r.a.), mke wa Mtume (s.a.w.) alipoulizwa na maswahaba aieleze tabia ya Mtume, aliwajibu kuwa tabia yake ni Qur'an. Kwa maana nyingine tabia na mwenendo wa Mtume Muhammad (s.a.w.) ulijengwa juu ya msingi wa Qur'an. Aliishi maisha yake yote kama alivyoelekezwa na Mola wake katika Qur'an.

Naye Allah (s.w.) amemsifu Mtume wake kwa tabia yake njema katika aya ifuatayo:

وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ ﴿٤﴾

*Na bila shaka una tabia njema kabisa.* [68:4]

Hivyo inatudhihirikia kwamba ili tuwe waumini hatunabudi kuishi kwa kufuata Qur'an na Sunnah ya Mtume (s.a.w.). Katika kitabu hiki tutarejea baadhi ya aya za Qur'an zinazotufahamisha moja kwa moja sifa za watu wema ambao wameitwa kwa jina la waumini, wacha Mungu, waja wa Rahmani, kundi la Allah, n.k.

1. **Suratul-Mu-uminun (23:1-11,57-61)**

قَدْ أَفْلَحَ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١﴾ الَّذِينَ هُمْ فِي صَلَاتِهِمْ
خَاشِعُونَ ﴿٢﴾ وَالَّذِينَ هُمْ عَنِ اللَّغْوِ مُعْرِضُونَ ﴿٣﴾

*Hakika wamefuzu Waislamu. Ambao katika Sala zao huwa ni wanyenyekevu. Na ambao hujiepusha na mambo ya upuuzi(23:1-3)*

وَٱلَّذِينَ هُمْ لِلزَّكَوٰةِ فَٰعِلُونَ ﴿٤﴾ وَٱلَّذِينَ هُمْ
لِفُرُوجِهِمْ حَٰفِظُونَ ﴿٥﴾ إِلَّا عَلَىٰٓ أَزْوَٰجِهِمْ أَوْ مَا
مَلَكَتْ أَيْمَٰنُهُمْ فَإِنَّهُمْ غَيْرُ مَلُومِينَ ﴿٦﴾

*Na ambao (nguzo ya) Zaka wanaitekeleza. Na ambao tupu zao wanazilinda. Isipokuwa kwa wake zao au kwa (wanawake) wale iliyowamiliki mikono yao ya kuume, (kulia) Basi hao ndio wasiolaumiwa.(23:4-6)*

فَمَنِ ٱبْتَغَىٰ وَرَآءَ ذَٰلِكَ فَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْعَادُونَ ﴿٧﴾
وَٱلَّذِينَ هُمْ لِأَمَٰنَٰتِهِمْ وَعَهْدِهِمْ رَٰعُونَ ﴿٨﴾

*(Lakini) anayetaka kinyume cha haya, basi hao ndio warukao mipaka (ya Mwenyezi Mungu).Na ambao amana zao na ahadi zao wanaziangalia, (wanazitekeleza). (23:7-8)*

وَٱلَّذِينَ هُمْ عَلَىٰ صَلَوَٰتِهِمْ يُحَافِظُونَ ﴿٩﴾ أُو۟لَٰٓئِكَ
هُمُ ٱلْوَٰرِثُونَ ﴿١٠﴾ ٱلَّذِينَ يَرِثُونَ ٱلْفِرْدَوْسَ هُمْ فِيهَا
خَٰلِدُونَ ﴿١١﴾

*Na ambao Sala zao wanazihifadhi.Hao ndio warithi. Ambao watarithi Pepo wakae humo milele. (23:9-11)*

إِنَّ ٱلَّذِينَ هُم مِّنْ خَشْيَةِ رَبِّهِم مُّشْفِقُونَ ﴿٥٧﴾ وَٱلَّذِينَ
هُم بِـَٔايَـٰتِ رَبِّهِمْ يُؤْمِنُونَ ﴿٥٨﴾ وَٱلَّذِينَ هُم بِرَبِّهِمْ لَا
يُشْرِكُونَ ﴿٥٩﴾

*Kwa hakika hao ambao kwa kumuogopa Mola wao wananyenyekea. Na hao ambao Aya za Mola wao wanaziamini. Na hao ambao Mola wao hawamshirikishi (23:57-59)*

وَٱلَّذِينَ يُؤْتُونَ مَآ ءَاتَوا۟ وَّقُلُوبُهُمْ وَجِلَةٌ أَنَّهُمْ
إِلَىٰ رَبِّهِمْ رَٰجِعُونَ ﴿٦٠﴾ أُو۟لَـٰٓئِكَ يُسَـٰرِعُونَ فِى
ٱلْخَيْرَٰتِ وَهُمْ لَهَا سَـٰبِقُونَ ﴿٦١﴾

*Na hao ambao wanatoa (Zaka na sad aka katika mali) waliyopewa, na 'hali nyoyo zao zinaogopa kwa kuwa watarejea kwa Mola wao Basi wote hao ndio wafanyao haraka katika mambo ya kheri na ndio wendao mbele katika hayo.*(23:60-61)

Aya hizi zinatufahamisha wazi kuwa waumini wa kweli watakaofuzu katika maisha yao ya hapa dunani na huko Akhera ni wale wenye sifa zifuatazo:
(1)Husimamisha swala kwa kuswali kwa unyenyekevu, na kuzihifadhi swala zao. Kuhifadhi swala kwa kuchunga sharti zote za swala na kutekeleza nguzo zote za swala kwa ukamilifu.

(2)Hujiepusha na laghwi. Laghwi ni mambo yote yanayopumbaza na kupoteza muda. Michezo yote ya kupumbaza, kama vile gololi, bao, karata, mpira, draft, n.k. ni laghwi.

(3)Watoao zakat na sadakat

(4)Hujihifadhi tupu zao kwa kujiepusha na zinaa.

(5)Kuchunga amana zao. Yaani huzichunga amama za watu na za Allah (s.w.) na kuzirejesha au kuzitumia inavyostahiki kulingana na maelekezo ya mwenyewe.

(6)Huchunga ahadi zao walizoahidiana na watu na zile walizomwahidi Allah (s.w.).

(7)Wafanyao haraka katika mambo ya kheri kwa kuzidisha unyenyekevu kwa Allah (s.w.) na kukumbushana mara kwa mara marejeo ya Akhera.

(8)Wanajiepusha na kumshirikisha Allah (s.w.).

Wenye kujipamba na sifa hizi Mola wao amewaahidi pepo ya daraja ya juu kabisa -Firdaus. Vile vile hapa duniani wataishi maisha ya raha na utulivu wa moyo.

## 2. Al-Furqaan (25:63-77)

وَعِبَادُ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلَّذِينَ يَمْشُونَ عَلَى ٱلْأَرْضِ
هَوْنًا وَإِذَا خَاطَبَهُمُ ٱلْجَٰهِلُونَ قَالُوا۟ سَلَٰمًا ﴿٦٣﴾

*Na waja wa Mwenyezi Mungu (anaowapenda ni wenye sifa hizi): Ni wale wanaokwenda (na kurejea) ulimwenguni kwa unyenyekevu na wajinga wakisema nao (maneno mabaya) huwajibu. (maneno ya) Salama. (25:63)*

وَٱلَّذِينَ يَبِيتُونَ لِرَبِّهِمْ سُجَّدًا وَقِيَٰمًا ﴿٦٤﴾ وَٱلَّذِينَ يَقُو
لُونَ رَبَّنَا ٱصْرِفْ عَنَّا عَذَابَ جَهَنَّمَ ۖ إِنَّ عَذَابَهَا كَانَ غَرَامًا

*Na wale wanaopitisha baadhi ya saa za usiku kwa ajili ya Mola wao kwa kusujudu na kusimama. Na wale wanaosema: "Mola wetu! Tuondolee adhabu ya Jahanamu, bila shaka adhabu yake ni yenye kuendelea. (25:64-65)*

إِنَّهَا سَاءَتْ مُسْتَقَرًّا وَمُقَامًا ﴿٦٦﴾

*Hakika hiyo (Jahanamu) ni kituo kibaya na mahali (pabaya kabisa) pa kukaa" (25:66)*

وَالَّذِينَ إِذَا أَنفَقُوا لَمْ يُسْرِفُوا وَلَمْ يَقْتُرُوا وَكَانَ بَيْنَ
ذَٰلِكَ قَوَامًا ﴿٦٧﴾

*Na wale ambao wanapotumia hawatumii kwa fujo wala hawafanyi ubahili bali wanakuwa katikati baina ya hayo. (25:67)*

وَالَّذِينَ لَا يَدْعُونَ مَعَ اللَّهِ إِلَٰهًا آخَرَ وَلَا يَقْتُلُونَ
النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ وَلَا يَزْنُونَ ۚ وَمَن يَفْعَلْ
ذَٰلِكَ يَلْقَ أَثَامًا ﴿٦٨﴾

*Na wale wasiomuomba mungu mwingine pamoja na Mwenyezi Mungu, wala hawaui nafsi aliyoharimisha Mwenyezi Mungu isipokuwa kwa haki wala hawazini, na atakayefanya hayo atapata madhara (papa hapa ulimwenguni kabla ya akhera). (25:68)*

يُضَاعَفْ لَهُ الْعَذَابُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَيَخْلُدْ فِيهِ مُهَانًا

*Na atazldishiwa adhabu siku ya Kiama na atakaa humo kwa kufedheheka (muda mrefu kabisa) milele. (25:69)*

إِلَّا مَن تَابَ وَءَامَنَ وَعَمِلَ عَمَلًا صَٰلِحًا فَأُوْلَٰٓئِكَ
يُبَدِّلُ ٱللَّهُ سَيِّـَٔاتِهِمْ حَسَنَٰتٍۗ وَكَانَ ٱللَّهُ غَفُورًا
رَّحِيمًا ﴿٧٠﴾

*Ila yule atakayetubia na kuamini na kufanya vitendo vizuri basi hao ndio Mwenyezi Mungu atawabadilishia maovu yao kuwa mema na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Miwingi wa kurehemu. (25:70)*

وَمَن تَابَ وَعَمِلَ صَٰلِحًا فَإِنَّهُۥ يَتُوبُ إِلَى ٱللَّهِ
مَتَابًا ﴿٧١﴾

*Na aliyetubia na kufanya wema, basi kwa hakika yeye anatubu kweli kweli kwa Mwenyezi Mungu. (25:71)*

وَٱلَّذِينَ لَا يَشْهَدُونَ ٱلزُّورَ وَإِذَا مَرُّواْ بِٱللَّغْوِ مَرُّواْ كِرَامًا
﴿٧٢﴾ وَٱلَّذِينَ إِذَا ذُكِّرُواْ بِـَٔايَٰتِ رَبِّهِمْ لَمْ يَخِرُّواْ
عَلَيْهَا صُمًّا وَعُمْيَانًا ﴿٧٣﴾

*Na wale ambao hawashuhudii shahada za uwongo, na wanapopita penye upuuzi hupita kwa hishima (yao).Na wale ambao wanapokumbushwa aya za Mola wao hawaziangukii kwa uziwi na upofu, (hawajifanyi viziwi nazo na vipofu). (25:72-73)*

وَٱلَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا هَبْ لَنَا مِنْ أَزْوَٰجِنَا وَذُرِّيَّٰتِنَا
قُرَّةَ أَعْيُنٍ وَٱجْعَلْنَا لِلْمُتَّقِينَ إِمَامًا ﴿٧٤﴾

*Na wale wanaosema: “Mola wetu! Tupe katika wake zetu na watoto wetu yaburudishayo macho (yetu) (nyoyo zetu), na Utujalie kuwa waongozi kwa wamchao (Mungu). (25:74)*

أُوْلَٰٓئِكَ يُجْزَوْنَ ٱلْغُرْفَةَ بِمَا صَبَرُواْ وَيُلَقَّوْنَ فِيهَا

تَحِيَّةً وَسَلَٰمًا ﴿٧٥﴾

*Hao ndio watakaolipwa ghorofa (za Peponi) kwa kuwa walisubiri na watakuta humo hishima na amani. (25:75)*

خَٰلِدِينَ فِيهَا ۚ حَسُنَتْ مُسْتَقَرًّا وَمُقَامًا ﴿٧٦﴾ قُلْ مَا

يَعْبَؤُاْ بِكُمْ رَبِّى لَوْلَا دُعَآؤُكُمْ ۖ فَقَدْ كَذَّبْتُمْ فَسَوْفَ

يَكُونُ لِزَامًا ﴿٧٧﴾

*Wakae humo mielele: kituo kizuri na mahali pazuri (kabisa) pa kukaa. Sema: “Mol a wangu asingekujalini kama si kule kuomba, (kumuabudu) kwenu,” Na nyinyi mumekwishakadhibisha basi (adhabu) itakuwa yenye kukushukieni tu”* (25:66-77)

Aya hizi zinatufahamiha kuwa waja wa Allah anaowapenda na aliowawia radhiyake na kuwaahidi malipo mema ya hapa duniani na huko akhera ni hawa wenye sifa zifuatazo:

(1) Wanaishi katika dunia hii kwa unyenyekevu. Yaani si watu wenye kibri kwa watu wala kwa Allah (s.w.). Hawawi na majivuno au kujikweza mbele ya wanadamu wenzao na mwenendo wao ni ule wa kufuata mwongozo wa Qur'an na Sunnah ya Mtume (s.a.w.).

(2) Wanaojiepusha na kuzozana au kubishana na watu. Yaani

inapotokea kutoelewana katika maongezi na watu, huyaakhirisha maongezi yale na kuagana kwa wema.

(3) Wanaamka usiku wa manane kuswali Tahajjud kwa ajili ya kutafuta radhi za Allah (s.w.).

(4) Mara kwa mara humuomba Allah (s.w.) awaepushe na adhabu ya Jahannamu. Hawaishii tu kuomba dua hii bali hujitahidi kwa jitihada zao zote kujiepusha na yale yote yatakayowapelekea kupata adhabu ya Allah (s.w.).

(5) Hawamshirikishi Allah (s.w.) na chochote katika dhati yake, sifa zake, ufalme wake na hukumu zake.

(6) Wanajiepusha na kuua nafsi yoyote ambayo haifanya kosa la kustahili kuuawa. Anayestahiki kuuawa kwa hukumu ya Qur'an ni pamoja na yule aliyeua mtu kwa makusudi, jambazi, anayepigana na Waislamu katika vita vya jihad.

(7) Wanaojiepusha na zinaa.

(8) Huleta toba ya kweli baada ya kuteleza na kwenda kinyume na Allah (s.w.) na Mtume wake. Toba ya kweli hupatikana kwa kufanya yafuatayo:

(a)Kujuta moyoni kwa kosa ulilolifanya na kuazimia kutolirudia tena.

(b)Kumuomba Allah (s.w.) msamaha kwa unyenyekevu.

(c)Kuwa na imani na yakini juu ya Allah (s.w.) na vipengele vyote vya nguzo za imani.

(d)Kuzidisha amali njema kama vile kuzidisha kutoa sadaqa na kuwafanyia watu wema, kuzidisha kuleta swala za sunnah na funga za sunnah.

(9) Hujiepusha na kutoa ushahidi wa uwongo. Muumini wa kweli atatoa ushahidi wa kweli hata kama ni dhidi ya nafsi yake mwenyewe au ya jamaa yake wa karibu sana. Wale wenye kusimamia ukweli bila ya kujali udugu au urafiki ndio watu wa kundi la Mwenyezi Mungu "Hizbu Allah".

(10) Hujiepusha na mambo ya lagh-wi (upuuzi) ambayo huwapotezea muda na kuwatoa katika lengo la kuumbwa kwao. Lengo la kuumbwa kwetu ni kumuabudu Allah (s.w.) kama inavyodhihirika katika Qur'an:

وَمَا خَلَقْتُ ٱلْجِنَّ وَٱلْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥٦﴾

*"Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu".* [51:56]

Kutokana na aya hii tunawajibika kumubudu Allah (s.w.) kwa muda wote wa saa 24 za siku. Tunaweza kumuabudu Allah (s.w.) kwa muda wote endapo tufafanya kila jambo letu kwa ajili ya kutafuta radhi yake kwa kufuata mwongozo wake na wa Mtume wake. Hatuna budi kumzingatia Allah (s.w.) na kuchunga mipaka yake kwa kila tunalolifanya.

(11) Wanapokumbushwa aya za Allah (s.w.) huzinyenyekea kwa kuzifuata ipasavyo.

(12) Wanajitahidi kulea familia yao katika maadili ya kumtii Allah (s.w.) na Mtume wake na kuomba msaada wa Allah (s.w.)

Malipo ya waumini wenye kujizatiti na kujipamba na vipengele hivi vya tabia njema ni ghorofa za peponi kama ilivyo ahidiwa katika aya 75 na 76 - (25:75-76).

## 3. Al-Ma'arij (70:19-35)

إِنَّ ٱلْإِنسَٰنَ خُلِقَ هَلُوعًا ﴿١٩﴾ إِذَا مَسَّهُ ٱلشَّرُّ جَزُوعًا

﴿٢٠﴾ وَإِذَا مَسَّهُ ٱلْخَيْرُ مَنُوعًا ﴿٢١﴾

*Kwa hakika binadamu ameumbwa hali ya kuwa mwenye papatiko. Inapomgusa shari huwa mwenye fazaa. Na inapomgusa kheri huwa anaizuilia. (70:19-21)*

إِلَّا ٱلْمُصَلِّينَ ﴿٢٢﴾ ٱلَّذِينَ هُمْ عَلَىٰ صَلَاتِهِمْ دَآئِمُونَ

﴿٢٣﴾ وَٱلَّذِينَ فِىٓ أَمْوَٰلِهِمْ حَقٌّ مَّعْلُومٌ ﴿٢٤﴾ لِّلسَّآئِلِ

وَٱلْمَحْرُومِ ﴿٢٥﴾

*Ila wanaosali; (hao hawana sifa mbaya hiyo). Ambao wanadumisha Sala zao. Na ambao katika mali zao iko sehemu maalumu. Kwa ajili ya aombaye na anayejizuilia kuomba (japo anahitaji).(70:22-25).*

وَٱلَّذِينَ يُصَدِّقُونَ بِيَوْمِ ٱلدِّينِ ﴿٢٦﴾ وَٱلَّذِينَ هُم مِّنْ

عَذَابِ رَبِّهِم مُّشْفِقُونَ ﴿٢٧﴾ إِنَّ عَذَابَ رَبِّهِمْ غَيْرُ

مَأْمُونٍ ﴿٢٨﴾

*Na ambao wanaisadikisha siku ya malipo. Na ambao wanaiogopa adhabu (itokayo) kwa Mola wao. Hakika adhabu ya Mola wao si yakusalimika nayo mtu (mbaya). (70:26-28)*

وَٱلَّذِينَ هُمْ لِفُرُوجِهِمْ حَٰفِظُونَ ﴿٢٩﴾

إِلَّا عَلَىٰٓ أَزۡوَٰجِهِمۡ أَوۡ مَا مَلَكَتۡ أَيۡمَٰنُهُمۡ فَإِنَّهُمۡ غَيۡرُ
مَلُومِينَ ﴿٣٠﴾

*Na ambao wanahifadhi tupu zao. Isipokuwa kwa wake zao au wale iliyowamiliki mikono yao ya kuume basi hao hawalaumiwi(70:29-30)*

فَمَنِ ٱبۡتَغَىٰ وَرَآءَ ذَٰلِكَ فَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡعَادُونَ ﴿٣١﴾

*Lakini wanaotaka kinyume cha haya basi hao ndio wanaoruka mipaka. (70:31)*

وَٱلَّذِينَ هُمۡ لِأَمَٰنَٰتِهِمۡ وَعَهۡدِهِمۡ رَٰعُونَ ﴿٣٢﴾
وَٱلَّذِينَ هُم بِشَهَٰدَٰتِهِمۡ قَآئِمُونَ ﴿٣٣﴾ وَٱلَّذِينَ هُمۡ
عَلَىٰ صَلَاتِهِمۡ يُحَافِظُونَ ﴿٣٤﴾

*Na ambao wanaangalia amana zao na ahadi zao (maagano yao). Na ambao ni imara katika ushahidi wao Na ambao wanazihifadhi Sala zao (70:32-24)*

أُوْلَٰٓئِكَ فِي جَنَّٰتٖ مُّكۡرَمُونَ ﴿٣٥﴾

*Hao ndio watakaokuwa katika Mabustani wakihishimiwa.(70:35)*

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa mwanadamu pamoja na maendeleo ya sayansi na teknolojia atakayofikia katika wakati wowote ule wa historia yake, hataweza kutulizana na kufarjiika, kukinai na kushukuru na kuishi kwa furaha na amani mpaka awe ni mwenye kujipamba na vipengele vya tabia njema vifuatavyo:

(1) Kusimamisha swala.
(2) Kutoa zakat na sadakat kuwapa wanaostahili.
(3) Kuwa na imani ya yakini juu ya siku ya mwisho. Hujitahidi kujiepusha na yale yote yanayomghadhibisha Allah (s.w.) kwa kuchelea adhabu yake kali isiyo na mfano wake:

فَيَوْمَئِذٍ لَّا يُعَذِّبُ عَذَابَهُۥٓ أَحَدٌ ﴿٢٥﴾

*"Basi siku hiyo hataadhibu yoyote namna ya kuadhibu kwake (Mwenyezi Mungu)".* [89:25]

(4) Kuhifadhi tupu kwa kujiepusha na zinaa na machafu mengine yanayoshabihiana na zinaa.
(5) Kutekeleza amana na ahadi.
(6) Kuwa imara katika kutoa ushahidi na kusimamia haki.

Watu wenye sifa hizi pamoja na kutulizana katika maisha ya hapa ulimwenguni, wanangojewa na malipo yaliyo bora zaidi huko Akhera ambayo ni pepo na heshima kubwa.

## 4. At-Tawba (9:71,111-112)

وَٱلْمُؤْمِنُونَ وَٱلْمُؤْمِنَٰتُ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَآءُ بَعْضٍ ۚ
يَأْمُرُونَ بِٱلْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ ٱلْمُنكَرِ وَيُقِيمُونَ
ٱلصَّلَوٰةَ وَيُؤْتُونَ ٱلزَّكَوٰةَ وَيُطِيعُونَ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥٓ ۚ
أُو۟لَٰٓئِكَ سَيَرْحَمُهُمُ ٱللَّهُ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٧١﴾

*Na wanaoamini wanaume na wanaoamini wanawake ni marafiki wao kwa wao. Huyaamrisha yaliyo mema na kuyakataza yaliyo mabaya na kusimamisha Sala na hutoa*

*Zaka na humtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu atawarehemu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima. (9:71)*

إِنَّ ٱللَّهَ ٱشْتَرَىٰ مِنَ ٱلْمُؤْمِنِينَ أَنفُسَهُمْ وَأَمْوَٰلَهُم
بِأَنَّ لَهُمُ ٱلْجَنَّةَ ۚ يُقَٰتِلُونَ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ فَيَقْتُلُونَ
وَيُقْتَلُونَ ۖ وَعْدًا عَلَيْهِ حَقًّا فِى ٱلتَّوْرَىٰةِ وَٱلْإِنجِيلِ
وَٱلْقُرْءَانِ ۚ وَمَنْ أَوْفَىٰ بِعَهْدِهِۦ مِنَ ٱللَّهِ ۚ فَٱسْتَبْشِرُوا۟
بِبَيْعِكُمُ ٱلَّذِى بَايَعْتُم بِهِۦ ۚ وَذَٰلِكَ هُوَ ٱلْفَوْزُ ٱلْعَظِيمُ

*Mwenyezi Mungu amenunua kwa Waislamu nafsi zao na mali zao (watoe nafsi zao na mali zao katika kupigania dini) Ili na yeye awape Pepo. Wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu wanaua na wanauawa. Hii ndiyo ahadi aliyojilazimisha (Mwenyezi Mungu) katika Taurati na Injili na Qurani. Na ni nani atekelezaye zaidi ahadi yake kuliko Mwenyezi Mungu? Basi furahini kwa biashara yenu mliyofanya naye (Mwenyezi Mungu). Na huko ndiko kufuzu kukubwa. (9:111)*

ٱلتَّٰٓئِبُونَ ٱلْعَٰبِدُونَ ٱلْحَٰمِدُونَ ٱلسَّٰٓئِحُونَ
ٱلرَّٰكِعُونَ ٱلسَّٰجِدُونَ ٱلْءَامِرُونَ بِٱلْمَعْرُوفِ وَٱلنَّاهُونَ
عَنِ ٱلْمُنكَرِ وَٱلْحَٰفِظُونَ لِحُدُودِ ٱللَّهِ ۗ وَبَشِّرِ ٱلْمُؤْمِنِينَ

*(Hao walioahidiwa kupata haya ni wale) wanaotubia (wakikosa) wanaofanya Ibada (kweli kweli) wanaomshukuru (Mwenyezi Mungu) wanaofunga wanaorukuu na kusujudu*

*(yaani wanaosali) wanaoamrisha yaliyo mema na wanaokataza yaliyo mabaya, na wanaohifadhi mipaka ya Mwenyezi Mungu (hawapindukii). Basi wape habari njema hao walioamini (hivi).* (9:112)

Katika aya hizi tunajifunza kuwa waumini wa kweli husifika na fisa zifuatazo:

(1) Hupendana na kuulinda udugu na urafiki baina yao. Kinyume chake hujiepusha kuwafanya Wayahudi, Wakristo na makafiri wengine kuwa marafiki zao wa ndani. Wanazingatia wito wa Allah (s.w.) ufuataao:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَتَّخِذُواْ ٱلْيَهُودَ وَٱلنَّصَٰرَىٰٓ
أَوْلِيَآءَ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَآءُ بَعْضٍ ۚ وَمَن يَتَوَلَّهُم مِّنكُمْ
فَإِنَّهُۥ مِنْهُمْ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ لَا يَهْدِى ٱلْقَوْمَ ٱلظَّٰلِمِينَ ﴿٥١﴾

*"Enyi mlioamini msiwafanye Mayahudi na Wakristo kuwa marafiki. Na miongoni mwenu atakayefanya urafiki huo nao, basi huyo atakuwa pamoja nao. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongozi (njia ya kheri) watu madhalimu".* [5:51]

Allah (s.w.) anasisitiza:

إِنَّمَا وَلِيُّكُمُ ٱللَّهُ وَرَسُولُهُۥ وَٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱلَّذِينَ
يُقِيمُونَ ٱلصَّلَوٰةَ وَيُؤْتُونَ ٱلزَّكَوٰةَ وَهُمْ رَٰكِعُونَ ﴿٥٥﴾

*"Rafiki yenu khasa (wa kumsafia nia) ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na walioamini ambao husimamisha swala na hutoa zaka na hali yakuwa wananyenyekea".* [5:55]

Allah (s.w.) anaendelea kutunasihi juu ya suala la kuunda urafiki na maadui:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَتَّخِذُواْ ٱلَّذِينَ ٱتَّخَذُواْ
دِينَكُمۡ هُزُوٗا وَلَعِبٗا مِّنَ ٱلَّذِينَ أُوتُواْ ٱلۡكِتَٰبَ مِن
قَبۡلِكُمۡ وَٱلۡكُفَّارَ أَوۡلِيَآءَۚ وَٱتَّقُواْ ٱللَّهَ إِن كُنتُم
مُّؤۡمِنِينَ ٥٧

" *"Enyi mlioamini! Msiwafanye marafiki wale walioifnyia mzaha na mchezo dini yenu miongoni mwa wale waliopewa kitabu kabla yenu (Mayahudi na Wakristo) na miongoni mwa makafiri wengne. Na mcheni Mwenyezi Mungu kama nyinyi ni wenye kuamini (kweli)"* [5:57]

(2) Huamrisha yaliyomema na kukataza yaliyo mabaya. Muislamu wa kweli hawezi kutulizana kwenye jamii ambayo haiwajibiki ipasavyo katika kutekeleza majukumu yao ya kijamii. Hali kadhalika muumini wa kweli hawezi kutulizana na kuyaaha maovu yaendelee kutendeka mbele yake.

(3) Husimamisha swala na kutoa zka.

(4) Humtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa kufuata yale yote aliyoamrishwa na kuacha yale yote aliyokatazwa.

(5) Huingia biashara na Allah (s.w.) kwa kutoa mali yake na nafsi yake (nguvu zake na roho yake) ili kuhakikisha kuwa dini ya Allah (s.w.) inasimama katika jamii.

(6) Hutubia wanapomkosea Allah (s.w.).

(7) Humuabudu Mola wao katika kila kipengele cha maisha kwa kuhifadhi mipaka ya Allah (s.w.) katika kila hatua ya maisha yao.

## 5. Ar-Raad (13:19-29)

أَفَمَن يَعْلَمُ أَنَّمَآ أُنزِلَ إِلَيْكَ مِن رَّبِّكَ ٱلْحَقُّ
كَمَنْ هُوَ أَعْمَىٰٓ ۚ إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُو۟لُوا۟ ٱلْأَلْبَٰبِ ﴿١٩﴾

*Je Anayejua ya kwamba yaliyoteremshwa kwako kutoka kwa Mola wako ni haki (akayafuata basi) ni kama aliye kipofu? Wenye akili ndio wanaozingatia. (13:19)*

ٱلَّذِينَ يُوفُونَ بِعَهْدِ ٱللَّهِ وَلَا يَنقُضُونَ ٱلْمِيثَٰقَ ﴿٢٠﴾
وَٱلَّذِينَ يَصِلُونَ مَآ أَمَرَ ٱللَّهُ بِهِۦٓ أَن يُوصَلَ وَيَخْشَوْنَ
رَبَّهُمْ وَيَخَافُونَ سُوٓءَ ٱلْحِسَابِ ﴿٢١﴾

*(Na ni hawa) Ambao wao hutimiza ahadi ya Mwenyezi Mungu wala hawavunji ahadi (za wanadamu wenzao) Na ambao huyaunga aliyoamuru Mwenyezi Mungu yaungwe na humuogopa Mola wao, na huiogopa hisabu mbaya (itakayowapata wabaya huko akhera kwa hivyo wakajitahidi kujiepusha na vitendo vyao hao wabaya). (13:20-21)*

وَٱلَّذِينَ صَبَرُوا۟ ٱبْتِغَآءَ وَجْهِ رَبِّهِمْ وَأَقَامُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ
وَأَنفَقُوا۟ مِمَّا رَزَقْنَٰهُمْ سِرًّا وَعَلَانِيَةً وَيَدْرَءُونَ
بِٱلْحَسَنَةِ ٱلسَّيِّئَةَ أُو۟لَٰٓئِكَ لَهُمْ عُقْبَى ٱلدَّارِ ﴿٢٢﴾

*Na ambao husubiri (wakastahmilia wenziwao) kwa kutaka radhi ya Mola wao na wakasimamisha Sala na wakatoa katika vile tulivyowapa (wakavitoa) kwa siri na dhahiri na wakayaondoa maovu kwa mema. Hao ndio watakaopata malipo (mema) ya nyumba (ya Akhera). (13:22)*

جَنَّٰتُ عَدْنٍ يَدْخُلُونَهَا وَمَن صَلَحَ مِنْ ءَابَآئِهِمْ وَأَزْوَٰجِهِمْ وَذُرِّيَّٰتِهِمْ ۖ وَٱلْمَلَٰٓئِكَةُ يَدْخُلُونَ عَلَيْهِم مِّن كُلِّ بَابٍ ﴿٢٣﴾

*Mabustani ya milele watayaingia wao (pamoja) na waliofanya wema miongoni mwa wazee wao na wake wao na kizazi chao. Na Malaika wanawaingilia katika kila milango. (13:23)*

سَلَٰمٌ عَلَيْكُم بِمَا صَبَرْتُمْ ۚ فَنِعْمَ عُقْبَى ٱلدَّارِ ﴿٢٤﴾

*(Wanawaambia): "Salamun Alaykumli (iwe amani juu yenu) kwa sababu mlisubiri (mlistahmili katika kufanya mema na kuacha mabaya na mkastahmiliana mkakaa vizuri na wenzenu) Basi ni mema yaliyoje matokeo ya nyumba (ya Akhera kwa wanaomcha Mungu). (13:24)*

وَٱلَّذِينَ يَنقُضُونَ عَهْدَ ٱللَّهِ مِنۢ بَعْدِ مِيثَٰقِهِۦ وَيَقْطَعُونَ مَآ أَمَرَ ٱللَّهُ بِهِۦٓ أَن يُوصَلَ وَيُفْسِدُونَ فِى ٱلْأَرْضِ ۙ أُو۟لَٰٓئِكَ لَهُمُ ٱللَّعْنَةُ وَلَهُمْ سُوٓءُ ٱلدَّارِ

*Na wale wanaovunja ahadi ya Mwenyezi Mungu (na za wanadamu wenzao) baada ya kuzifunga na wanakata aliyoamuru Mwenyezi Mungu yaungwe na wanafanya uhanribifu katika nchi; hao ndio watakaopata laana na watapata nyumba mbaya. (13:25)*

ٱللَّهُ يَبْسُطُ ٱلرِّزْقَ لِمَن يَشَآءُ وَيَقْدِرُ ۚ وَفَرِحُوا۟ بِٱلْحَيَوٰةِ

ٱلدُّنۡيَا وَمَا ٱلۡحَيَوٰةُ ٱلدُّنۡيَا فِي ٱلۡأٓخِرَةِ إِلَّا مَتَٰعٞ ﴿٢٦﴾

*Mwenyezi Mungu hukunjua riziki kwa amtakaye na huidhikisha (kwa amtakaye). Na wamefurahia maisha ya dunia (ya mambo mabaya kuliko Akhera). Na uhai wa dunia kwa mkabala wa Akhera si kitu ila ni starehe ndogo tu. (13:26)*

وَيَقُولُ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ لَوۡلَآ أُنزِلَ عَلَيۡهِ ءَايَةٞ مِّن رَّبِّهِۦۗ قُلۡ
إِنَّ ٱللَّهَ يُضِلُّ مَن يَشَآءُ وَيَهۡدِيٓ إِلَيۡهِ مَنۡ أَنَابَ ﴿٢٧﴾

*Na wanasema wale waliokufufu: Kwa nini hakuteremshiwa miujiza kutoka kwa Mola wake?" Sema: Hakika Mwenyezi Mungu humuachia apotee amtakaye (kwa kuwa hataki kuelekea kwake) na huwaongoza wanaoelekea kwake. (13:27)*

ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَتَطۡمَئِنُّ قُلُوبُهُم بِذِكۡرِ ٱللَّهِۗ أَلَا
بِذِكۡرِ ٱللَّهِ تَطۡمَئِنُّ ٱلۡقُلُوبُ ﴿٢٨﴾

*(Nao) ni wale walioamini na zikatulia nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Sikilizeni! Kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu nyoyo hutulia. (13:28)*

ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ طُوبَىٰ لَهُمۡ
وَحُسۡنُ مَـَٔابٖ ﴿٢٩﴾

*Wale walioamini na kufanya vitendo vizuri raha itakuwa yao, na marejeo mema"* (13:29)

Katika aya hizi tunajifunza kuwa wenye akili "*Ulul-albaabi*" mbele ya Allah (s.w.) ni waumini ambao pamoja na kumkumbuka

Allah (s.w.) katika kila kipengele cha maisha yao kwa kuhifadhi barabara mipaka yake (rejea 3:190-191), pia wana sifa zifuatazo:

(1) Hutimiza ahadi ya Mwenyezi Mungu wala hawavunji ahadi za wanadamu wenzao.

(2) Huyaunga aliyoamuru Mwenyezi Mungu yaungwe. Yaani huyafuata yale anayoyaridhia Allah (s.w.) na huyaacha yale yanayomghadhibisha.

(3) Humuogopa Mola wao na huiogopa hisabu mbaya itakayowapata wabaya huko akhera. Kwa hiyo wakajitahidi kujiepusha na vitendo vibaya.

(4) Husubiri kwa kutaka radhi ya Mola wao.

(5) Husimamisha swala.

(6) Hutoa katika vile Allah (s.w.) alivyowaruzuku kwa siri na dhahiri.

(7) Huondoa maovu kwa mema. Yaani mtu akikutendea uovu ukazidisha kumfanyia wema mpaka aone haya kuendelea kuutenda uovu. Pia ina maana kuwa baada ya muumini kung'amua kuwa amefanya makosa, hutubia upesi kwa Mola wake na kuzidisha kufanya mema.

(8) Hutulizana nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu.

Wenye sifa hizi ndio watakaopata malipo mema ya nyumba ya akhera.

## 6. As-Sajadah (32:15-17)

إِنَّمَا يُؤْمِنُ بِـَٔايَـٰتِنَا ٱلَّذِينَ إِذَا ذُكِّرُوا۟ بِهَا خَرُّوا۟ سُجَّدًا
وَسَبَّحُوا۟ بِحَمْدِ رَبِّهِمْ وَهُمْ لَا يَسْتَكْبِرُونَ ۩ ﴿١٥﴾

*Hakika wanaoziamini Aya Zetu ni wale tu ambao wanapokumbushwa kwazo huanguka kusujudu na humtukuza Mola wao kwa (kutaja) sifa Zake, nao hawatakabari. (32:15)*

تَتَجَافَىٰ جُنُوبُهُمْ عَنِ ٱلْمَضَاجِعِ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ
خَوْفًا وَطَمَعًا وَمِمَّا رَزَقْنَـٰهُمْ يُنفِقُونَ ﴿١٦﴾

*Huinuka mbavu zao kutoka vitandani wakati wa usiku ili kumuabudu Mola wao kwa kuogopa Moto na kutaraji Pepo na hutoa (Zaka na sadaka) katika yale tuliyowapa. (32:16)*

فَلَا تَعْلَمُ نَفْسٌ مَّآ أُخْفِىَ لَهُم مِّن قُرَّةِ أَعْيُنٍ جَزَآءًۢ بِمَا
كَانُوا۟ يَعْمَلُونَ ﴿١٧﴾

*Nafsi yoyote haijui waliyofichiwa katika hayo yanayofurahisha macho (huko Peponi): ni malipo ya yale waliyokuwa wakiyafanya.* (32:17)

Tunajifunza katika aya hizi kuwa waumini wa kweli ni wale pia wenye sifa zifuatazo:

(1) Wanapokumbushwa kwa aya za Qur'an huzinyenyekea kwa kuzifuata inavyostahiki na humkumbuka Mola wao na kumtukuza inavyostahiki.

(2) Huamka usiku wa manane kuswali Tahajjud kwa ajili ya kutafuta radhi za Allah kwa matarajio ya kupata pepo na kuepukana na moto wa Jahannam.

(3) Hutoa katika yale Alla (s.w.) aliyowaruzuku.

Wenye kujipambana na sifa hizi wana malipo makubwa huko akhera.

**7. Al-Ahzab (33:35-36)**

إِنَّ ٱلۡمُسۡلِمِينَ وَٱلۡمُسۡلِمَٰتِ وَٱلۡمُؤۡمِنِينَ وَٱلۡمُؤۡمِنَٰتِ
وَٱلۡقَٰنِتِينَ وَٱلۡقَٰنِتَٰتِ وَٱلصَّٰدِقِينَ وَٱلصَّٰدِقَٰتِ
وَٱلصَّٰبِرِينَ وَٱلصَّٰبِرَٰتِ وَٱلۡخَٰشِعِينَ
وَٱلۡخَٰشِعَٰتِ وَٱلۡمُتَصَدِّقِينَ وَٱلۡمُتَصَدِّقَٰتِ
وَٱلصَّٰٓئِمِينَ وَٱلصَّٰٓئِمَٰتِ وَٱلۡحَٰفِظِينَ فُرُوجَهُمۡ
وَٱلۡحَٰفِظَٰتِ وَٱلذَّٰكِرِينَ ٱللَّهَ كَثِيرٗا وَٱلذَّٰكِرَٰتِ أَعَدَّ
ٱللَّهُ لَهُم مَّغۡفِرَةٗ وَأَجۡرًا عَظِيمٗا ٣٥

*Bila shaka wanaume wenye kufuata vizuri nguzo za Uislamu, na wanawake wanaozifuata vizuri nguzo za Uislamu, na wanaume wanaoamini vizuri nguzo za Imani, na wanawake wanoamini vizuri nguzo za Imani, na wanaume wanaotii na wanawake wanaotii na wanaume wasemao kweli, na wanawake wasemao kweli na wanaume wanaosubiri, na*

*wanawake wanaosubiri, na wanaume wanaonyenyekea na wanawake wanaonyenyekea na wanaume wanaotoa (Zaka na) sadaka, na wanawake wanaotoa (Zaka na) sadaka na wanaume wanaofunga na wanawake wanaofunga na wanaume wanojihifadhi tupu zao na wanawake wanojihifadhi, na wanaume wanaomtaja Mungu kwa wingi na wanawake wanaomtaja Mwenyezi Mungu (kwa wingi), Mwenyezi Mungu amewaandalia msamaha na ujira mkubwa. (33:35)*

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى ٱللَّهُ وَرَسُولُهُۥٓ أَمْرًا أَن يَكُونَ لَهُمُ ٱلْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ ۗ وَمَن يَعْصِ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَٰلًا مُّبِينًا ﴿٣٦﴾

*Haiwi kwa mwanamume aliyeamini wala kwa mwanamke aliyeamini, Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wanapokata shauri, wawe na hiari katika shauri lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, hakika amepotea upotofu (upotevu) ulio wazi (kabisa)* (33:36)

Aya hizi pia zinatufahamisha kuwa waumini wa kweli watakaostahiki kupata pepo ya Allah (s.w.) ni wale:

(1) Wanaoamini kwa vitendo nguzo zote za imani.
(2) Wanaosimamisha kwa ukamilifu nguzo zote za Kiislamu.
(3) Wasemao kweli.
(4) Wanaohifadhi tupu zao.
(5) Wanao mnyenyekea na kumtaja Mwenyezi Mungu kwa wingi.
(6) Wanaomtii Allah (s.w.) na Mtume wake kwa kufuata maamrisho yote na kuacha makatazo yote.

## 8. Ash-Shuura (42:36-43)

فَمَآ أُوتِيتُم مِّن شَيْءٍ فَمَتَٰعُ ٱلْحَيَوٰةِ ٱلدُّنْيَا ۖ وَمَا عِندَ
ٱللَّهِ خَيْرٌ وَأَبْقَىٰ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ
يَتَوَكَّلُونَ ﴿٣٦﴾

*Basi vyote hivi mlivyopewa ni starehe ya maisha ya dunia tu, lakini ktlichoko kwa Mwenyezi Mungu ni bora na cha kudumu (milele). Watakistahiki wale walioamini na wakawa wanamtegemea Mola wao. (42:36)*

وَٱلَّذِينَ يَجْتَنِبُونَ كَبَٰٓئِرَ ٱلْإِثْمِ وَٱلْفَوَٰحِشَ
وَإِذَا مَا غَضِبُوا۟ هُمْ يَغْفِرُونَ ﴿٣٧﴾

*Na wale wanaojiepusha na madhambi makubwa na mambo mabaya, na wale ambao wanapokasirika husamehe. (42:37).*

وَٱلَّذِينَ ٱسْتَجَابُوا۟ لِرَبِّهِمْ وَأَقَامُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ وَأَمْرُهُمْ
شُورَىٰ بَيْنَهُمْ وَمِمَّا رَزَقْنَٰهُمْ يُنفِقُونَ ﴿٣٨﴾

*Na wale waliomuitikia Mola wao (kwa katika amri Zake) na wakasimamisha Sala, na wanashauriana katika mambo yao na wanatoa katika yale tuliyowaruzuku. (42:38)*

وَٱلَّذِينَ إِذَآ أَصَابَهُمُ ٱلْبَغْىُ هُمْ يَنتَصِرُونَ ﴿٣٩﴾

*Na wale ambao jeuri inapowafikia huzitetea nafsi zao. (42:39).*

وَجَزَٰٓؤُا۟ سَيِّئَةٍ سَيِّئَةٌ مِّثْلُهَا ۖ فَمَنْ عَفَا وَأَصْلَحَ فَأَجْرُهُۥ

عَلَى ٱللَّهِ ۚ إِنَّهُۥ لَا يُحِبُّ ٱلظَّٰلِمِينَ ﴿٤٠﴾

*Na malipo ya ubaya ni ubaya ulio sawa na (ubaya) huo; lakini anayesamehe na kusuluhisha ugomvi; ujira wake uko kwa Mwenyezi Mungu; bila shaka Yeye hawapendi madhalimu. (42:40)*

وَلَمَنِ ٱنتَصَرَ بَعْدَ ظُلْمِهِۦ فَأُو۟لَٰٓئِكَ مَا عَلَيْهِم مِّن سَبِيلٍ

*Na wale wanaolipiza kisasi baada ya kudhulumiwa, hao hakuna njia ya kulaumiwa. (42:41)*

إِنَّمَا ٱلسَّبِيلُ عَلَى ٱلَّذِينَ يَظْلِمُونَ ٱلنَّاسَ وَيَبْغُونَ فِى

ٱلْأَرْضِ بِغَيْرِ ٱلْحَقِّ ۚ أُو۟لَٰٓئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٤٢﴾

*Bali lawama iko juu ya wale wanaodhulumu watu na wakawafanyia jeuri katika ardhi pasipo haki; hao ndio watakaopata adhabu iumizayo. (42:41)*

وَلَمَن صَبَرَ وَغَفَرَ إِنَّ ذَٰلِكَ لَمِنْ عَزْمِ ٱلْأُمُورِ ﴿٤٣﴾

*Na anayesubiri na kusamehe (atalipwa wema wake). Bila shaka hili ni katika mambo makubwa ya kuazimiwa kufanywa (na kila Muislamu)*(42:43)

Katika aya hizi pia tunajifunza kuwa miongoni mwa sifa za waumini watakaostahiki kupata starehe za kudumu za huko akhera ni:

(1) Wenye yakini juu ya Mwenyezi Mungu na kumtegemea yeye tu basi.

(2) Wenye kujiepusha na madhambi makubwa na mambo mabaya.

(3) Wenye kusamehe wanapokasirika. Yaani hawachukui uamuzi wa hasira. Huvuta subira mpaka hasira ziwaishie ndio wachukue uamuzi mara nyingi husamehe.

(4) Wenye kumuitikia Allah kwa kufuata kila aliloamrisha na kuacha kila alilolikataza.

(5) Wenye kusimamisha swala.

(6) Wenye kutoa katika yale Allah (s.w.) aliyowaruzuku.

(7) Wenye kushauriana katika mambo yao ili waweze kuyatekeleza kwa ushirikiano na kwa ufanisi.

(8) Wenye kudai haki zao wanapodhulumiwa. Yaani wenye kusimama kidete kupambana na madhalimu.

## 9. Al-Fat-h (48:29)

مُّحَمَّدٌ رَّسُولُ ٱللَّهِۚ وَٱلَّذِينَ مَعَهُۥٓ أَشِدَّآءُ عَلَى ٱلۡكُفَّارِ
رُحَمَآءُ بَيۡنَهُمۡۖ تَرَىٰهُمۡ رُكَّعٗا سُجَّدٗا يَبۡتَغُونَ فَضۡلٗا
مِّنَ ٱللَّهِ وَرِضۡوَٰنٗاۖ سِيمَاهُمۡ فِي وُجُوهِهِم مِّنۡ أَثَرِ
ٱلسُّجُودِۚ ذَٰلِكَ مَثَلُهُمۡ فِي ٱلتَّوۡرَىٰةِۚ وَمَثَلُهُمۡ فِي ٱلۡإِنجِيلِ
كَزَرۡعٍ أَخۡرَجَ شَطۡـَٔهُۥ فَـَٔازَرَهُۥ فَٱسۡتَغۡلَظَ فَٱسۡتَوَىٰ عَلَىٰ
سُوقِهِۦ يُعۡجِبُ ٱلزُّرَّاعَ لِيَغِيظَ بِهِمُ ٱلۡكُفَّارَۗ وَعَدَ ٱللَّهُ

ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّٰلِحَٰتِ مِنْهُم مَّغْفِرَةً وَأَجْرًا

عَظِيمًۢا ﴿٢٩﴾

*Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na walio pamoja naye ni wenye nyoyo thabiti mbele ya makafiri na wenye kuhurumiana wao kwa wao. Utawaona wakiinama kwa kurukuu na kusujudu (pamoja), wakitafuta fadhila za Mwenyezi Mungu na radhi (yake). Alama zao zi katika nyuso zao kwa taathira, (athari) ya kusujudu. Huu ndio mfano wao katika Taurati. Na mfano wao katika Injili (umetajwa hivi): Kuwa (wao) ni kama mmea uliotoa matawi yake' kisha (matawi hayo) yakautia nguvu ukawa mnene ukasimama sawasawa juu ya kigogo chake ukawafurahisha walioupanda ili awakasirishe makafiri kwa ajili yao. Mwenyezi Mungu amewaahidi walioamini na kutenda mema katika wao msamaha na ujira mkubwa.*
(48:29)

Aya hii inatufunza kuwa tumuigize Mtume na wale walioamini pamoja naye katika kuusimamisha Uislamu katikajamii. Waislamu wa kweli hupendana, huhurumiana na hushikamana pamoja katika kuusimamisha na kuuhami Uislamu. Huwa wagumu kwa makafiri maadamu wanaupiga Uislamu vita hata wakiwa ni baba zao au watoto wao au jamaa zao wengine wa karibu. Waislamu wa kweli hawamchelei yeyote katika kusimamisha haki.

## 10. Al-Hujurat (49:15)

إِنَّمَا ٱلْمُؤْمِنُونَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ بِٱللَّهِ وَرَسُولِهِۦ ثُمَّ لَمْ

يَرْتَابُوا۟ وَجَٰهَدُوا۟ بِأَمْوَٰلِهِمْ وَأَنفُسِهِمْ فِى

سَبِيلِ ٱللَّهِ ۚ أُو۟لَـٰٓئِكَ هُمُ ٱلصَّـٰدِقُونَ ﴿١٥﴾

*Wenye kuamini kweli kweli ni wale waliomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake kisha wakawa si wenye shaka na wakaipigania dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zao na nafsi zao, Hao ndio wenye kuamini kweli,* (49:15)

Pia rejea sifa za waumini wa kweli zilizoorodheshwa katika Al-Anfal (8:2-4) na Al-Hujurat (49:15). Hizi zmefafanuliwa vizuri katika sura ya atu ya kitabu hiki.



## Zoezi la Tano

1. (a) Kwa maelezo mafupi kabisa, tabia ya Mtume (s.a.w) ni.__________

(b) Tabia na Mwenendo wa Muislamu vimejwa katika misingi mikuu miwili:__________________ na ___________________________

2. Bainisha sifa za waumini wa kweli zinazopatikana katika sura zifuatazo:
   (a) Al Mu-uminun (23:1-11,57-61)
   (b)Al-Furqaan (25:63-77)
   (c) Al-Ma'arij (70:19-35)
   (d) At tawba (9:71,111-112)
   (e) Ar-Raad (13:19-29)
   (f) As-Sajadah (32:15-17)
   (g) Al-Ahzab (33:35-36)
   (h) Ash-Shuura (42:36-43)
   (i) Al-Fat-h (48:29)
   (j) Al-Hujurat (49:15)

3. Taja na kueleza kwa kifupi manufaa anayopata
   (a) mtu kwa kujipamba na tabia njema
   (b) na Jamii anamoishi mtu huyo

# Uislamu Baada ya Makhalifa

Baada ya kutawafu Mtume (s.a.w) migogoro mingi ilianza kujitokeza ndani ya dola ya Kiislamu. Walizuka watu waliojitangazia Utume, walitokea watu waliokataa baadhi ya nguzo za Uislamu kama vile kutoa Zakkah. Hata hivyo migogoro hii iliweza kudhibitiwa na Makhalifa waliochukua nafasi za kuiongoza dola.

Migogoro iliendelea kuongezeka kadiri muda ulivyopita mpaka ikapelekea kuuawa kwa Khalifa wa tatu Uthman bin Affan. Uongozi wa Khalifa Ali ulishuhudia mapigano ya Waislamu wenyewe kwa wenyewe kwa kipindi chote cha takriban miaka minane aliyoongoza dola. Hatimaye Khalifa Alli bin Abu Twalib naye aliuliwa katika mlolongo huo wa matatizo ya kutokuelewana miongoni mwa Waislamu.

## DOLA YA BANU UMMAYA

Zao la migogoro ya wakati wa Khalifa Ali ambaye aliuliwa katika sakata hizo ilikuwa ni maongozi ya Kiislamu kuachwa na Waislamu kuingia katika utawala wa kifalme. Mu'awiya mtoto wa Abu Sufiani ndiye aliasisi utawala huu. Mpaka hivi leo baadhi ya nchi za Kiarabu ufalme huu unaendelea. Katika utawala huu dini ilitenganishwa na siasa jambo ambalo ni msiba mkubwa kwa Waislamu.

Katika kuendesha dola kila aliyeacha uongozi aliurithisha kwa mwanae. Kwa mwenendo huu yafautayo yalitokea:

- Utaratibu wa kuchagua viongozi kutokana na sifa zao ulivunjwa.
- Taasisi ya shura ilivunjwa.

- Raia walipokonywa uhuru wa kutoa mawazo na kuwakosoa viongozi.
- Baitul-Mal (Hazina ya Dola) ikafanywa ni mali binafsi ya nyumba ya mfalme.
- Tabia za kijahili za majivuno ya kikabila na nasaba zikaibuka.
- Kujengwa kwa makasri ya kifahari kama makazi ya wafalme.
- Dini ilitenganishwa na siasa, Mashekhe waadilifu walitenganishwa na kundi la watawala.

Pamoja na hali hii walijitokeza baadhi ya viongozi ambao walikuwa wachamungu sana na waliokuwa na ghera ya kuona watu wakiishi Kiislamu.

**Miongoni mwao ni kama Umar bin Abdul-Aziz.**

Alipotwaa madaraka akimrithi Suleiman bin Abdul-Mulik alifanya mageuzi makubwa kuelekea katika Uislamu kama ifuatavyo:

- Aliyafanya maisha yake kuwa rahisi zaidi.
- Aliwaondoa wagavana wote waliokuwa katili.
- Alirejesha hadhi ya Baitul Mali. Hivyo fedha ya umma ilikusanywa na kutumiwa kwa uadilifu.
- Alichunga sana matumizi kutoka Baitul Mali kwa yeye mwenyewe na alikuwa mkali kufuatilia maafisa waliofuja mali ya umma.
- Aliamuru na kusimamia marekebisho ya mizani.
- Aliwagawia raia ardhi iliyotengwa na tawala za kabla yake kwa ajili ya wakubwa.
- Alifanya kazi ya kuwajenga watu kimaadili kwa kusimamia kikamilifu suala la kuamrisha mema na kukataza mabaya.
- Alisimamia kuvunjwa kwa mila za kijahili kama vile mishikamano ya kikabila na kiukoo badala ya kushikamana kwa ajili ya Allah.
- Kiuchumi aliisimamia nguzo ya zaka na ukusanyaji wa kodi mbali mbali.

- Hata katika vita Umar bin Abdul-Aziz aliwataka askari wake kujiegemeza kwa Allah (s.w) hivyo wasifanye ufisadi katika kushambulia.

Kwa uadilifu na utendaji wake mzuri katika kuendesha serikali, Umar alifananishwa na Abubakar na aliitwa khalifa wa tano wa Dola ya Kiislamu.

Hata hivyo kiongozi huyo muadilifu alitawala kwa kipindi cha miaka mwiwili na miezi mitano akafariki dunia. Msururu wa utawala wa kifalme ulifuatia na utawala wa Banu Umayya uliendelea kumomonyoka kutokana na uasi mbali mbali ndani ya dola na hatimaye kuporomoka kabisa wakati wa utawala wa Marwan II.

Machafuko yaliyotokea wakati wa utawala wa Marwan II, miji mbali mbali ilitaka kujitenga na utawala wa Banu Umayya. Machafuko haya yaliudhoofisha kabisa utawala huu.

Hali hii ilitoa mwanya kwa watu wa ukoo wa Abbas kujiimarisha na kisha kutangaza uasi dhidi ya utawala wa banu Umayya. Abu Muslim akitumia propaganda zenye kugusa hisia za watu kwa wito wa Ahlul Bayt alifanikiwa kupata watu wengi waliomuunga mkono. Aliendesha mapambano na kumshinda gavana wa Iraq. Abul Abbas kuwa khalifa. Baada ya kuchaguliwa Abul Abbas alijipa jina la As safah. Na huo ukawa ndio mwanzo wa utawala wa ukoo wa Abbas na mwisho wa utawala wa Banu Umayya.

Utawala wa banu Umayah ilikuwa lazima uanguke kwa sababu kuu zifuatazo:-

- Wengi wa viongozi waliochukua ufalme au ukhalifa walikuwa waovu. Maisha ya anasa na ufahari yaliwaghururi wakawa hawawajibiki kwa yeyote.
- Waliyaacha mafundisho ya Qur-an na hivyo misuguano na chuki kati ya nasaba, na nasaba; koo na koo; uliibuka. Msingi wa usawa ulivunjika na chuki za kikabila zikatawala.

Matokeo yake ni uadui, machafuko na kujitenga kwa baadhi ya majimbo kutoka

- Kuota mizizi kwa imani ya ushia.

- Kuibuka kwa ukoo wa al-Abbas ibn Muttalib uliodai kuwa na haki ya kutawala kwa; vile wanatokana na ukoo wa Banu-Hashim ulioheshimika sana.

## UTAWALA WA BANU ABBAS

Baada ya kuanguka utawala wa Umayya, ukoo wa Abbas ulichukua nafasi. Walirithi karibu maovu yote yaliyokuwa yakifanywa wakati wa utawala wa Umayyah. Serikali iliendeshwa kidiketa, mali ya umma iliendelea kufujwa na maadili mema yalikuwa mbali na utawala. Mauaji makubwa ya watu wa ukoo wa Muawiyya yaliyofanywa na Abul Abbas ni moja katika mifano mibaya ya kutajwa ya viongozi wa wakati wa banu Abbas.

Hata hivyo walipatikana ndani ya utawala huu msururu viongozi wema waliofanya mengi ya kupigiwa mfano. Abu Jaafar al-Mansur ni wa kwanza kati yao. Alikuwa mcha-Mungu na muadilifu. Alianzisha na kuendeleza taasisi mbali mbali za taaluma kama vile Fasihi, historia, madawa na utabibu, astronomia na sanaa. Aliimarisha kilimo na biashara. Alisikiliza na kujali shida za raia. Alipanua mipaka ya dola ya Kiislamu, na aliwashinda kijeshi. Warumi na wakawa wanalipa kodi. (Dinari 90,000 kwa mwaka). Alitumia muda wake mwingi kuangalia shughuli za serikali na muda mfupi sanaa kwa familia.

Mwingine katika viongozi walioonyesha ucha-Mungu na uadilifu wa hali ya juu ni Harunal-Rashid (170-194) AH. Pamoja na kufanya kama yale aliyoyafanya Abu Jaafar al-Mansur; Harun Rashid hakuweza kulala ndani, muda mwingi akizunguka kujua

miongoni mwa raia wake yupi mwenye shida na alifanya jitihada ya kuitatua.

Miongoni mwa mambo yaliyofanywa katika kipindi hiki cha banu Abbas ni upanuzi wa taaluma za aina mbali mbali. Jambo hili liliifanya dola ya Kiislamu kuwa na umaarufu wa hali ya juu ikilinganishwa na dola zinginezo. Maulamaa wa Kiislamu walizama katika uandishi na utafiti katika nyanja mbali mbali ambazo zimekuwa ndiyo msingi wa maendeleo ya teknolojia ya sasa.

## MAIMAMU WANNE WA FIQ-HI

Pamoja na uongozi mbaya uliokuwepo katika dola ya Kiislamu, watu wengi walikamatana na Uislamu. Viongozi wa dini waliheshimiwa sana na waumini wao. Kimsingi viongozi wa dini walitiiwa zaidi na raia wengi.

Waumini hawa walihitajia kupata ufumbuzi wa Kiislamu kwa matatizo mbali mbali yaliyowasibu. Kutokana na kupanuka kwa dola ya Kiislamu iliyoshika Bara zima la Asia, Kaskazini na Magharibi mwa Afrika, Ulaya nchi za Mediterania (Uhispania) n.k ilikuwa ni muhimu Uislamu utoe fat-wa mbali mbali juu ya mambo ya kijamii vinginevyo zingeibuka sheria na kanuni tofauti na Uislamu wenyewe. Awali jitihada zilifanywa kutoa fatwa juu ya masuala kulingana na Qur-an na Sunnah. Hiki kilijulikana kama kipindi cha "Tabiina"; ambapo maimamu;

- Nuiman ibn Thabit Abu Hanifa.
- Abu Abdullah Malik Ibn Anas.
- Muhammad ibn Idris al-Shafii na
- Ahmad ibn Hambal.

Walitumia uhai wao kutoa ufafanuzi, rai na fat'wa juu ya sheria mbli mbali za Kiislamu. Walitoa mchango mkubwa sana katika sheria ya Kiislamu na walikubaliana katika mambo yote ya

msingi (Usul). Na hawakufarakana kwa tofauti za maoni zilizojitokeza katika mambo madogo madogo.

Kamwe Maimamu hawa hawakuanzisha madhehebu jambo ambalo limetawala katika baadhi ya waumini wa sasa. Suala la madhehebu manne ndani ya Sunni wal-Jamaa ni zao la fikra za watu wa sasa na wala hao (Maimamu wanne) wanaoitakidiwa kuyaanzisha hawakuyajua.

## Ukusanyaji wa Hadith

Sambamba na utoaji wa Fatwa ulifanyika ukusanyaji wa Hadith katika kipindi kinachojulikana kama 'Attabii – Tabiina". Wakusanyaji maarufu wa hadith walikitumia muda wao mwingi kukusanya, kuchambua na kuzigawa katika makundi na kuzitia katika vitabu. Kwa juhudi zao hizo leo hii tuna vitabu sita mashahuri vya hadith sahihi vinavyojulikana kwa jina "Sahihi Sita". Vitabu hivi ni:

(1) Sahihi ul-Bukhari ya Imamu Bukhari.
(2) Sahihi Muslim ya Imamu Muslim.
(3) Jamii at-Tirmidh ya Imamu Tirmidh.
(4) Sunan – Abu Daud ya Abu Daud.
(5) Sunan – An Nasaai – ya Abu Abdur-Rahman bin Anasai.
(6) Sunan ibn Majah ya Muhammad bin Muhammad bin Yazid ibn Majah.

## UPINZANI WA WAKRISTO DHIDI YA DOLA YA KIISLAMU

Tokea kusimamishwa kwa dola ya Kiislamu Wakristo kama ilivyokuwa kwa imani zingine walikuwa na uhuru kamili wa kufuata imani yao, walikuwa na fursa za kujiendeleza kielimu na kiuchumi kama raia wengine. Yote hayo haya kuondoa chuki yao dhidi ya waislamu na Uislamu.

Wakristo waliendesha vita mara kadhaa dhidi ya Waislamu. Vita hivi vinafahamika kama vita vya msalaba. Viliitwa hivyo kwa vile pamoja na sababu za maslahi binafsi ya wapiganaji lakini

sababu kuu ilikuwa ni chuki ya wakristo dhidi ya Uislamu na waislamu.

Katika vita hivi sehemu nyingi zilizovamiwa, Waislamu waliuwawa makumi ya maelfu bila huruma. Kadhalika uharibifu wa mali na uchomaji wa vitabu aina mbali mbali ulifanywa na wavamizi hawa. Pamoja na uharibifu huu, viongozi mashuhuri wa kiislamu waliotoa upinzani mkali na hata kuweza kukomboa baadhi ya maeneo yaliyotekwa na wakristo hawakulipiza kisasi kwa lolote.

Huo ulikuwa ushambuliaji wa Uislamu na Waislamu kwa silaha na ana kwa ana. Hivi sasa uislamu unapigwa vita kifikra. Ni kawaida hivi sasa kusikia maneno kama vile Waislamu wenye siasa kali, magaidi, Wahab, Mujahidina, Al-Kaida n.k. Majina haya yanatumiwa kutoa taswira potofu ya Uislamu na Waislamu katika vichwa vya walimwengu. Kwa majina haya wasiojua Uislamu ni vigumu kuunasibisha na zuri lolote. Hali hii imeupaka Uislamu motope kwa kiwango kikubwa sana.

## HARAKATI ZA KUHUISHA UISLAMU SEHEMU MBALI MBALI DUNIANI

Kila wakati katika maeneo mbali mbali duniani pamekuwa pakiinukia watu walisimama kidete kutaka kuurejesha Uislamu katika hadhi yake. Hadhi ya Uislamu ni kuwa juu ya dini zingine hata kama makafiri na washirikina watachukia.

Muhammad bin Abdul-Wahab (1703) alianzisha harakati za kuhuisha sunna ya Mtume (s.a.w) na tawhiid ndani ya Saudia ya sasa. Muhammad Ahmad (1844) (MAHD wa Sudan) aliendesha harakati za kutaka Uislamu usimame ndani ya Sudani ya sasa. Vuguvugu la Uislamu leo hii ndani ya Sudani ni zao la harakati zake.

Bader-U-Zaman Said Nurs: Alipambana kutaka utawala dhalimu wa Mustafa Kamal Ataturk wa Uturuki uondoke na badala yake nchi iendeshwe kwa taratibu za Uislamu.

Wengine ni Jamal-Udin Afghani (1839) wa Afghanistan, Hassan al-Banna (1906) wa Ikhwani Muslimina ya Misri) na Sayyid Abul A 'ala Maududi (1903) (wa Jamaatil Islamiya ya Pakistani. Wote hawa harakati zao ni mifano ya kuigwa na Waislamu wa leo wenye ghera ya kuona Uislamu unasimama katika jamii. Historia fupi za baadhi yao ni kama ifuatavyo:

## MUHAMMAD BIN ABDULWAHAB (SAUDIA)

Sheikh Muhammad bin Abdul-Wahab alizaliwa mwaka 1703; huko Najd. Kipindi alichozaliwa usingeweza kumtofautisha Muislamu na asiye Muislamu kwani mafunzo ya Uislamu yalikuwa yametupwa kwa kiwango kikubwa.

Baada ya kuchukua mafunzo ya Uislamu kwa Walimu wengi wa miji mbali mbali Sheikh Muhammad alirejea Najd na kuanza kazi ya kufundisha Uislamu. Kwa elimu na kazi yake hii alipata umaarufu mkubwa sana.

Sheikh Muhammad bin Abdulwahab alianzisha na kuendesha harakati za kuhuisha Sunnah ya Mtume kwa vitendo.

Kwa umaarufu wake watawala wa Najd hawakuridhika kukaa naye walipanga njama za kumuua, baadaye wakaamua kumfukuza nchini kwa kisingizio kuwa anavunja sheria zao. Baada ya kwenda huku na huko akitafuta makazi na mahali pa kazi alipokelewa na Amir Muhammad bin Saud ambaye alikubali kushirikiana naye katika programu yake ya kuhuisha Sunnah ya Mtume.

Maadui wa program ya Sheikh Abdulwahab walimzulia propaganda kuwa amezua dini mpya ambapo anawaita makafiri Waislamu wote wasiokubaliana na dini yake. Kwa mbinu hii maadui

hawa waliweza kumgombanisha Sheikh huyu na Waislamu ambao ndio aliowalenga. Sumu hii imeenea hadi sasa japo wengine hawajui chimbuko lake, utawasikia Waislamu wenye kupendelea kusoma maulidi wakiwaita wasiofanya hivyo mawahabi n.k.

## MAHD WA SUDAN

Muhammad Ahmad alizaliwa 1844 katika jimbo la Dongola. Wakati huo Sudan ilikuwa chini ya Muingereza; yaani ilitawaliwa na Uingereza kupitia kwa vibaraka wa Misri. Elimu yake ya Uislamu aliipatia nchini Sudan. Alijiunga na Twarika iliyojulikana kwa jina la Sumaniya ya Sheikh Muhammad Sharif Nurdini. Sifa za uchamungu wake zilienea kwa haraka hata akafanywa kiongozi aliyechini ya mkuu wa Tarika.

Alipofariki Sheikh Muhammad Sharif; Muhammad Ahmad alichukua uongozi wa tarika. Sheikh huyu alijitangaza kuwa yeye ndiye Imam Mahd aliyeahidiwa mnamo mwaka 1881. Hili lilitokana na maneno ya watu wengi waliokuwa wakimtaja kwa muda mrefu kuwa aweza kuwa Imam aliyeahidiwa. Sheikh Muhammad Ahmad aliendesha harakati za kusimamisha dola ya Kiislamu ndani ya Sudani. Athari ya harakati zake imeonekana hadi hivi leo kwa Wasudani kuwa mstari wa mbele katika kuuhami Uislamu.

## HASSAN AL-BANNA (Ikhwani Muslimin ya Misri)

Ikhwani Muslimiin ni kikundi cha harakati chenye lengo la kuusimamisha Uislamu, ambapo sheria za Allah (s.w) zitatawala katika kila kipengele cha maisha ya Muislamu kijamii na kwa mtu binafsi. Kikundi hiki kimeenea karibu nchi zote za Kiarabu. Kiliasisiwa na shahid Hassan Al-Banna aliyezaliwa mwaka 1906. Baada ya kuhitimu stashahad ya elimu 1927 Sheikh Hassan alipangiwa kusomesha huko Ismailiya. Kulingana na nchi ya Misri ilivyokuwa imegubikwa na wimbi kubwa la Umagharibi ambapo tabia ya kina mama kwenda nusu uchi ilishamiri, nadharia ya kutenganisha

dini na siasa ilitawala, kuenea vishawishi mbali mbali vya zinaa n.k; Hassan alBanna alijiona ana jukumu zito la kuuelimisha umma na kuuhuisha upya Uislamu. Jitihada zake zikaanza kwa kuunda kikundi cha wenye kuamrisha mema na kukataza maovu.

Jamii ilielekea katika maangamizi kwa kasi kubwa baada ya kuutupa mfumo wa maisha ya Kiislamu. Kwa kuifikiria sana jamii hii Hassan al-Banna aligundua kuwa:-

- Mahubiri ya Masheikh misikitini hayatoshi.
- Masheikh wengi walishindwa kabisa kupambana na waliojiita Secularists na Modernists.
- Masheikh waliowengi walinunuliwa kirahisi na serikali.

Yote haya yalimsukuma kuanzisha kikundi cha harakati za Kiislamu mnamo 1928 akakiita "Ikhwani Muslimiin".

Waislamu walielimishwa juu ya Uislamu wao kwa njia ya mihadhara, darasa mawaidha misikitini na kwa maandishi.

Miaka mine baadaye serikali ilishaanza kulijia juu kundi hili la harakati. Mwaka 1948 kundi hili lilipigwa marufuku na serikali na tarehe 12/2/1949 Hassan Al-Banna aliuliwa kwa kupigwa risasi. Kuuwawa kwake hakukusitisha shughuli za kundi. Hassan ismail Hudhaybi alishika hatamu na harakati zikaendelea. Mwaka 1954 serikali ilifanya hujuma kubwa kwani iliingia kwenye zoezi la kamata kamata na kuwaingiza kizuizini wanaharakati waliowengi. Baadhi yao walihukumiwa kunyongwa.

Harakati za Ikhwani zilihuishwa tena 1958 ikiungana na jumuiya ya wanawake iliyoongozwa na Zainab al-Ghazali. Ilikuwa ni Abdul Fattah Ismail na Zainab Al-Ghazali walioanzisha tena harakati hizo.

Wakati Ikhwani wakiendelea na kuweka programu za kuhuisha Uislamu serikali ya Jamal Abdul Nasser ilikuwa ikiandaa mauaji

ya siri kwa wanaharakati walioonekana vinara ambao ni Sayyid Qutub, AbdulFattah na Zainab al-Ghazali.

Mnamo 1965 majasusi wa serikali ya Nasser wakisaidiana na C.I.A. na K.G.B. waliandaa orodha ya majina ya wanaharakati waliotakiwa kutiwa mbaroni. Pamoja na Sayyid Qutub walikamatwa wanaharakati na watu wengine kwa maelfu. Sayyid Qutub alihukumiwa kunyongwa na wengine walihukumiwa kuanzia vifungo vya miaka sita hadi maisha.

**SAYYID ABDUL ALA MAUDUUDI (Jamaat Islamiya Pakistan)**

Jamaat Islamiya ni miongoni mwa harakati ambazo mpaka leo zipo na zinaendelea kufanya kazi ya kuhuisha Uislamu. Muasisi wa harakati za jamaati Islamiya ni Sayyid Abdul Ala Mauduudi ambaye alizaliwa mnamo 25 Septemba 1903 huko Aurangabad – Pakistani.

Harakati za Jamaat Islamiya zilikita zaidi katika kutoa elimu sahihi ya Uislamu kwa kupitia semina, Itqaf, kambi na machapisho. Kadhalika Jamaati-Islamiya imejenga na kuendesha taasisi za elimu katika viwango mbali mbali.

Kadhalika Jamaat Islamiya ilianza kutoa huduma mbali mbali za kijamii mara baada ya uchumi wake kuimarika. Huduma hizi ni kama vile afya, kusaidia wenye njaa, kusaidia waliofikwa na maafa mbali mbali.

Utaratibu mzuri wa mafunzo, utendaji na ushirikishwaji wa wanajumuiya katika shughuli mbali mbali uliiwezesha Jamaat Islamiya kuendelea na kazi za harakati hata pale viongozi wakuu wanapowekwa ndani au kufariki.

Maulana Mauduudi alijiuzulu uongozi wa harakati mwaka 1972 kutokana na udhaifu wa afya na alifariki dunia mwaka 1979.

## KUIBUKA KWA TWARIKA MBALIMBALI

Baada ya kuanguka dola ya Kiislamu na hivyo mafunzo sahihi ya Kiislamu kukosa usimamizi wa kuyachunga, na wakati huo huo kusimama kwa maovu mbali mbali ambayo wakati mwingine yalipata baraka za watawala, waliibuka watu waliobuni njia nyepesi walizodhani kuwa zingewatakasa na kuwakurubisha zaidi kwa Allah (s.w).

Baada ya kuona dunia imejaa uovu watu walijiundia njia zitakazowatakasa wao binafsi huku wakijitenga na uovu huo wakiwaacha watu kuendelea nao. Watu hawa walikuja julikana kama sufii au watawa.

Sufii ni mtu anayejitolea maisha yake kwa kujitenga na maisha ya kila siku ili amdhukuru Allah (s.w), hajishughulishi na mambo yote ya kidunia. Usufii huwafanya watu wakatenganisha maisha ya dunia na dini na hivyo hawajihusishi na lolote la kisiasa, elimu iliyoitwa ya kidunia, utoaji huduma mbali mbali za kijamii, uamrishaji wa mema na kutataza mabaya n.k. Kwa bahati mbaya Masufii hujikweza katika utakaso mpaka wakajipa utakatifu na hivyo wengine wakaitwa Mawalii wenye baraka na karama.

### Ni upi mtizamo wa Uislamu juu ya Usufii?

Mwenendo huu wa kiitikadi haukubaliki katika Uislamu kwani mwanaadamu kaletwa hapa duniani kuwa Khalifa wa Allah (s.w). Autawale na kuuendesha ulimwengu kwa kufuata muongozo wake. Awe mwakilishi wa Allah (s.w). Itikadi ya Usufii unashajihisha unyonyaji, uzembe na mwishowe uwezekano wa kumshirikisha Allah (s.w).

## KUINGIA UISLAMU AFRIKA YA MASHARIKI

Historia anaonyesha kuwa Uislamu uliingia Afrika ya Mashariki kunako karne ya nane. Kundi la Waomani ambalo lilizuru pwani ya Afrika Mashariki na kutua katika miji ya Lamu na Mombasa ndilo la mwanzo kuingiza Uislamu hapa. Pamoja na Uislamu ilipatikana Lugha ya Kiswahili pamoja na utamaduni wa Kiswahili ambao unanasibishwa na Uislamu.

## KUINGIA KWA UKRISTO NA HARAKATI ZA KANISA

Ukristo ni dini iliyoingia Tanzania katika karne ya kumi na nane miaka elfu moja baada ya kuingia Uislamu. Wamisionari waliokuja Afrika ndio waliofungamana na kuja kwa ukoloni. Kwa mwendo huu historia ya Kanisa katika Afrika ni ile ya kushirikiana na kuwa watiifu kwa serikali ya kikoloni.

Wajerumani walipofika Tanganyika waliwakuta waislamu wanafahamu kuandika, kusoma na kuhesabu. Walitumia herufi za Kiarabu. Kwa ajili hii waliwaajiri Waislamu kama walimu, wakalimani na makarani serikalini. Wamisionari na wakoloni kwa ujumla ustaarabu huu wa waislamu waliuonea wivu.

La muhimu ni kuwa kutokana na jinsi Uislamu ulivyokuwa umepiga hatua katika Afrika ya Mashariki wazungu waliandalia nguvu kubwa katika kuudhoofisha.

Mbinu za kuwaghilibu waislamu ziliasisiwa na miongoni mwazo zipo mpaka leo. Mfano mwanzo Muislamu hakuwa tayari kuwa na mashirikiano ya ndani na Mkristo.

Wakristo waliwaghilibu Waislamu na kujifanya wanao urafiki nao na kwamba waishi pamoja kundugu. Matokeo ya hili ni kuwepo mwingiliano wa hata Waislamu kuoana na wakristo ambapo mwishowe waislamu huingizwa katika ukristo.

Pili wakristo wlijipenyeza vijijini na kuanzisha huduma mbali mbali za kijamii kama vile shule, hospitali, vitengo vya malezi ya watoto yatima na kusaidia wasio na uwezo, lakini lengo kuu ni kupenyeza mawazo ya ukristo katika vichwa vya wanaowapa huduma. Hili linafanyika hata sasa na wengi wa watu wazima kwa watoto wamebatizwa kwa njia hii.

Kadhalika Sivalon anaeleza kuhusu kuandaliwa rasmi kwa wakatekista ili wakaishi vijijini. Na hili likapelekea wakristo hawa kuchukua nafasi muhimu za uongozi wa chama na serikali katika vijiji kata na tarafa.

Wengi wamekuwa ndio viongozi wa vijiji, makatibu wa kata na makatibu wa tarafa, nafasi ambazo ni muhimu katika kutoa miongozo ya awali ya uendeshaji wa nchi. Viongozi hawa ama kwa makusudi au kwa msukumo wa imani yao kwa kanisa huamua mengi kinyume na maslahi ya Uislamu na yakapita kama maamuzi ya kiserikali.

Waarabu wa mwanzo waliokuja kutafuta biashara, walifungua shule za Qur-an ambamo waliwafundisha watu kusoma na kuandika kwa kutumia herufi na namba za Kiarabu. Wajerumani walipoingia nchini kwa nia ya kuifanya nchi yetu koloni lao, waliwatumia wasomi hawa kama wasaidizi katika shughuli mbali mbali za kiofisi. Hali hii iliwafanya wakristo ambao kimsingi hawakujua kusoma kuanza kuilalamikia serikali kuwa inawapendelea Waislamu.

Wakoloni wa Kijerumani wakishirikiana na mashirika ya kikristo (Wamisionari) yaliyokuwepo walianza mkakati wa kuwasomesha wakristo kwa nia ya wao pia waweze kuajirika serikalini. Mikakati ya makusudi ya kuwakwaza waislamu kielimu ilifanywa ikiwemo:-

- Kuacha kutumika kwa herufi za Kiarabu.
- Waislamu kutopewa mgao wa pesa kwa ajili ya uanzishaji na uendeshaji wa shule.

- Pale fedha zilipotolewa waislamu walipewa kidogo sana ikilinganishwa na wakristo.
- Serikali ya kikoloni kuja na sera ya kutoruhusu kufunguliwa wa shule ya msingi kipindi Waislamu walipoamua kuanzisha shule zao.
- Pale waislamu walipofungua shule zao kulazimishwa wafundishe Qur-an tu, vinginevyo watashtakiwa.

Unyanyaswaji huu uliwafanya waislamu kuchukua hatua za makusudi kujinasua. Hivyo utakuta katika safu ya kupigania uhuru wa Tanganyika waislamu wa wengi sana kimsingi twaweza kusema kuwa ndiyo nguvu pekee iliyoongeza chache katika kupigania uhuru.

Ni waislamu walioanzisha vikundi mbali mbali kwa ajili ya kujikomboa ikiwemo vyama vya Wafanyakazi k.m.f. TAA ambayo baadaye ilibadili sana zake na kuwa chama cha siasa (TANU) vile vile waliunda al-Jamiatul-Islamiyya fiy TANGANYIKA na African Association. Kadhalika kuliundwa vyama kama vile AMNUT.

Wakati Waislamu wanahangaika kuutafuta mustakibali wa nchi dhidi ya manyanyaso ya wakoloni Wakristo waliokuwa wamependelewa na wakoloni hawahujishughulisha katika harakati za kudai uhuru. Kwa bahati mbaya sana hawakujua yaliyoko vifuani mwa wakristo. Walijipa mwiko ambao ni kinyume na Uislamu "**kutochanganya dini na siasa**". Walifanya hivyo kwa kuhofu wakakatisha tamaa wakristo wachache waliokuwa nao kiharakati. Hata hivyo yaonyesha wakristo hawa walikuwa na malengo zaidi ya yale waliyoyapanga pamoja wenzao Waislamu. Tukirejea maneno yaliyomo katika taarifa iliyoandikwa na Padri William Collins wa Maryknoll Fathers kuhusu mwalimu Nyerere anasema:

> *"... Shirika la Maryknoll limeona kuwa msaada wowote linaoweza kuwa patia viongozi wa kikatoliki utakuwa ni kulisaidia kanisa. Huyu (Mwl. Nyerere) ni mkatoliki mzuri, mtu mwenye msimamo wa busara katika kuwaelekeza watu wake..."*

Hivyo kwa namna moja au nyingine walijua kuwa uhuru utakapokuwa umepatikana na lazima walifanye kanisa na wakristo kuwa na nafasi nzuri katika nchi. Na hivi ndivyo ilivyo sasa.

Pamoja na kuwa awali kanisa na waumini wake walijiweka mbali na siasa za kuutafuta uhuru wa nchi baada ya uhuru kupatikana lilijitokeza kama mshauri wa karibu wa serikali. Si hilo tu bali pia likajipa wajibu na haki ya kuikosoa serikali mpya. Hivi ndivyo kanisa lilivyojijengea ushawishi ndani ya serikali ya Tanganyika na hatimaye Tanzania.

Palianza kuonekana misuguano ya wazi wazi baina ya watendaji wa serikali na viongozi wa Waislamu. Ilivyo kulikuwa na njama ya siri ya kuwatoa Waislamu ndani ya TANU na serikali pia. Ahadi za huko nyuma za kuondoa upogo wa mgawanyo wa madaraka serikalini, nafasi za elimu baina ya Waislamu na Wakristo zilisahaulika. Badala yake mwaka 1963 mwezi Machi 11, kamati kuu ya TANU ilipiga kura kuvunja kamati ya wajumbe kumi na moja ya Baraza la Wazee wa TANU. Katika hii ilivunjwa kwa kisingizio kuwa imekuwa kero kwani inachanganya dini na siasa. Nongwa ni kwa vile walikuwa wakiushauri uongozi wa chama uangalie upogo (imbalance) uliyopo katika mambo mengi ya kinchi ukizingatia makundi mawili Waislamu na wakristo.

Jumuiya za Kiislamu zilionekana kujali na kutetea maslahi ya Waislamu zilipigwa vita vya wazi Jumuiya hizo ni East African Muslim Welfare Society (EAMWS) na AlJamiatul Islamiyya fii Tanganyika.

Maasi ya Jeshi ya tarehe 20 Januari 1964 yalimpa fursa Nyerere kuwaweka kizuizini viongozi wa vyama vya wafanyakazi na Masheikh maarufu katika Tanganyika. Uvumi uliokuwepo ni kuwa Masheikh walikuwa wanapanga njama za kupindua serikali. Wanazuoni wengine walipewa notisi ya kuondoka nchini kama wahamiaji wasiotakiwa. Mfano wa hawa ni Sharif Hussein Badawiy na mdogo wake Mwinyibaba walirudishwa kwao Kenya.

Wajumbe wa mkutano mkuu wa Waislamu mwaka 1963 walipowasili Dar es Salaam baadhi yao (wateule) walikaribishwa na Nyerere kwenye chakula cha usiku katika Government House. Nyerere alitumia fursa hii kuwashauri wajumbe wale waanzishe jumuiya ya Waislamu wa Tanganyika ichukue nafasi ya EAMWS. Wajumbe hawa waliileta hoja hii mkutanoni. Kwa vile Mufti Sheikh Hassan bin Amir alikuw aamepata fununu hii, alikuwa amemfahamisha Katibu wa EAMWS wa Tabora mzee Waikela ambaye alikuwa mwanzilishi wa TANU huko Tabora na rafiki wa karibu wa Nyerere juu ya mpango huu. Nyerere alitaka ianzishwe jumuiya nyingine ya Waislamu wa Tanganyika ambayo itaongozwa na wanafiki wasio na haja ya kutetea maslahi ya Waislamu na Uislamu. Waikela kwa ujasiri mkubwa aliweza kuipinga dhana hii na kuwaonyesha wajumbe chanzo cha fikra hii na kutoa changamoto kuwa na aje Nyerere aeleze msimamo wake juu ya kadhia hii.

Baada ya jaribio hili kushindwa njama za chini chini za serikali kuihujumu EAMWS ziliendelea ambapo kuwekwa kizuizini kwa Masheikh mwaka 1964 kuliwafanya wengi wa viongozi wa EAMWS kujiweka mbali na jumuiya yao jambo lililosababisha matawi mengi ya jumuiya kudhoofika. Baada ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha, Adamu Nasibu aliyekuwa Katibu wa EAMWS tawi la Bukoba alisimama kulitafsiri azimio hili kwa mtazamo wa Qur-an kuliunga mkono azimio tena kwa mealezo kuwa liko sawa na Qur-an kulimfanya adamu Nasibu apate umaarufu mkubwa sana serikalini.

Mwaka 1968 17 Oktoba Adamu nasibu alitangaza mkoa wake (Bukoba) kujitoa kwenye EAMWS. Jambo hili lilipigwa debe magazetini na ktika radio ya serikali. Wakati haya yakiendelea viongozi wa juu wa EAMWS Tewa Saidi Tewa na Bibi Titi walikuwa wakipata kibano kikali na serikali ikiwa ni pamoja na kupoteza nafasi zao za uongozi serikalini na katika chama. Sheikh Hassan bin Amir aliondolewa Tanganzia bara na kupelekwa visiwani.

Hali hii ilitoa fursa nzuri kwa kundi lililoongozwa na Adamu Nasibu dhidi ya uongozi wa EAMWS kuumaliza kabisa umoja na mshikamano wa Waislamu.

Tarehe 12 – 13 Desemba 1968 kundi la Adamu Nasibu liliitisha mkutano uliokuwa na lengo la kujadili katiba ya jumuiya mpya ya Waislamu. Serikali ilihusika sana kuhakikisha mkutano huu uliofanyika Iringa unafanikiwa. Ni katika kikao hiki iliundwa BAKWATA; na kwa kutumia nguvu za madaraka iliyo nayo serikali iliifuta jumuiya ya EAMWS siku chache baadaye. Kisha kwa kutumia madaraka hayo hayo na kinyume cha sheria serikali ilikabidhi mali zote za EAMWS kwa BAKWATA. Kwa vile BAKWATA haikuwa na watendaji wenye uwezo wa kumiliki na kuendesha miradi ya Waislamu iliyokuwa chini ya EAMWS vyote hivi vilififia na hatimaye vingine kufa kabisa. Nyuba nyingi za wakfu mpaka hivi leo ziko mashakani kupotea na zingine zilishapotea kabisa.

Kwa vile Waislamu wengi hawakuwa radhi na kuundwa kwa BAKWATA walijiweka mbali na chomo hiki kipya. Kadhalika kushindwa kwa BAKWATA kuutetea Uislamu na Waislamu katika matukio mbali mbali kuliifanya izidikuwa mbali na watu. Mfano BAKWATA ilishindwa kulaani Sofia Kawawa alipoikashifu Qur-an (1988) badala yake ikawalani walioandamana kupinga kauli hiyo ya Sofia Kawawa. Vile vile Waislamu wa Mwanza walipodhulumiwa na sungusungu kwa kupigwa, kulazimishwa kuliabudu jua na misahafu kuchanwa ni Mufti wa BAKWATA aliyepewa redio kueleza kuwa yote hayo hayakuwa ya kweli na likuwa kilichochanwa sio msahafu bali ni kijiyasini tu!

Kwa vile Waislamu walikuwa na ghera ya kuendeleza Uislamu wao ilibidi kuanzisha vyombo mbali mbali vilivyosajiliwa serikalini na baadhi visivyosajiliwa.

Ilivyo njama dhidi ya Uislamu nchini Tanzania zimewekwa kistratejia sana kiasi kwamba inahitaji kuwa na jicho la ziada kuweza

kuzigundua. Mara nyingi matatizo yanayowakumba Waislamu ukiyachunguza utaona ni misuguano baina ya Waislamu wenyewe kwa wenyewe. Wenye agenda zao hubaki nyuma ya pazia wakielekeza nini kifanywe na waliowatuma kufanya Hujuma.

Mfano kuvunjika kwa EAMWS waliowekwa safu ya mbele ni Adam Nassibu, Sheikh Kassim Juma na Abdalllah Chaurembo hawa waliungwa mkono hadharani na mzee Rashidi Kawawa na marehemu Abeid Amani Karume (wote Waislamu). Nyerere aliyekutana na viongozi wa EAMWS (Tewa Said Tewa na Bibi Titi) wakiwa wamekwenda kumshitakia juu ya namna vyombo vya habari vya serikali vinavyoshabikia na kuukuza mgogoro uliomo ndani ya jumuiya yao, naye akawajibu kuwa "mmeamua kunipiga vita mkae tayari", haonekani kuhusika kabisa na kuvunjika kwa EAMWS.



# Zoezi la Sita

1. Bainisha mambo saba yanayotafautisha Uongozi wa kiislamu wakati wa makhalifa na utawala wa Kifalme uliowekwa badala yake.

2. Katika Dola ya Banu Umaiya, Umar bin Abdul Aziz alifanya mambo gani wakati wa utawala wake?

3. Taja maimamu wanne na kazi zao walizofanya wakati wa Tabiina.

4. Orodhesha vitabu mashuhuri vinavyoeleza Sunnah ya Mtume (s.a.w)

5. Eleza kwa ufupi kuhusu vita vya msalaba kwa kufuata mfululizo ufuatao:
   (a) Maana ya Vita vya Msalaba
   (b) sababu za kupiganwa vita hivyo
   (c) Matokeo ya Vita
   (d) Athari za vita hivyo

6. Eleza Wanaharakati waliojitokeza kufanya jitihada za kuhuisha uislamu kwa kufuata mfululizo ufuatao:
   (a) Jina la mwanaharakati
   (b) Mahala alipozaliwa na kufanya harakati hizo
   (c) Jumuiya aliyoasisi
   (d) Mambo aliyosimamia

7. Eleza namna Uislamu ulivyoingia Afrika Mashariki

8. Bainisha mbinu zilizotumiwa kuuhujumu Uislamu wakati wa Ukoloni na baada ya Uhuru